ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.

48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.

68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Nne – Tarehe 29 Machi, 2010

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa Kura ya Maoni. Ahsante.

Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kura ya Maoni na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Zahra Ali Hamad (Kny: Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Waziri Kivuli wa Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Upande wa Upinzani kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kura ya Maoni na mambo yanayohusiana na hayo. Ahsante sana.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 68

Uhalifu wa Kutumia Nguvu

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Hivi sasa kuna wimbi kubwa la uhalifu wa kutumia nguvu. Katika mwezi wa Februari, 2010 kumetokea kesi nne tofauti za mauaji. Kwanza, Kusini Unguja, katika wizi uliofanyika hoteli na mtu mmoja kufa. Pili, Donge Kaskazini Unguja, ambako mtu mmoja alichomwa kisu na kufa. Tatu, Kibweni, Magharibi Unguja, ambako walinzi walivamiwa na kupigwa mapanga na mmoja kufa. Nne, Kaskazini Pemba, kijiji cha Fundo ambako mwanamke mmoja na mwanawe mchanga waliuawa.

(a) Je, Mhe. Waziri, serikali ina mikakati gani maalum ya kukabiliana na vitendo vya uhalifu kama hivyo.

(b) Je, kwa mujibu wa uchunguzi wa Polisi uhalifu huu umefanywa na wahalifu wa ndani au nje ya Zanzibar.

(c) Je, serikali inatoa wito gani kwa wananchi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya WAziri Kiongozi – Alijibu:-

Bismillahi Rahmani Rahiym. Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 68 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Jeshi la Polisi limepokea taarifa za uhalifu ulifanyika katika mwezi Februari 2010. Matukio mengine manne yalielezwa yote yameripotiwa na kuchukuliwa taratibu za kisheria, kati ya matukio hayo ni mawili tu ndio yenye sura ya ujambazi ambayo ni:-

1. Mhe. Spika, tarehe 14/2/2010 katika eneo la Uroa Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja, watu wanaokisiwa watano walivamia Hoteli ya *SAMAKI LODGE* kwa lengo la kuiba. Watu hao walivamia na kumjeruhi kwa mapanga mmiliki wa hoteli hiyo. Katika kukabiliana na wavamizi hao walinzi walifanikiwa kumkamata mtuhumiwa mmoja na katika purukushani hizo, mtuhumiwa mmoja aliuawa wengine watatu walifanikiwa kutoroka.

2. Tukio la tatu limetokea tarehe 21/2/2010 eneo la Kibweni Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, ambapo wahalifu waliwavamia walinzi wa nyumba ya kuishi na kumuua mlinzi mmoja. Katika tukio hilo hakuna kilichoibiwa.

Mhe. Spika, matukio mengine ambayo hayana sura ya ujambazi ni:-

1. Tukio lililotokea Donge, Mkoa wa Kaskazini Unguja karibu na Daraja la Tinga Tinga. Mtu mmoja alikutwa amekufa ambapo baada ya uchunguzi imebainika kuwa amechomwa kisu, pembeni ya marehemu palikutikana ujumbe unaomaanisha kuwepo kwa madai kati ya aliyekufa na waliosababisha kifo hicho.

(2) Tukio lililotokea tarehe 21/2/2010 eneo la Fundo Mkoa wa Kaskazini Pemba, ambapo bwana mmoja amemuuwa mkewe na mwanawe mwenye umri wa miaka 9. Inasadikiwa sababu ya mauwaji haya ni wivu wa mapenzi kati ya wanandoa hawa wawili.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsane sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, Jeshi la Polisi limeanzisha mfumo mzuri wa ulinzi shirikishi au polisi jamii, kwa kuzingatia hayo wananchi huwa tayari kutoa msaada au maelezo kwamba pahala fulani kuna mtu anaonekana mwenendo wake si mzuri.

Je, Mhe. Waziri katika tukio lililotokea huko Uroa na jambazi sugu ambalo limeuwawa, anajua kwamba jambazi hili lilikuwa linatishia usalama wa wananchi mbali mbali. Pili jambazi hili limeshapelekwa na kesi kama tatu hajahukumiwa anaachiwa huru kwa mipango anayoifanya mwenyewe kwa mujibu wa uwezo wake. Namuomba Mhe. Waziri atueleze, masuala kama hayo wakati wananchi wanatoa taarifa zao na mtu anapochukuliwa hatua anafika siku mbili tu Mahkamani anaachiwa huru, huku si kuwavunja moyo wananchi na kusababisha ongezeko la ujambazi katika nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba Jeshi la Polisi limeanzisha ulinzi ambao unaitwa Polisi Jamii. Ulinzi huu umeanzishwa kwa makusudi ili kulisaidia Jeshi la Polisi kuweza kupata taarifa za wahalifu katika maeneo yetu mbali mbali.

Mhe. Spika, kupitia ulinzi huu wa Polisi Jamii umeweza kusaidia sana kupunguza matukio mbali mbali ya uhalifu ambayo yangeweza kutokea katika jamii yetu. Kwa hivyo, kwanza Mhe. Spika, naomba sana niwapongeze wananchi kwa kuitikia wito huu wa serikali kupitia Jeshi la Polisi na ndio maana kwa kiasi fulani pamoja na matukio yaliyotokezea, lakini katika *record* basi Zanzibar sasa hivi tunaongoza katika nchi ambayo ina matukio madogo sana ya uhalifu pamoja na ujambazi. Hii yote inatokana na kwamba wananchi sasa wanashirikiana na polisi kwa ajili ya kutoa taarifa na Jeshi la Polisi linachukua hatua mapema kabla uhalifu haujatokea.

Mhe. Spika, nikiendelea na swali lake ni kwamba, hili jambazi lililouawa katika tukio lile la ujambazi ni kweli Jeshi la Polisi lilipata taarifa kutoka maeneo mbali mbali kutokana na usugu wa jambazi hili. Jeshi la Polisi lilichukua hatua na zikafuata taratibu zikampeleka mpaka Mahkamani, lakini Jeshi la Polisi likishafikisha taarifa zake Mahkamani kwenye vyombo vya sheria inamaana kazi yake inakuwa imemaliza na kazi iliyobakia ni ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahkama.

Kwa hivyo, mtuhumiwa anapopelekwa polisi kwanza wananchi wanavyotakiwa sio baada ya kupeleka taarifa polisi iwe kazi yao imekwisha, wanapopeleka taarifa polisi mfano, fulani tunamtuhumu kwa ujambazi au fulani kafanya ujambazi, kwa hivyo, ili Mkurugenzi wa Mashtaka aweze kusimamia kesi ile vizuri basi wale wananchi wanatakiwa kuendelea

kusimamia kesi ile kwa kutoa ushahidi mpaka Mahkamani. Sasa wakati mwengine majambazi yanakuwa yanakamatwa baada ya taarifa za wananchi, lakini wananchi wale baada ya kutoa taarifa jambazi lile likishakamatwa kazi wanaiachia polisi wao wanaona kazi yao imemaliza.

Mhe. Spika, ndio maana wakati mwengine linapopelekwa Mahkamani ujambazi hili hata kama limeonekana limeuwa lakini kama hakuna shahidi ambaye ataweza kusimamia ushahidi wa kesi ndio mara nyingi utakuta anaachiwa. Kwa hivyo, ni kweli jambazi hili limeshapelekwa Mahkamani karibu mara mbili limeachiwa, lakini Mwenyezi Mungu sasa amepitisha rehema zake limekamatwa huko Uroa na limeuawa. Kwa hivyo, sasa hiyo labda ilikuwa ndio hukumu yake. Kwa sababu akipelekwa Mahkamani anatoka, hatusemi anatoka kwamba labda majaji wanakuwa wanakula rushwa au vitu vingine, hakuna, taratibu za ushahidi kama zinakuwa hazikukamilika pale Hakimu hana uwezo wa kuweza kumtia hatiani mtuhumiwa.

Kwa hivyo, tunawaomba sana wananchi Mhe. Spika, wajitahidi sana pale wanapompeleka mtuhumiwa polisi basi vile vile wasione tabu kwenda Mahkamani kuweza kutoa ushahidi. Ahsante.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri alipokuwa anajibu swali mama alikiri kwamba katika matukio manne, mawili yana sura ya ujambazi.

Katika kupunguza matatizo huwa jambo unalifanyia utafiti. Je, Mhe. Waziri huu ujambazi kwa utafiti wenu mtakaofanya ama mnaofanya majambazi hao ni wa ndani ya nchi ama wametokea nje ya nchi. Hilo la kwanza.

Pili, kwa kuwa bado masuala haya kila muda yanajirudia. Je, serikali ina mikakati gani juu ya kumaliza suala hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, nakiri kama alivyosema kuwa katika matukio haya kama nilivyoeleza hapo mwanzo kwamba katika matukio manne basi mawili ndio yenye sura ya ujambazi na mengine yalikuwa yanahusu suala la kudaiana na moja limehusiana na suala la mapenzi.

Mhe. Spika, ameuliza Mhe. Mwakilishi kwamba je, hawa majambazi ambao wanakuja kufanya vitendo vya uhalifu, baada ya uchunguzi wetu tumegundua wanatoka nje au ndani ya nchi. Mhe. Spika, suala hili kwanza watuhumiwa wa ujambazi wanakuwa ni Wazanzibari wao wenyewe. Hata inapotokea kwamba kuna wengine kutoka nje ya Zanzibar basi katika uchunguzi wetu tunagundua kwamba wale wanaotoka nje basi wanakuwa wanakaribishwa na wale

wananchi wa hapa hapa Zanzibar. Kwa hivyo, bado kazi tuliyokuwanayo tujaribu kama tulivyozungumza tushirikiane na Jeshi la Polisi ili hawa wanaoshirikiana na majambazi kutoka nje basi tuweze kuwadhibiti ili haya madhara yasiweze kutokea.

Mhe. Spika, swali jengine ni suala la serikali kuwa tuna mkakati gani. Mhe. Mwakilishi mmoja kati ya mkakati tuliouanzisha kama nilivyosema katika swali la msingi ni huu utaratibu wa kuanzisha Polisi Jamii.

Mhe. Spika, Zanzibar ni ndogo sana kijiografia, tunajuana na anapoingia mgeni basi mtaa mzima unajua kwamba leo katika mtaa wetu ameingia mgeni. Mhe. Spika, kama Zanzibar ni ndogo na sote tunajuana mitaani basi mtu yeyote mwenye tabia za uhalifu au vitendo vyovyote vibaya basi mara nyingi tunakuwa tunafahamu katika mitaa yetu.

Lakini tatizo letu kama nilivyozungumza Mhe. Spika, hata kama wakati mwengine tunajua kuwa fulani ni mkorofi mtaanii kwetu, suala la kwenda kuripoti Kituo cha Polisi na kwenda kusimama katika ushahidi hilo ndio tatizo kubwa linalotukwaza. Wengine wanaogopa majirani zao, wengine jamaa zao lakini wengine wanasema aah! nitakuja kuonekana mimi mbaya. Sasa ili tuweze kuishi katika hali ya amani na utulivu tuondoe mambo ya muhali tuwafichue wahalifu ili tuweze kuishi katika hali ya amali.

Kwa hivyo, mkakati wa serikali sasa hivi kupitia Jeshi la Polisi ni kuwa limo katika maboresho makubwa sana ya kuweka sawa namna gani mwendo au muundo wa Jeshi la Polisi. Moja katika mkakati wake ili kurahisisha hizi shughuli basi ni kuanzisha Polisi Jamii na ndio maana kama nilivyosema mwanzo matukio ya ujambazi sio kama Zanzibar yasingetokea, yangetokea lakini kuna shughuli nyingi ambazo zinafanywa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi, kwa hivyo ile mipango inakuwa inaharibiwa na ndio maana sasa hivi majambazi wameanza kuvunjika moyo wameanza kukimbia Zanzibar. Ahsante.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, nakushukuru na naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo Mahkamani na kwa ushahidi wa kesi zinavyoendeshwa, wahalifu wengi wanatoka Tanzania Bara ingawa Wazanzibari wamo.
Je, serikali haioni kwamba wahalifu hawa wanaingia Zanzibar ni kwa sababu tu hakuna mchakato wa kuwadhibiti wakati wa uingiaji nchini.

Pili serikali haioni kwamba sasa kuna haja ya kuweka utaratibu wa hawa wageni wanaoingia angalau wajulikane wanaingia lini na wataondoka lini.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Abubakar Khamis kwamba katika takwimu zilizoko Mahkamani ambazo mimi sikuwahi kuzifanyia utafiti, anasema kesi nyingi zinazohusiana na masuala ya ujambazi basi zinawahusisha wananchi wanaotoka Tanzania Bara. Sasa ameuliza kwamba kuna mkakati gani baada ya kuona kwamba wahalifu wengi wanatoka Tanzania Bara kwa kuweza kuanza kudhibiti na kuweza kujua ni nani wameingia na nani ametoka ili kuweza kuweka utaratibu mzuri.

Mhe. Spika, hili suala zamani lilikuwepo kwamba wananchi wa pande zote mbili sio wa Tanzania Bara tu, hata Wazanzibari wanapokwenda Tanzania Bara. Kulikuwa kuna utaratibu wa kutumia vitambulisho au paspoti ambazo mtu akishafika bandarini au uwanja wa ndege anagongewa ili kuonekana kwamba huyu mtu ameingia. Sasa baadae hili suala likafanyiwa marekebisho. Kwa hivyo, lile suala la udhibiti wa kutumia paspoti au vitambulisho likaondoka.

Masuala haya ya usalama ni kweli yanakwendsa na takwimu, sasa hili suala tutazidi kulifanyia utafiti kama alivyosema Mhe. Abubakar, tutajaribu kuangalia utafiti. Kama ni kweli kuwa wahalifu wengi wanatoka Tanzania Bara basi tutajaribu kukaa serikali mbili tuangalie sasa, kwa sababu serikali zote mbili siamini kama wanapenda matukio haya ya uhalifu. Kwa hivyo, tutakaa sote na kwa bahati nzuri tuna vikao vyetu vile vya kuzungumzia kero za muungano.

Sasa kama kuna mambo ya uhalifu yanayosababishwa na wananchi wetu wa pande zote mbili suala hili tunaweza tukashauriana katika vikao na tukiona kwamba litaweza kutusaidia basi tunaweza tukashauri serikali zetu mbili kwamba turejeshe ule utaratibu. Kwa kuwa sasa hivi Zanzibar tunavyo vitambulisho vya Uzanzibari na wenzetu wamo katika mchakato wa kuanzisha vitambulisho vya kitaifa na vitambulisho vile vitaweza kumu-*identify* mgeni na mwenyeji. Kwa hivyo, baada ya kuweza kufanya mchakato huo nafikiri zoezi hili Mhe. Abubakar linaweza likenda vizuri sana, kwa sababu mtu yeyote atakayepita bandarini au uwanja wa ndege atatakiwa aoneshe kitambulisho chake, akionesha kitaweza kurikodiwa na tarehe ngapi ameingia, tarehe ngapi ametoka na hata kama linatokea tukio la ujambazi basi mtu yule anaweza kudhibitiwa.
Mhe. Spika, tayari kuna wananchi ambao walikiuka masharti ya Zanzibar waliweza kuzuiliwa wasiingie tena Zanzibar. Kwa hivyo, bado Serikali ya Zanzibar ina nguvu za kisheria ya kuweza kumdhibiti mtu yeyote ambaye mkorofi asiingie Zanzibar na agizo hilo litatekelezwa mara moja.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kama nilivyosema kuwa mkakati kama nilivyomwambia Mhe. Abubakar na hizo takwimu tutajaribu kuzifuatilia halafu tutajaribu kupeleka mapendekezo yetu. Lakini naamini baada ya kukamilika zoezi la vitambulisho vya kitaifa basi zoezi hili litakuwa jepesi sana kuweza kulitekeleza. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 1
Kutofautiana kwa Ada za Maegesho ya Magari (*Car Parks*)
Katika Mji wa Zanzibar

Mhe. Ali Abdalla Ali (Kny: Mhe. Amina Iddi Mabrouk) – Aliuliza:-

Naipongeza wizara kupitia Manispaa kwa kuanzisha Maegesho ya Magari katiak mji wetu kwa nia ya kukusanya mapato na usalama wa magari. Kinachoshangaza ni kutofautiana kwa ada za maegesho hayo ndani ya Manispaa moja. Mfano, Forodhani hutozwa shilingi 1,000/-, Darajani nyuma ya Marikiti hutozwa shilingi 500/= na sehemu zilizobaki hutozwa shilingi 250/- kwa gari moja.

(a) Je, Mhe. Waziri, vigezo gani vimetumika kutoza ada tofauti.

(b) Je, Manispaa hukusanya kiasi gani kwa mwaka mmoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 1 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Mwakilishi kwa kutupongeza kwa hatua yetu ya kuimarisha maegesho ya magari katika mji wetu.

(a) Mhe. Spika, vigezo vinavyotumika katika ada tofauti ya maegesho hayo ni kwamba huwa tunatoza kati ya shilingi 1,000 katika eneo la Forodhani ili kudhibiti uingiaji na kupunguza msongamano wa magari katika eneo la Mji Mkongwe na hasa eneo la bustani ya Forodhani kwa sababu ya usalama na pia kwenda sambamba na uhifadhi ya wa Mji Mkongwe.
Pia katika eneo la Darajani nyuma ya Marikiti huwa tunatoza shilingi 500/- badala ya shilingi 1,000/- kutokana na mahitaji ya jamii kuwa mengi katika eneo hilo la Mji Mkongwe.

Kwa maeneo yaliyobaki kiwango kinachotozwa ni shilingi 250/-.

(b) Kwa wastani wa Baraza la Manispaa linakusanya kiasi cha shilingi milioni 18 kwa mwaka kwa huduma hiyo ya maegesho ya magari.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Spika, pamoja na majibu yake Mhe. Waziri napenda anijuilishe kwamba ni maeneo gani ambayo kama Manispaa wenyewe wameanzisha kwa ajili ya maegesho ya magari, mbali na hizi sehemu ambazo wanakuwa wakipandia pandia tu.

(b) Mhe. Spika, Benki ya *FBME* ilihama katika eneo moja kuja eneo jengine, katika kufanya hivyo ili kuwa-*safe* wale wateja wao wamejijengea pia *parking* kwa ajili ya wale Waheshimiwa ambao watafika pale kwa ajili ya shughuli zao katika benki yao. Sasa tunaona watu wa manispaa wakikusanya fedha pale, ni sheria ipi inayoipa mamlaka ya kukusanya ada za maegesho katika taasisi kama hizo ambazo mtu amejijengea kwa ajili ya shughuli zake kurahisisha kwa wateja wake lakini wanakuja wao kukusanya. Ni sheria ipi inayowapa mamlaka haya.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, maeneo ambayo tunashughulika nayo ni maeneo ya Mji Mkongwe kwa ujumla ndio sehemu ambazo zinatozwa kodi ya *parking*. Lakini sehemu zilizobakia huku Vikokotoni, Darajani nyuma, Mlandege na kwengineko huko bado hatujaweza kuingia. Lakini katika maeneo yote ya Manispaa hutozwa kodi hiyo.

Swali (b) maegesho ya Benki ya *FBME* ni eneo ambalo waliliomba benki hii na baadhi ya sehemu wamekubaliwa kuweka maegesho kwa wanaokuja wote kwa shughuli za benki. Sheria iliyotufanya kuweza kukusanya ni sheria ile ile ambayo tunaitumia katika Manispaa ya Mji Mkongwe.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa mujibu wa kodi hizi ambazo zinatozwa na kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri inaonekana kwamba pana uvujaji mkubwa wa kodi hizi. Kwa mfano, kukodisha *park* moja kwa shilingi 1,000/- na kwa mujibu wa ukubwa wa nchi yetu na gari zake labda wastani kwa mwezi tunaweza kupata shilingi milioni 3. Hivyo haoni kuwa suala hili ni bora akaliachia kampuni au *ZRB* ili hii kodi isipotee bure. Kama upo uwezekano lini rai hii itakubalika kupelekwa *ZRB* au kukodisha katika kampuni ambazo zinaweza zikakusanya pesa vizuri.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, mpaka sasa hivi sijaweza kuthibitisha kama kuna uvujaji wa mapato katika fedha zinazopatikana kutokana na maegesho ya magari. Mhe. Ame Mati kama unazo kumbukumbu zozote au vielelezo vyovyote kuhusiana na suala hili ungekuja tukashirikiana tukahakikisha hizi kodi tunazikusanya zote na hazipenyi.

Mhe. Spika, kwa hivyo, namthibitishia kwamba hakuna mapato mpaka sasa hivi yanayopotea. Isipokuwa sisi sasa hivi bado tunaendelea kufanya utafiti zaidi kuangalia hali ikoje katika utozaji wa kodi kama zinazotozwa ni sawa au ziongezwe au zisiongezwe.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Kwa kuwa wizi wa vifaa vya gari hapa Mjini Unguja umekithiri ni mkakati gani unaopangwa na Manispaa wa kuwawekea watu sehemu za kuegesha magari hasa wakati wa usiku katika mitaa mbali mbali ya Unguja, kwa ulinzi wa magari yao pamoja na kuwekewa malipo ya kulipa ili gari zao zikae katika hali ya usalama.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, kwanza nataka nimpongeze Mhe. Mwakilishi kwa mara zote tunapokutana popote pale huwa ananishikilia kuhusiana na maeneo ya kuegesha magari, usafi wa masoko, usafi wa mji, taa haziwaki na mengineyo. Kwa hivyo, nakushukuru sana nab ado ningestaajabu kwamba suala hili linamalizika hukupata hata sehemu ya swali la nyongeza lakini bahati nzuri umepata.

Mhe. Spika, ukweli suala la *parking* kwa maeneo ambayo wananchi wetu wanakwenda ili kuweka usalama wa magari hayo, sisi wengine si watembeaji sana wa usiku, lakini tunahitaji ushauri zaidi wa kuliangalia suala hili la ulinzi wa magari ambayo yanakuwa yameegeshwa sehemu tofauti katika mambo ya shughuli mbali mbali, utakuta gari zile zinaibiwa vioo na vitu vyengine. Kwa hivyo, hili linataka tushirikiane zaidi kuangalia tutaitumia kodi kama ni fimbo, pia tutaitumia kodi kama ni kielelezo cha kuweka ulinzi katika gari hizi ambazo zinakaa katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, ukweli hapa kodi inaweza ikapatikana hasa wakati wa usiku kuna maeneo kama nilivyoyataja hayo ambayo gari nyingi huwa zinaibiwa vifaa hivyo. Kwa hivyo, tukapata kuweka askari wa Manispaa kulinda na wakati huo huo na wao wananchi wakapata kutoa kodi ambayo itaisaidia Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Nam. 47

Mradi wa Ukusanyaji Maji ya Mvua

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Mradi wa ukusanyaji wa maji ya mvua *(Rain water havesting)* hivi sasa unatimia umri wa miaka kumi (10) tangu kuanzishwa. Baadhi ya maeneo ya majaribio ya mradi huo ni Kijiji cha Bumbwini Matetema, Wilaya ya Kaskazini "B", na Makunduchi na Mtende Wilaya ya Kusini.

Mhe. Waziri, kwa kuwa mradi huu unasaidia sana wakulima, Serikali ina mikakati ya kuuendeleza.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 47 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara yangu inakiri kwamba kazi ya ukusanyaji wa maji ya mvua na kuyatumia kwa kilimo ni jambo muhimu na linasaidia sana wakulima. Sisi katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira tutaendelea kufanya utafiti zaidi kwa maeneo mengine ili wakulima zaidi wafaidike na hatua hii. Hivi sasa mbali na maeneo yaliyotajwa kwa Unguja, lakini pia kwa Pemba kazi hii imestawi zaidi na sasa hivi tunaandaa wataalamu zaidi wa fani hii kuweza kuwasaidia wakulima wengi zaidi.

Mhe. Spika, Wizara imetayarisha Mpango maalum wa uvunaji maji kwa matumizi ya kilimo na kuwasilisha kwa wafadhili kwa ajili ya kupata fedha za kutekeleza mpango huo.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika jibu lake ametaja kwamba katika kisiwa cha Pemba kuna hatua ambazo zimeanza katika suala hili la uvunaji wa mvua. Lakini bonde la Mangwena lililopo Wete ni bonde la umwagiliaji maji ambalo vyanzo vyake vya maji vinatokana na vilima vilivyoko katika Shehia za Kizimbani, Gando, Wete na Bopwe.

Kwa sababu mara nyingi bonde hili hukosa maji ya umwagiliaji na wakulima wakapata tabu sana. Je, Mhe. Waziri na wizara kwa jumla ni mkakati gani wa kuona kwamba vilima vile angeweza kuvitumia vizuri kuona kwamba anavuna maji ya mvua na kulisaidia lile bonde ili kuondokana na uhaba wa maji ya mvua hasa katika kipindi cha kiangazi kikubwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika jibu mama kwamba lengo kuu la serikali sasa hivi ni kuhakikisha kwamba tunaelekea katika kilimo kwanza cha umwagiliaji. Lakini la pili nilisema kwamba mchakato umeanza mkubwa sana zaidi kule Pemba na sasa hivi tumo katika matayarisho kuomba fedha zaidi kwa wafadhili ili kuhakikisha katika maeneo kama hayo aliyoyataja ya Mangwena tunapata kuyakusanya maji kwa ajili ya kurejesha katika kilimo.

Kwa sababu kwa mfano mvua za masika sasa hivi zinazonyesha tunapata maji mengi lakini yanakwenda pwani, sasa lengo letu hatutaki tuyaachie maji yaende pwani. Pia tumo katika mipango ya kuhakikisha kwamba mito yetu tunaizungusha kwa sababu vianzio vyetu vya maji vinakwenda pwani, tunataka sasa maji yawe yanazunguka yanarudi katika maeneo ya kilimo. Hayo ndio malengo makubwa ya serikali na tumo katika kutafuta wafadhili kwa ajili ya kazi hiyo. Pale tutakapokuwa tunapata fedha serikali tutakuwa tunaendelea kuifanya kazi hiyo.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kuna mchakato wa kuanzisha sehemu za ukusanyaji wa maji huko Pemba. Anaweza kutuambia Mhe. Waziri wamechagua sehemu gani na gani kuweza kuanzia shughuli hiyo na mradi huo waliokusudia kuufanya katika makisio yao utachukua kiasi gani cha fedha.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, maeneo ya Pemba ambayo tayari sasa hivi tumeanza kukusanya maji tuna Weni, Kinyakuzi, Saninga, Tibirinzi na Mipopooni. Lakini kuhusu fedha tutatumia kiasi gani hili nitalijibu kwa maandishi kwa sababu sikujitayarisha.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kujibu zaidi swali la nyongeza la Mhe. Mohamed Ali Salim. Sehemu ambazo zinashughulikiwa kwa jumla nafikiri tumezitaja. Lakini kuhusu gharama hii kama tulivyosema katika jibu letu mama kwamba tunashirikiana na wafadhili ili kupata fedha za kuendeleza mradi huu. Kwa hivyo, kwa wakati huu tutashindwa kujibu pesa ngapi hasa kwa sababu mpaka tuzipate. Lakini hizo tulizozipata kwa sasa hivi na kuendeleza miradi hii, basi hizo tutaweza kuzileta kwa maandishi.

Mhe. Ame Ussi Juma: Mhe. Spika, kabla sijajibiwa swali langu nina maelezo kidogo tu. Kwa kuwa Mhe. Waziri ni mtu msikivu na muungwana anayejali maendeleo ya nchi yetu. Kwa hivyo, juzi swali hili ameshanipatia ufumbuzi wa skuli hiyo ambayo niliitaja. Sasa tunachongoja kwake ni utekelezaji. Swali naliondoa.

Nam. 62

Mabanda ya Skuli yaliyojengwa na Wananchi

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 19

Uhaba wa Wafanyakazi - Kitengo *Ultra Sound* Mnazi Mmoja

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza**:-**

Kitengo cha *Ultra Sound* ni muhimu sana kwa matibabu ya kisasa kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa uhakika wa afya za wagonjwa. Lakini kitengo hicho kina upungufu wa wafanyakazi, hasa baada ya mtaalamu wake mmoja kufariki.

Je, Mhe. Waziri, Wizara yako imechukua hatua gani kuongeza wataalamu wenye ujuzi kwa kutosha kuendesha kitengo hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 19 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika kuongeza wataalam wenye ujuzi wa kutosha wa *Ultra Sound*, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Taasisi ya *World Medical Colours* ya Italy iliendesha mafunzo ya miaka mitatu ya *Ultra Sound* ambapo wataalam hao kutoka Italy waliendesha mafunzo hayo hapa hapa nchini na hivi karibuni wafanyakazi wanne wakiwemo madaktari wawili walihitimu mafunzo hayo.

Aidha, Wizara yangu ina mpango wa kusomesha awamu nyengine ya wataalam wa *Ultra Sound* kwa kuwatumia wataalam hao wa Italy kuja hapa nchini. Vile vile Wizara yangu ina mpango wa kuwapeleka wafanyakazi wengine huko Uganda kwa ajili ya mafunzo hayo.

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kabla ya yote kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa juhudi yake kubwa ya kung'arisha na kufanyia ukarabati katika majengo haya ya hospitali.

Mhe. Spika, mnamo mwezi wa Oktoba kuna mfanyakazi mmoja wa kitengo hiki alifariki baadhi ya wagonjwa wengi wakawa wanapata usumbufu kwa

kusimama na choo kidogo milangoni mpaka ikawa inavuja pale. Je, tokea muda ule baada ya kufariki huyu aliwahi kutafuta mtaalam mwengine wa kusaidia kazi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwanza tuzipokee pongezi zake alizotupa katika kuboresha huduma zetu za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Tunazipokea pongezi hizo kwa furaha kubwa kwa sababu hiyo ndio juhudi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nataka kusema kwamba hili suala ni kama tofauti kidogo. Kwa sababu suala la vyoo vidogo huwa vinapelekwa maabara. Hili ni suala la maabara na wafanyakazi wa maabara wapo na bado wanaendelea. Hata kama alifariki mfanyakazi huyu kwa huku basi itakuwa bado wafanyakazi wengine wapo.

Suala la *Ultra Sound* naona kama halihusiani na kupeleka choo kidogo. Kwa hivyo, nahisi hili suala kidogo ni tofauti. Ningependa tu kumfahamisha kwa sababu masuala yote ya choo kidogo yanapelekwa maabara.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kidogo niongezee. Nilivyomfahamu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Amani i kwamba hivi sasa tuna upungufu wa wataalam wa *Ultra Sound* baada ya Ndugu Moh'd Haji kufariki dunia.

Mhe. Spika, sasa hivi tuna mahusiano mazuri na ndugu zetu wa Italy wanaitwa *World Medical Colours* ambao hao wanawafundisha wafanyakazi wetu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Unguja na Pemba huwa wanakuja hapa na sasa hivi wamekamilisha muda wa miaka mitatu.

Saba tumewafundisha Pemba na Unguja tumewafundisha sita. Wawili ni madaktari Dk. Khadija na Dk. Hassan. Wengine wanne ni Ndugu Khamis Abdulrahman, Ndugu Salma Suleiman na Ndugu Mwana Omar na huyu marehemu. Kwa hivyo hawa tunao. Pamoja na mwengine yupo Hospitali ya Mwembeladu Ndugu Ashura ambaye amefundishwa na Wafaransa.

Sasa upungufu ni kweli upo kwa sababu mahitaji ni makubwa lakini tumefanya utaratibu mwengine kwamba hawa watakuja tena kuwafundisha wafanyakazi wengine na isitoshe tutapeleka wengine Uganda. Kwa hiyo, hili tatizo baada ya muda mfupi litatatuka na hakutokuwepo tena na watu kupata haja ndogo au kubwa pale. Kwa sababu tutafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba tutalitatua tatizo hili kwa haraka iwezekanavyo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, *Ultra Sound* ni muhimu sana hasa kwa wanawake wajawazito. Ukizingatia kama wananchi wa Micheweni wanapata tabu sana kutoka Micheweni kufuatilia *Ultra Sound* Chake Chake. Je, Mhe. Waziri ana mpango wowote ule wa kuwawekea wananchi wa Micheweni *Ultra Sound* ili kupunguza msafara mrefu. Ikiwa hakuna je, ni lini anafikiria kufanya hivyo.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kweli sasa hivi wanaohitaji Ultra Sound Hospitali ya Micheweni wanakwenda Chake Chake ambako tuna wataalam watatu wa *Ultra Sound*. Mhe. Spika, tunataka kuangalia kwamba pia Micheweni, Vitongoji na kwengineko kuweka *Ultra Sound*. Kwa hivyo, *inshaallah* jambo hili tutalichukua na tutalifanyia kazi ili kuondosha usumbufu kwa watu wa Micheweni.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, ni jambo kufurahisha kuwa tumeleta wataalam kuja kuwafundisha madaktari wetu utaalam wa *Ultra Sound*.

(a) Je, mafunzo haya yaliyotolewa ni ya daraja gani.

(b) Kwa kuwa wameshamaliza mafunzo yao hawa wa awamu ya mwanzo. Je, wameshapata vyeti vyao vinavyohusika.

(c) Baada ya kumaliza kwao Mhe. Waziri anaweza akatwambia kawagawa vipi, katika hospitali gani, wangapi wangapi.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwanza vyeti wamekwishapewa wamekamilisha miaka mitatu ya mafunzo. Hawa wataalam kutoka Italy huwa wanakuja wanawafundisha Pemba, wanakuja Unguja wakisha wanarudi kwa vitendo. Maradhi yote wanaoneshwa na wakiingia tu wenyewe wanakusoma wanakuonesha picha na wanakuandikia ripoti. Isitoshe Dk. Khadija amekwenda mpaka Italy huko huko Milano.

Mgawanyo tulioufanya Pemba Chake Chake watatu, Wete wawili, Mkoani mmoja na mmoja kenda kusomea Udaktari. Unguja wako *Mnazimmoja Hospital* wote sita.

Nam. 39

Kombe la Dunia Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza**:-**

Mnamo tarehe 20/11/2009, Kombe halisi la Dunia liliingia Zanzibar na kupokelewa na Mhe. Naibu Waziri Kiongozi kwa niaba ya Mhe. Rais hadi viwanja vya Forodhani ambapo Wazanzibari walipata nafasi ya kuliona. Mbali na kombe hilo kudhaminiwa na Kampuni ya vinywaji baridi ya Coca Cola kwa kushirikiana na Kituo cha Radio binafsi cha Zenj FM.

(a) Je, Serikali ilitumia fedha kiasi gani katika ziara hiyo ya Kombe la Dunia.

(b) Serikali imejifunza nini kutokana na ujio wa Kombe la Dunia hapa nchini.

(c) *ZFA* kama mdau mkubwa na muhimu kwa masuala ya mpira wa miguu, walishirikishwa na kushiriki kwa kiwango gani wakati wa ziara hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 39 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa mnamo tarehe 20/11/2009 Kombe halisi la Dunia la *FIFA* lililetwa hapa Zanzibar na kupokewa na Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Muchezo kwa niaba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

(a) Mhe. Spika, katika ziara hiyo ya Kombe la Dunia la *FIFA* hapa Zanzibar, Serikali haikutumia fedha zake, kwani gharama zote za shughuli hiyo zilichangiwa na wadhamini na wafadhili mbali mbali wakiwemo wafanyabiashara maarufu hapa Zanzibar pamoja na Kampuni ya Coca Cola Zanzibar.

(b) Mhe. Spika, ujio wa Kombe la Dunia la *FIFA* hapa nchini umetufunza mengi na kutupa moyo ili tuendelee na dhamira yetu kuu ya kupata uwanachama wa kudumu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu wa Dunia *(FIFA)* ili nchi yetu ya Zanzibar iweze kushiriki moja kwa moja katika

kuliwania kombe hilo la mchezo unaopendwa zaidi kuliko michezo yote mingine duniani.

Mhe. Spika, napenda kunukuu Gazeti la Zanzibar Leo la tarehe 26 Machi, 2010 linalowanukuu Mawaziri wote wawili wa Habari, Utamaduni na Michezo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kapteni George Huruma Mkuchika na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo wa Zanzibar, Mhe. Ali Juma Shamuhuna wakiandaa mikakati rasmi ya kuipeleka Zanzibar *FIFA* na kikao kitakachofanyika hapo baadae mjini Zurich, Switzerland juu ya kuipatia uwanachama wa kudumu Zanzibar katika *FIFA*.

(c) Mhe. Spika, katika maandalizi ya kulipokea Kombe la Dunia la *FIFA* Wizara iliunda Kamati Maalum iliyoshirikisha watendaji mbali mbali kutoka taasisi za Serikali na za binafsi ili kuratibu ujio wa kombe hilo hapa nchini na miongoni mwa Wajumbe wa Kamati hiyo walikuwemo Wajumbe wawili kutoka Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar *(ZFA)* kati ya wajumbe kumi. Hiyo ni sawa sawa na asilimia 20 ya wajumbe waliokuwepo kutoka *ZFA* ambao wanaiwakilisha moja kwa moja *ZFA* Taifa pamoja na *ZFA* – Wilaya ya Mjini katika kamati hiyo ya kupokea Kombe la Dunia hapa Zanzibar.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, wafadhili waliolidhamini kombe hili kuja Zanzibar waliamua kuitumia redio binafsi ya Zenj FM kutangaza moja kwa moja taarifa za kombe lile na wananchi wakafaidika. Ni kwa nini wakachukua uamuzi huo wasichague Sauti ya Tanzania Zanzibar kutangaza kombe lile.

Swali (b) nilimsikia kiongozi mmoja wa *ZFA* akilalamika kwamba kwenye mapokezi ya kombe lile hata wao hawakuzingatiwa kupangiwa sehemu ya kukaa, protokoli haikuzingatiwa na wakaachwa wamesimama hadi kumalizika kwa sherehe ile. Ni kwa nini.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwanza naomba nimkatalie kwamba Zenj FM haikuwemo katika orodha ya wadhamini wote waliodhamini Kombe la Dunia hapa Zanzibar. Orodha kamili tunayo na Zenj FM sio mmoja wapo. Zenj FM kama redio binafsi waliamua wao wenyewe kutoa matangazo moja kwa moja kupitia simu ya mkononi kutoka viwanja vya Forodhani na tokea kupokea mpaka kufika mwisho.

Sauti ya Tanzania Zanzibar wao katika mipangilio yao ya kazi ya kawaida waliamua kutoa taarifa hizo kupitia taarifa zake za habari na taarifa mbali mbali za matangazo ya ujio wa Kombe la Dunia kabla halijafika Zanzibar.

Kwa hiyo, Zenj FM sio mfadhili mmojawapo wa Kombe la Dunia hapa Zanzibar.

Jibu (b) kuhusiana na *ZFA* kupata sehemu ya kukaa. Hilo Mhe. Spika, naomba nikatae kwamba si kweli na sisi hatukupokea malalamiko yoyote baada ya shughuli hiyo kwamba *ZFA* walikosa sehemu ya kukaa. Ile kamati iliyoundwa ambayo ilikuwa na wajumbe wawili kutoka *ZFA*, yaani *ZFA* Taifa na *ZFA* Wilaya ndio ilikuwa inapanga mipango yote ya kukaa na namna ya Kombe la Dunia ziara yake itakavyokwenda pamoja na lile eneo la Forodhani viti vyote vilivyopangwa na kadhalika.

Sasa sidhani kama kuna kasoro hiyo ikiwa wajumbe wao wamo mle katika ile kamati na mabosi wao wakaja kukosa pahala pakukaa. Hilo haliwezekani. Mipango ya namna ya kukaa na kupiga picha na Kombe la Dunia ilikuwa imekamilika na ilifanywa kwa ufasaha mkubwa sana. Kwa hiyo, tunavyofahamu sisi hatuna taarifa yoyote kwamba kuna kiongozi yeyote wa *ZFA* au mtu yeyote aliyekosa nafasi ya kukaa.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa kushiriki kikamilifu katika sherehe ambayo ni ya historia katika nchi yetu kwa niaba ya Mhe. Rais.

Lakini pia Mhe. Spika, nimpongeze Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, niwapongeze Baraza la Michezo, *ZFA* na Serikali kwa jumla, hasa tukizingatia kwamba ujio wa kombe hili ni heshima ya nchi yetu.

Kwa kuwa tumepata heshima hiyo na changamoto tunaelekea kwamba tumo katika mchakato wa kuomba kuwa mwanachama katika Shirikisho la Soka Duniani. Je, wizara kupitia Baraza la Michezo na kupitia *ZFA* lina mkakati gani hivi sasa wa kuhakikisha kwamba tunapata viwango vizuri kwa wachezaji wetu.

Lakini pia si vibaya kwa wananchi wetu, wachezaji wetu au makocha wetu wazalendo wanapatiwa mafunzo ya kutosha, ili kujiimarisha na huko mbele tunakoelekea hasa tukitegemea kwamba Mwenyezi Mungu akipenda iko siku na sisi tutakuwa moja katika timu ambayo inashiriki katika Kombe la Dunia.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwanza kabisa katika huo mkakati naamini Mhe. Waziri ameshakusikia na wewe ukiwa kama Mjumbe mmoja wapo wa Baraza la Michezo la Taifa Zanzibar nawe pengine utapata bahati ya kushiriki katika huo ujumbe utakaokwenda huko Zurich, Switzerland kwenda kuzungumza masuala ya *FIFA.*

Kwa kuwanukuu Waheshimiwa Mawaziri wawili katika mazungumzo yao pamoja na Gazeti la Zanzibar Leo basi ziara wamesema watajumuisha pia nayo *TFF* ikiongozwa na Rais wa *TFF* Leodgar Tenga pamoja na mwanamichezo mashuhuri ambaye alikuwa kiongozi Ndugu Said El Maamry. Kwa hiyo, natarajia kutoka Zanzibar Mhe. Waziri ameshalisikia hilo.

Lakini la pili Mhe. Spika, kuhakikisha viwango vizuri vinapatikana. Ninaamini Mhe. Waziri alitumia busara na hekima kubwa sana za kuchagua viongozi wa Baraza la Michezo na miongoni mwao mmoja wapo ni muuliza swali hili Mhe. Ali Suleiman Ali. Sasa nadhani hili Mhe. Spika, linatakiwa litokane na *ZFA* moja kwa moja pamoja na Baraza la Michezo kuja kwetu sisi kutwambia kwamba hii ndio mikakati yetu tuliyopanga kuongeza viwango.

Jana Mhe. Waziri katika matamshi yake pale Uwanja wa *Mao Tse Tung* wakati akiibua vipaji mbali mbali vya Zanzibar alitamka kwamba tunaleta watu kwa ajili ya kutumiwa ikiwemo pamoja na kocha kutoka nchini Misri ambaye ni mtaalam aliyekuja badala ya yule kocha aliyekuwepo mwanzo Ndugu Badr El Din, huyu anaitwa Abdulfatah. Waliulizwa viongozi pia vipi mnamtumia kocha huyu ili kuwaendeleza watoto hawa tuliokuwa tunawazindua jana wenye vipaji mbali mbali.

Mhe. Spika, hili zaidi lianatakiwa linatokana na ZFA wenyewe pamoja na wajumbe wa Baraza la Michezo. Mimi nashukuru sana kwamba mmoja wapo wa mjumbe mkuu wa Baraza la Michezo la Zanzibar ni Mhe. Ali Suleiman Ali. Kwa hivyo, kazi kwake, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Naelewa kwamba kuanzia sasa Mhe. Ali Suleiman Ali anatayarisha suti ya kuingilia Zurich. Swali limechukua muda mrefu kidogo, tuendelee na maswali yanayofuata.

Na. 29

Tatizo la Maegesho ya Magari Kwenye Bandari ya Malindi

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

(a) Mhe. Waziri, baada ya kazi nzuri na ya kupongezwa ya ujenzi wa Gati ya Malindi, Shirika lina mkakati gani wa kuondoa tatizo la pahala pa kuegeshea magari kwenye Bandari ya Malindi?

(b) Tulielezwa kuwa ikihama Afisi ya Mkaguzi wa Magari (*silver*) eneo hilo litatumika kwa maegesho ya magari. Je, mpango huo ukoje?

(c) Kwa kuwa hivi sasa ni zaidi ya nusu mwaka na utekelezaji wa jambo hilo haujafanyika. Je, tatizo la lililokwamisha zoezi hilo nini?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 29 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kutokana na ukosefu wa maeneo ya wazi katika eneo la Bandari ya Malindi Unguja, wizara yangu kupitia Shirika la Bandari ililazimika kulivunja banda lililokuwa likitumiwa na Mkaguzi wa Magari yaani *Silver*, pamoja Shirika la Meli ili kupata eneo la wazi kwa ajili ya kuyawezesha magari yanayokuja bandarini kushusha na kupakia abiria kupitia gari mpya ya abiria, eneo hilo si kwa ajili ya kufanya maegesho ya magari.

(b) Kazi ya kuvunja banda hilo na kusawazisha eneo hilo imekamilika katika mwezi wa Septemba, 2009 pamoja na matayarisho mengine. Kazi ya uwekaji wa sakafu ya lami katika eneo hilo ilisita kutokana na matatizo kwa kipindi kirefu. Hata hivyo, kazi hiyo inatarajiwa kuanza hivi karibuni kwa vile tayari wizara yangu imeshanunua lami ambayo itafanya kazi hiyo na imeshafika nchini.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri anasema kazi ya kuvunja ilimalizika tokea mwezi Septemba na kwamba tatizo liliopo sasa hivi ni kuweka lami ambayo ilikuwa haipo. Mimi sidhani Mhe. Spika, kwamba lami hii ikipatikana itakwenda pale ikamwagwe tu, ni lazima kuna matengenezo ya awali yafanyike ambayo sasa hivi bado yanaonekana baada ya kuvunja hakuna lililofanyika. Je, Mhe. Naibu Waziri anaweza kutueleza ni kwa nini baada ya

uvunjaji ule hazikuendelea kazi nyengine za matayarisho ili itakapokuja lami basi imalizie kazi tu?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, ni kwamba kazi zote ambazo ni za awali za matayarisho kwa ajili ya uwekaji wa lami ziko tayari, labda pengine Mhe. Mjumbe hajatembelea hapo bandarini. Pengine suala ambalo analizungumza inawezekana ikawa, aidha hilo eneo tunalolizunguza hajalifahamu vizuri au la. Kwa sababu eneo ambalo tayari linatiwa lami ni kule ndani ambako tayari kuko vizuri. Inawezekana pengine Mhe. Mjumbe ni muda mrefu hajapita eneo hilo na kuona. Kwa wale ambao wamepita basi wataona kwamba kazi hiyo imefanywa na kinachosubiriwa ni kutia hiyo lami tu.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) ya swali hili.

Mhe. Spika, kwa kuwa gati imeanza kufanya kazi vizuri, ambapo meli za mizigo zikifika katika Bandari ya Zanzibar inateremshwa haraka haraka na kufanya kazi iwe nzuri. Lakini tatizo liliopo ni maegesho ya magari ya mizigo ambapo jambo hili bado halijapatiwa ufumbuzi.

(a) Je, Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, wameshaandaa mikakati yoyote mizuri ambapo kutakuwa na maegesho ya magari na mizigo ya kutosha katika upanuzi wa bandari utakaofanywa hapo baadae hadi kufikia Mpigaduri?

(b) Je, kuna mikakati yoyote ya maegesho ya magari pamoja na mizigo katika Bandari ya Mkoani kwa pande zake za mbavuni, ili kutoa nafasi kubwa ya maegesho ya magari pamoja na mizigo katika bandari hiyo ya Mkoani? Ahsante.

Mhe. Spika: Swali lilikuwa linajikita kwa Bandari ya Malindi. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Waziri jibu swali hilo linalohusu Bandari ya Malindi. Hilo swali jengine Mhe. Mjumbe atatafuta utaratibu wa kuuliza swali mama.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri katika swali la msingi.

Mhe. Spika, mpango wetu serikali sio kuipanua bandari mpaka Mpigaduri, isipokuwa ni kujenga bandari mpya ya Mpigaduri. Kwa hivyo, katika bandari mpya ya Mpigaduri kutakuwa na kila kitu ambacho kinahitajika katika bandari ya kisasa.

Tunatarajia kuwa na bandari ya kileo pengine kuliko bandari zote za Afrika ya Mashariki. Isipokuwa kule kwa sasa tutaendelea kutumia kwa kushusha wageni, wasafiri wa kawaida na mizigo ya kawaida ya ndani.

Katika hilo ambalo Mhe. Naibu Waziri amelizungumza, tukishatengeneza pale basi kutakuwa na maegesho kwa ajili ya taxi na gari za mizigo pale ndani. Lakini hizi gari za abiria watakuwa wanakwenda kushusha abiria wao na kuondoka, haturuhusu kufanya maegesho kule ndani.

Nam. 30

Kiwango cha Ubora wa Barabara Zetu

Mhe. Ali Denge Makame - Aliuliza:-

(a) Je, Mhe. Waziri, kwa nini barabara zetu huchukua muda mfupi kuharibika na kuwa na mashimo?

(b) Je, kiwango cha ujenzi wa barabara hizo ni duni?

(c) Kama hiyo ndio sababu Je, tuna tatizo la utaalamu au nyenzo zinazotumika, kama vile lami ni ya kiwango cha chini?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 30 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Muda wa matumizi ya barabara na uzima wake hutegemea na aina ya ujenzi wa barabara husika, pamoja na hali halisi ya udogo wa eneo husika.

Kwa mfano:

(i) Barabara ya kifusi iliyojengwa na kuwekwa miundombinu ya mitaro, makalvati na vyenginevyo hudumu baina ya miaka 3 hadi 5.

(ii) Barabara za kokoto kavu – tabaka moja, yaani "*single layer surface dressing*" hudumu baina ya miaka 5 hadi 7.

(iii) Barabara ya lami ya kupika "*Double layer*" hudumu baina ya miaka 7 hadi 12.

(iv) Barabara za lami ya kupika "*Asphalt Concrete*" hudumu baina ya miaka 10 hadi 20.

Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Kuharibika kwa barabara na kuwa na mashimo hakusababishwi na kuwa barabara hizo ni mbovu au tatizo la Mtaalamu au nyezo zilizotumika, bali ni kutokana na aina ya ujenzi uliofanywa kama nilivyokwishaeleza katika maelezo yangu hapo juu.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa tunao wataalamu wetu wa UUB wa ujenzi wa barabara.

(a) Je, hawa wanasoma nchi gani au chuo gani katika utengenezaji wa barabara hizi?

(b) Kwa kuwa wananchi huwa wanahitaji barabara iliyokuwa bora na nzima zaidi. Je, ataniambia ni lini au siku gani barabara iliyokuwa ikilalamikiwa sana ya Benjamini Mkapa ambayo *line* ya pili haijatengenezwa na wao wananchi wanataka barabara iliyokuwa madhubuti na fedha zinaambiwa zimeshafika na kwa muda mrefu. Je, wananchi hawa ni lini watatengenezewa barabara ile ili wajitayarishe kwa kuondoa matofali yao ya magari yao ya ng'ombe katika maeneo yale? Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwanza amesema kwamba wataalamu wetu wamekwenda nchi gani kusoma.

(a) Mhe. Spika, kama zilivyo wizara nyengine, wizara yetu ina mpango pia wa kuwasomesha wafanyakazi wake katika nchi mbali mbali duniani pale mahitaji yatakapopatikana.

(b) Kuhusu barabara ya Benjamini Mkapa. Mhe. Spika, kama unavyoelewa kwamba kazi zetu ni nyingi kwa hivyo, tunahitaji muda ili tujipange vizuri, barabara hiyo itajengwa na tunawaambia wananchi kwamba wasiwe na wasi wasi. Ni kweli kwamba pesa hizo tayari ziko Wizara ya Fedha kwa hivyo tunaweza kuijenga barabara hiyo wakati wowote.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru sana, namshukuru pia Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Napenda kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Spika, baada ya Mhe. Naibu Waziri kueleza viwango vya utaalamu vya utengenezaji wa barabara, mimi napenda kumuuliza kwamba barabara ya Chake Chake Mkoani iliyojengwa na PRISMO miaka michache iliyopita.

(a) Je, ile imekusudiwa iishi miaka mingapi na katika vile viwango vya kitaalamu alivyovitaja, barabara ile imo katika kiwango kipi?

(b) Je, imekusudiwa kupita magari ya tani ngapi?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchumizi: Mhe. Spika, barabara ya Mkoani- Mtuhaliwa. Kwa sababu barabara ya Mkoani - Chake Chake inasehemu mbili. Kuna barabara ya Mkoani - Mtuhaliwa na Mtuhaliwa - Chake Chake.

Mhe. Spika, kwa barabara ya Mkoani - Mtuhaliwa kiwango chake ni cha *Asphalt Concrete* ambacho ni kati ya miaka 10 na 20 uzima wake. Kwa upande wa barabara ya Mtuhaliwa - Chake Chake ile ni kama imefanywa *surface dressing*, kwa sababu haikuvunjwa yote, ilifanyiwa matengenezo baada ya fedha kubakia.

Hiyo ndio katika hicho kiwango alichosema Mhe. Naibu Waziri kati ya miaka 5 na 7.

Vile vile kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba tunaangalia sana na mazingira ya eneo na hali halisi ilivyo. Lakini barabara zote katika ujenzi wake, kwanza kuna kitanda cha barabara ambacho kinaitwa *road bad* kabla ujenzi wenyewe kuanza, baadae tunakuja *sub grad* kifusi, halafu tunakuja *sub base* pia ni aina ya kifusi chengine, halafu tunakwenda katika base yenyewe, tunatumia kifusi maalum pale kama *crusher* au chenginecho.

Tukimaliza hapo tunaweka *primer* ile lami nyepesi, hatimaye ndio tunaweka ile lami ngumu. Kwa barabara zote za Unguja lami yetu ni ya aina moja. Kuna lami inaitwa at 80 kwa 100 hiyo ama sisi wenyewe wazalendo au wafadhili tunatumia lami ya aina hiyo.

Sasa kwa miradi hii inayojengwa na kampuni kubwa ambapo hatujengi wenyewe mawasiliano. Tenda inafanywa anatafutwa mjenzi, lakini na msimamizi wa ujenzi pia tunakuwa sio sisi Wizara ya Mawasiliano, pia anatafutwa msimamizi. Kwa hivyo, viwango vya kimataifa vinafuatwa. Isipokuwa tatizo letu wakati mwengine ni ardhi.

Kwa mfano ardhi ya Mkoani ni tofauti pengine na ardhi ya Wete. Au ardhi ya Makunduchi ni rahisi kujenga barabara ikadumu muda mrefu kuliko ardhi ya maeneo mengine kutokana na ardhi ilivyo. Pia barabara hizi zote za Zanzibar zina viwango vyake vya kupitisha gari, pengine tani 10 mpaka 14, hatuzidi hapo katika mabarabara yetu ya Unguja na Pemba.

Mhe. Ahmed Nassor Mazrui: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi. Mhe. Spika, barabara ya Bububu imejengwa miaka 28 iliyopita takriban kama hivi. Hivi karibuni imeparwa na kuchimbwa mashimo makubwa makubwa, halafu ikawachwa, sasa hivi mvua zinanyesha inazidi kuathirika.

Mhe. Spika, kutokana na mafunzo niliyopata kutoka katika wizara yake, nilikwenda kozi mimi, tuliambiwa njia inayoparwa na kuchimbwa mashimo pale pale izibwe. Sasa kuna mpango gani wa kumaliza kazi ile kabla ya kuathirika njia ile, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba barabara ya kutoka Kinazini Bububu utakuta sehemu nyengine zimekatwa na nyengine zimeparwa ili kuondoa tabaka la juu.

Kwanza Mhe. Spika, lengo letu la mwanzo ilikuwa ile njia yote tuondowe tabaka la juu na tutie *overlay*, lakini baadae baada ya mazungumzo na Serikali ya Japan na kuonesha nia ya kuja kuitengeneza tena njia ile tukaona tutakuwa tunatumia vibaya rasilimali za nchi.

Kwa hivyo tukaamua tuondowe lile tabaka la juu katika sehemu mbaya zaidi na tukate zile sehemu ambazo zina mashimo ambayo tunaweza tukatia viraka na kuendelea, ili Serikali ya Japan, maana yake mazungumzo yako katika hatua kubwa ya kuleta wataalamu wao, watakapokuja wasije wakaahirisha.

Lengo letu tunazungumza mpaka Bububu, lakini lengo letu la kuzungumza nao ili twende mpaka Kinazini ya Mkwajuni ili kuitengeneza barabara hii katika kiwango kipya.

Mhe. Spika, kuhusu kwamba tumeikata ile barabara na tumeiwacha. Mhe. Spika, nataka niwahakikishie kwamba tuliona kwamba kukata tukaanza kuweka viraka pale kidogo kidogo, tunaweza tukaleta usumbufu, lakini ni bora usumbufu wa siku tatu kwanza tuiondowe ile, halafu baadae ndio kazi ianze.

Tulitarajia kufanya kazi hii ya kuweka lami wiki iliyopita siku ya Alhamis, lakini bahati mbaya ile mvua ilituathiri katika *material* yetu yaliroa na yakiroa yale kama hayajakauka basi huwezi kuweka barabarani. Mwenyezi Mungu akipenda nafikiri wiki hii kama jua litatoka basi tunatarajia kuweka lami kwenye barabara hiyo ya Bububu na pia barabara ya Mwembemakumbi Chumbuni.

Nam. 13

Malipo ya Wafanyakazi Kupitia Benki

Mhe. Haji Mkema Haji – Aliuliza:-

Katika mikakati ya kudhibiti wizi wa mishahara na malipo ya mishahara hewa Serikali imeanzisha utaratibu wa kuwalipa wafanyakazi wake kwa njia ya Benki. Utekelezaji wa utaratibu huo umeanza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

(a) Je, Mhe. Waziri, taasisi nyingine zitaanza lini kutekeleza utaratibu huo?

(b) Kisiwani Pemba Benki zote ziko katika mji wa Chake-Chake huoni kuwa utekelezaji wa mpango huo utaleta usumbufu kwa wafanyakazi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba?

(c) Kama kuweka matawi ya benki kila mahala ni gharama, kwa nini utaratibu wa kuweka mawakala wa benki katika maeneo mbali mbali usitumike kama zinavyoweka mawakala Kampuni za Bima?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nam.13 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba utaratibu wa kulipa wafanyakazi mishahara yao kupitia benki umeanza, mbali na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, lakini pia Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ nayo imeanza pamoja na taasisi nyengine za serikali.

Mhe. Spika, serikali itaendelea kuhakikisha kwamba utaratibu huu unasimamiwa vizuri na unaelelezwa katika wizara zetu zote za serikali na taasisi zake na kuhakikisha kwamba zinatumia utaratibu huu, kwa kiasi kikubwa ni imani yetu kwamba wakitumia utaratibu huu basi utapunguza wimbi la wizi wa fedha za mishahara ya wafanyakazi zinazohifadhiwa katika Taasisi za Serikali.

(b) Mhe. Spika, lengo la utaratibu huu ni kuleta ufanisi katika masuala ya usimamizi na udhibiti wa fedha za Umma, iwapo kutatokea usumbufu wowote sio lengo lililokusudiwa. Vile vile tukizingatia ukuaji wa uchumi na shughuli za kimaisha zinazoendelea kutanuka Kisiwani Pemba, ni dhahiri kwamba Benki nazo zitafikiria kufungua matawi katika maeneo ambayo shughuli zake kiuchumi zinakuwa, hivyo haitokuwa usumbufu kwa siku za usoni.

Mhe. Spika, naomba tusaidiane Waheshimiwa Wawakilishi na waheshimiwa wengine kuwaelimisha wananchi wetu, umuhimu wa kuweka pesa zao benki ili benki zitakapofungua hayo matawi basi wateja wajitokeze wengi kuwekeza katika matawi hayo tofauti na huko nyuma ambapo ilibidi baadhi ya matawi yafunwe, kwa sababu ilikuwa hakuna wateja wa kuweka pesa zao.

(c) Mhe. Spika, suala la kufungua matawi ya benki kila mahala linahitaji kufanyiwa kazi zaidi, ikiwa ni pamoja na utafiti. Kama nilivyokwishasema kwamba shughuli za kiuchumi Kisiwani Pemba zinaendelea kukua, basi na benki nazo zinaweza kufanya utafiti wenyewe na kuona uwezekano wa kufungua matawi kwa ajili ya kutoa huduma hizo na kuwarahisishia kwa kuwaondoshea usumbufu, si wafanyakazi tu bali hata wafanyabiashara na wakulima kwa ujumla, ahsante.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, napenda kumpongeza Mhe. Waziri kutokana na majibu yake. Nina swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, utaratibu au mradi mzima wa malipo kwa njia ya benki ni moja katika kupunguza wizi. Bahati nzuri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeshaanza. Lakini Mhe. Spika, bado hivi karibuni tulisikia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kumevunjwa na fedha zimeibiwa.

(a) Je, fedha hizi zilizoibiwa zilikuwa ni za mishahara au ni za aina gani kama anavyojua yeye Mhe. Waziri?

(b) Mhe. Spika, katika utaratibu huu wa kuwaondolea usumbufu wananchi, waziri amezungumza kuwa basi atatoa wito kwa vyombo hivi. Je, ni hatua gani ambayo imechukuliwa Mhe. Waziri za mawasiliano na taasisi hizi ili kuhakikisha wanaharakisha jambo hili la kutoa huduma hizo katika vijiji ambavyo havina benki?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba hivi karibuni kulitokea wizi pale Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuvunjwa. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali yupo, naamini kuwa yeye atakuwa katika hali nzuri zaidi, baada ya mimi pengine kumaliza jibu hili ili kuelezea hasa kilichotokea pale. Mimi sijaipata ripoti kamili. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako namuomba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali anisaidie.

Lakini kwa upande wa pili, kwa kweli serikali inajiandaa vyema tu kwa taratibu kamili, mbali ya kuwaelimisha, lakini utaratibu mzima wa kuhakikisha kwamba wizara zote za serikali basi wafanyakazi wake watafungua akaunti zao kwenye mabenki halafu mishahara ipelekwe benki moja kwa moja. Kwa hivyo, huo utaratibu serikali kuu yenyewe inaandaa utaratibu.

Kwa hivyo, wacha tumalize huu utaratibu, kwa sababu tusifanye mambo nusu nusu ikawa utaratibu haujakamilika mishahara inatoka halafu ikawa vurugu vurugu tu. Kwa hivyo, nahisi mheshimiwa tutampa ripoti kadiri tunavyoendelea au utajulishwa na Baraza lako tukufu kadiri hali ya matayarisho, lakini tutahakikisha kwamba hilo zoezi linakamilika mapema inavyoyumkinika, ahsante.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa benki zote katika kisiwa cha Pemba zipo katika mji wa Chake-Chake na kwa kuwa Mkoani Pemba hakuna benki hata moja ya kuwahudumia wananchi na kwa kuwa wananchi wa Mkoani Pemba hufuata huduma zao katika mji wa Chake-Chake.

Je, Mhe. Waziri huoni kuna umuhimu wa kuweka mawakala au benki moja Mtambile Pemba ambapo ni katikati ya sehemu zote za Mkoani Pemba, ili kuwapunguzia wananchi usumbufu wa kufuata huduma zao masafa makubwa. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba benki nyingi Pemba ziko Chake-Chake zaidi kwa sababu ya mvuto wa kibiashara. Lakini tukija kwa upande wa huduma, ni kweli inabidi lazima huduma ziende kote, Chake-Chake, Mkoani, Gando na kote.

Mhe. Spika, benki yetu ya PBZ tayari ina mipango, nafikiri tumeshawahi kuzungumza suala hili, ina mipango ya kufungua ile *mobile services* na mkoani watafika. Pia tulisema hata wataweka mpaka ile ATM, ili mtu mwenyewe aende akatowe pesa. Kwa hivyo, mipango hiyo tunayo, lakini nasema kidogo

inabidi tuhakikishe, kwa sababu tuliwahi ku-*introduce* zamani hizo ATM pake Chake Chake zikafeli, unajua utaalamu kidogo nao una mambo. Kwa hivyo, hatutaki Mhe. Mwanajuma tuweke ATM kule halafu anakwenda kutoa pesa hazipati. Kwa hivyo, tunakamilisha hiyo mipango upesi upesi ili tuone kwamba hilo jambo linafanikiwa. Ahsante.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi alipokuwa akijibu, alikuwa na uhakika anatujibu Baraza hili kwa uhakika. Bahati nzuri swali lake amelijibu nusu, lakini pia alione aridhike mwenziwe Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali amsaidie ili hilo swali likamilike jibu lake na Baraza hili lipate faida. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naona hukumpa nafasi Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ili kuongezea jawabu ya lile swali ambalo nimeliuliza kuhusu wizi wa fedha za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika: nilifikiri angesimama ningejua kajitayarisha kwa hilo, sikumuona kasimama ndio nikaendelea. Kwa hivyo, nafikiri tutatafuta utaratibu ambapo anaweza akatoa maelezo baadae. Muda wetu unakaribia kwisha. Suala linalofuata, Mhe. Abass Juma Muhunzi.

Nam. 14

Mpango wa Benki Kuu wa Ujenzi wa Nyumba Nafuu

Mhe. Abass Juma Muhunzi – Aliuliza:-

Hivi karibuni Benki Kuu ya Tanzania (*Bank of Tanzania – BOT*) imetangaza kutekeleza mpango wa ujenzi wa nyumba nafuu za makaazi kwa wananchi.

(a) Kwa kuwa Benki Kuu ni Taasisi muhimu ya Muungano ambapo Zanzibar kama nchi ni ubia, Je, nchi hii ya Zanzibar imepangiwa kujengwa nyumba ngapi katika mpango huo?

(b) Je, katika hiyo kasma ya Zanzibar ya mradi wa nyumba hizo, Serikali imeshatenga maeneo ya ujenzi wa nyumba hizo. Maeneo hayo ni yepi?

(c) Kwa misingi ya kuwa Zanzibar ni wabia kama nchi, na kwa kuwa Baraza la Wawakilishi ndilo linalosimamia mipango na miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar,

Je, Mhe. Waziri unaweza kulieleza Baraza hili Mradi huu wa BOT utatekelezwa kwa muda gani na utagharimu kiasi gani cha fedha?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Benki Kuu chini ya Programu ya Mageuzi ya Kifedha ya Karne ya Pili yaani *Second Generation Financial Sector Reform* imeweka kwenye mtandao wake taarifa inayohusiana na mradi wa kuendeleza soko la mikopo ya kujengea nyumba yaani *Housing Finance Project* ambao unategemewa kuanzishwa hivi karibuni. Taarifa hizi ni moja ya hatua muhimu ya kupata mkopo ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari ipo kwenye majadiliano na Benki ya Dunia kupata mkopo huo.

Mhe. Spika, mkopo huu utakuwa na thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 40, ambapo sehemu kubwa itatumika kuanzisha chombo kitakachotoa mikopo kwa Taasisi za fedha ili ziweze kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Benki Kuu itaunda chombo kitakacho kopeshwa kiasi cha Dola za Kimarekani Milioni 30 ikiwa ni kianzio cha kukiwezesha kutoa mikopo kwa Taasisi za fedha zitakazokuwa zinatoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizi.

Sehemu ya pili ni kwa ajili ya kuendeleza utoaji wa mikopo midogo midogo ya kujengea nyumba. Madhumuni yake ni kuendeleza upatikanaji wa mikopo nafuu ya kujengea nyumba hasa kwa watu wenye kipato cha chini katika utaratibu huo huo.

Mhe. Spika, sehemu ya tatu itakuwa ni kusaidia upatikanaji wa nyumba za kununua. Sehemu hii ya mradi itasaidia uendelezaji wa makaazi binafsi na Mashirika ya Nyumba nchini kutengewa kiasi fulani cha mkopo huu, ambacho kitasaidia kutoa elimu kwa waendelezaji makaazi pamoja na kufanya utafiti wa ujenzi wa nyumba nafuu kwa kutumia vifaa vya bei nafuu.

Mhe. Spika, baada ya maeleo hayo mafupi, sasa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo:-

(a) Kutokana na maelezo niliyoyataja hapo juu ni dhahiri kwamba Benki Kuu haina mpango wa moja kwa moja kutekeleza ujenzi wa Nyumba za Bei Nafuu kwa Zanzibar au Tanzania Bara. Isipokuwa Benki Kuu chini ya *Program* ya Mageuzi ya Fedha itatumia mkopo wa Benki ya Dunia katika kuipatia taasisi maalum itakayoundwa, ili hatimaye taasisi hiyo itazipatia benki za ndani mikopo ambayo itakopeshwa na makampuni yatakayokuwa tayari kujenga nyumba za bei nafuu na juu.

(b) kutokana na utaratibu huu ambapo serikali haihusiki moja kwa moja katika ujenzi wa nyumba hizi serikali haijatenga maeneo yoyote, kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizi kwa sababu nilizozieleza hapo awali.

(c) Mradi wa kuendeleza Soko la Mikopo ya Ujenzi wa Nyumba ni wa muda wa miaka mitano. Kwa hivyo, mkopo unaotafutwa kutoka Benki ya Dunia ni wa Masharti Nafuu wa thamani ya Dola za Kimarekani milioni 40 na utalipwa kwa muda wa miaka 30. Hii ni baada ya miaka 10 ya kipindi cha mpito kabla ya urejeshwaji mkopo. Taasisi zitakazoanzishwa au kuhusika chini ya mradi huu zitakuwa endelevu.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kura ya Maoni na Mambo Mengine Yanayohusina na Hayo

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili ya kuwasilisha Mswada huu wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kura ya Maoni na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nataka nimshukuru sana Mhe. Mwenyekiti ya Katiba na Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi Mhe. Haji Omar Kheir, Makamo Mwenyekiti Mhe. Haji Mkema Haji pamoja na wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kwa kuupitia mswada huu na kufanya marekebisho kwa yale ambayo wameona yanafaa.

Vile vile nashukuru sana kwamba tumepata mashirikiano makubwa na kamati hii. Pia nichukue fursa hii kuishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuwaalika wadau mbali mbali kabla mswada huu kufanyiwa marekebisho, ili na wao kuweza kutoa mchango wao wa mawazo pamoja na kuwashauri Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa lengo la faida na maana juu ya sheria hii ambayo tunaianzisha kwa wananchi wetu wa Zanzibar.

Pamoja na kwamba Waheshimiwa Wajumbe wamepata nafasi kupeleka mswada huu kwenye majimbo yao na kuweza kupata maoni kutoka kwa wananchi wao. Kwa hiivyo, naamini Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watataweza kutoa michango yao hapa, kwa ajili ya kuifanya iwe bora zaidi sheria hii, ili iweze kuwa na maslahi kwa taifa letu.

Mhe. Spika, baada ya hayo sasa niende moja kwa moja kwenye uwasilishaji wa mswada huu. Kwa kweli kama nilivyoeleza mwanzo kwamba mswada huu ni maalum wa kuanzisha Kura ya Maoni.

Madhumuni ya mswada huu ni kutunga Sheria ya Kura ya Maoni. Vile vile mswada ni matokeo ya Azimio la Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliotoa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi kilichopita cha mwezi Januari mwaka 2010. Katika kikao hicho Baraza la Wawakilishi lilipitisha azimio lililoelekeza pamoja na mambo mengine kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010.

Aidha katika kulifanyiakazi azimio hilo, serikali imeamua kuandaa mswada wa sheria utakaoelekeza utaratibu mzima wa kufanyika Kura ya Maoni pale tu itakapotokea haja ya kufanya hivyo.

Mhe. Spika, mswada huu umegawika katika maeneo manne makuu kama hivi ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza imeanza na utangulizi ambapo jina, sheria, tarehe ya kuanza kutumika pamoja na tafsiri ya maneno kama yalivyotumika kwenye sheria imeelekezwa.

Sehemu ya Pili inahusu Masharti ya Kura ya Maoni, katika sehemu hii imeelekezwa amri ya Rais kuitisha Kura ya Maoni. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kuwa ndio dhamana wa kuendesha Kura ya Maoni na uteuzi wa maafisa wa kusimamia Kura ya Maoni. Vile vile vituo vya kura ya maoni, karatasi za kura, haki ya kushiriki katika kura ya maoni pamoja na utaratibu wa kupiga kura ya maoni.

Mhe. Spika, sehemu ya tatu inahusu matokeo ya Kura ya Maoni. Katika sehemu hii imeelekeza matokeo ya kura ya maoni kufuatwa na serikali na utaratibu wa kuhoji matokeo ya kura ya maoni.

Sehemu ya nne inahusu masharti ya jumla, ambapo imeelezwa mtu anayepiga kura hatatakiwa kueleza jinsi alivyopiga kura, kukataza kufanya uchochozi, fujo na vurugu wakati wa kura ya maoni. Vile vile gharama za kura ya maoni imeelekeza kijumla kwa tume na maafisa wa kura ya maoni kutumika kwa Sheria ya Uchaguzi pale ambapo itakapoona inafaa. Pia imeeleza makosa pamoja na adhabu.

Mhe. Spika, mswada huu kama nilivyoeleza kwamba umetokana na hoja ambayo iliyopitishwa katika kikao kilichopita. Pamoja na hayo, serikali kwa kuona umuhimu wa suala hili, basi tumeamua kuleta Mswada huu wa Sheria ya

Kura ya Maoni, ambayo sio tu itatumika kwa suala la kura ya maoni hili ambalo limeelezwa katika suala la mfumo wa maamuzi ya wananchi, aidha waamue tuendelee na serikali kama ulivyo mfumo wa hivi sasa au twende katika mfumo wa Serikali Shirikishi. Lakini sheria hii tunaianza na itakuwa sheria ya kudumu kwa yale mambo mengine yote ambayo yatahitaji kupata ridhaa ya moja kwa moja ya wananchi bila ya kupitia kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, basi sheria hii itaweza kutumika kama itakavyokuwa *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waache jazba, kwa sababu hapa hatufanyi maamuzi. Isipokuwa hapa tumekuja kuanzisha sheria ya Kura ya Maoni na wananchi wenyewe ndio watakaokuwa na maamuzi, tena maamuzi yenyewe sio kwa suala hili ambalo lipo mbele yetu, lakini kwa jambo lolote litakalokuwa na maslahi ya Zanzibar, basi wananchi watakuwa na haki ya kupiga Kura ya Maoni *(Makofi)*.

Suala la Kura ya Maoni aidha litakuja kwa Azimio la Baraza la Wawakilishi au mwenyewe Mhe. Rais atakapoona ipo haja ya kuitisha kura ya maoni kwa jambo lolote lile *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nadhani kwa maelezo hayo niliyoyatoa naamini Waheshimiwa Wajumbe watakuwa watulivu na watazungumzia hoja kwa ajili ya kuufanya uwe bora zaidi mswada huu, ili baadaye tuweze kuufanyiakazi.

Baada ya hayo machache nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunistahamilia. Lakini kama nilivyosema mwanzo kwamba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na Mhe. Waziri Kiongozi kwa kuweza kuniongoza na namna ya kuweza kusimamia sheria hii. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja *(Makofi)*.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii muhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana tena katika ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi, ili kuendelea kutekeleza sehemu ya majukumu yetu ya kitaifa, kwa lengo la kuwaletea mustakbali mzuri wa wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

Sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema hii aliyotujaalia katika shughuli yetu hii muhimu ya kuupitia Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kufanyika Kura ya Maoni na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo, hatimaye Waheshimiwa Wajumbe kuweza kuupitisha mswada huu.

Mhe. Spika, pili napenda kuendeleza shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi, kwa kuniruhusu nitowe mchango kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tumbatu.

Mhe. Spika, napenda pia, kuipongeza Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa uamuzi wao wa busara wa kuwaalika wadau kutoka taasisi mbali mbali kuja kuujadili mswada huu na kutoa maoni yao kwa kamati, kama ambavyo imeelezwa katika kanuni ya 106(9) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2009. Sambamba na kuzidi kutekeleza utawala bora na wa kidemokrasia.

Aidha, naomba nichukuwe nafasi hii niwapongeze na kuwashukuru wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao mbele ya Kamati yetu. Naomba niwatambue kwa kuzitaja Taasisi zilizoshiriki kama ifuatavyo;-

- Vyama vya Siasa visivyo na Uwakilishi kwenye Baraza la Wawakilishi – Zanzibar.
- Jumuiya Zisizo za Serikali (kwa kupitia *ANGOZA*)
- Jumuiya ya Wanasheria wa Zanzibar (*Zanzibar Law Society*)
- Madhehebu ya Dini ya Kikiristo na Kiislamu na
- Wataalamu na wasomi kutoka Vyuo Vikuu vya Zanzibar *(Makofi)*.

Mhe. Spika, napenda kutamka wazi kuwa wadau hawa walitoa maoni mazuri na madhubuti kwa lengo la kuuimarisha mswada wetu huo.

Wakati wa kuupitia na kuuchambua mswada huu uliopo mbele yetu katika kamati, kamati yetu ilipata ushirikiano wa kutosha kukamilisha majukumu yake kutoka kwa watendaji wote wa wizara hii pamoja na Mhe. Waziri wa Wizara ya Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi. Hivyo, kamati yetu inawashukuru wote hao kwa pamoja kwa mashirikiano mazuri waliyotupa kwa muda wote *(Makofi)*.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ina Wajumbe 10, ambao walihusika kikamilifu katika kuupitia mswada huu muhimu kwa maslahi ya nchi yetu na taifa kwa ujumla. Wajumbe wenyewe ni:-

1. Mhe. Haji Omar Kheri	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Haji Mkema Haji	-	M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Zahra Ali Hamad	-	Mjumbe
4. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Mjumbe
5. Mhe. Abdalla Juma Abdalla	-	Mjumbe
6. Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin	-	Mjumbe
7. Mhe. Fatma Abdalla Tamim	-	Mjumbe
8. Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe

9. Mhe. Najma Khalfan Juma	-	Mjumbe
10. Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	-	Mjumbe
11. Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
12. Ndg. Abdalla Ali Shauri	-	Katibu

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kufanyika Kwa Kura ya Maoni na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo, umekuja kufuatia Azimio la Baraza la Wawakilishi walilolitoa katika Mkutano wa 18 wa Baraza la Wawakilishi mwezi Januari mwaka 2010. Katika Mkutano huo Baraza la Wakilishi lilipitisha Azimio lililoeleza pamoja na mambo mengine kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa 2010 kufuatia Azimio hilo.

Serikali imeamua kuandaa Mswada wa Sheria utakaoeleza utaratibu mzima wa kufanyika kwa kura ya maoni pale tu itakapotokea haja ya kufanya hivyo.

Mhe. Spika, napenda kuchukuwa nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, kwa uamuzi wao wa pamoja bila ya kujali tofauti zao za kisiasa, kwa kuipitisha Azimio la Baraza la Wawakilishi kuhusiana na kuanzishwa kwa Serikali ya Umoja wa Kimataifa, ambapo suala hilo liliamuliwa kupelekwa kwa wananchi kupitia kura ya maoni, ili na wao watoe baraka zao *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nathubutu kusema kuwa kitendo hicho kimedhihirishia wazi dunia, kuwa Zanzibar ni miongoni mwa nchi inayoongozwa kwa kufuatwa misingi ya demokrasia na utawala bora. Kufuatia uamuzi huo ndio maana leo hii tunaujadili mswada huu na hatimaye kuwa sheria kamili iwapo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wataujadili na kuupitisha Mswada husika. Sanjari na kupata kibali cha Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa Kifungu cha 78(3) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Mhe. Spika, kamati yetu imeupitia mswada huu kwa kina kifungu kwa kifungu, sambamba na kuyafikiria maoni yaliyotolewa na wadau na kuweza kupendekeza marekebisho mbali mbali kwa lengo la kuuimarisha zaidi. Marekebisho haya yamejikita katika sehemu tofauti za mswada huu.

Kamati imependekeza katika kifungu cha 2 aya ya pili kutoka chini tafsiri ya neno "Kura ya Maoni" lirekebishwe na badala yake lisomeka kama ifuatavyo;-

"Maana yake ni utaratibu wa kupeleka suala au hoja kwa wapiga kura ili watoe uamuzi". Hii ni kutokana na kuwa tafsiri ya awali ilijikita katika mtazamo wa kisiasa pekee, wakati kura ya maoni inaweza kutokea hata kwa jambo ambalo sio la kisiasa.

Mhe. Spika, baadhi ya marekebisho tuliyapendekeza yalitokana na makosa ya kiuchapaji. Baadhi ya maneno hayo ni katika kijifungu cha 3(1), mstari wa pili kutoka juu neno la sita “kuopatikana”. Kamati imependekeza lisomeke “kutopatikana”. Katika kijifungu cha 4(1)(b) mstari wa kwanza kutoka juu neno la tatu “kusimami” Kamati imependekeza lisomeke “Kusimamia”.

Katika kifungu cha 12 kamati imependekeza kiongezwe kijifungu cha 12(4). Aidha hrufi za vijifungu vya kijifungu cha 12(3) yaani (a),(b),(c), na (d). vitafuata chini ya kijifungu hichi cha 12(4). Mhe. Spika, marekebisho mengine ni kama yanavyoonekana kwenye waraka wetu wa marekebisho.

Mhe. Spika, ili kuweka mpangilio wa sarufi vizuri kamati yetu pia, ilipendekeza kuongezwa na kufutwa baadhi ya maneno. Katika kijifungu cha 3(1) mstari wa kwanza kutoka chini maneno “dhidi ya” yaliyopo baina ya neno “kura” na “suala” yamefutwa na badala yake limependekezwa lisomeke neno “kuhusu”.

Aidha, katika kijifungu cha 3(2) mstari wa kwanza kutoka juu maneno “ya kura” yaliyopo baina ya neno “Amri” na “ya”, Kamati imependekeza maneno haya yafutwe. Pia, katika kijifungu cha 5(3) mstari wa pili kutoka juu, Kamati imependekeza liongezwe neno “na” baina ya neno “itakavyoelekezwa” na “Tume”. Halkadhalika, katika kijifungu cha 5(5) mstari wa pili kutoka juu neno “hii” liliopo baina ya neno “hiki” na “kuwa” limefutwa.

Mhe. Spika, kwa kuwa marekebisho kama haya ni mengi na sitoweza kuyataja yote ili kuulinda muda wako. Hivyo, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa marekebisho mengine yanapatikana kwenye waraka wetu wa mapendekezo ya marekebisho juu ya mswada huu.

Mhe. Spika, kijifungu cha 3(4) kamati yetu imependekeza kisomeke “Bila ya kuathiri masharti ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki, kura ya maoni inaweza kufanyika siku yoyote kama itakavyoelekezwa katika amri ya Rais”. Hii ni kutokana na kuwa ni vyema Mhe. Rais akapewa kupanga ni siku gani itakuwa muafaka kutekelezwa hili, kuliko kutamka moja kwa moja kuwa kura ya maoni itafanyika sambamba na Uchaguzi Mkuu.

Kamati inaishauri Serikali kufanya kura ya maoni siku tofauti na Uchaguzi Mkuu kwani kama tujuavyo kuwa siku ya uchaguzi wananchi huwa na hofu ya zoezi hili. Lakini pia, itakuwa tunawaongezea mzigo kwani huwachagua Wagombea watano kwa wakati mmoja *(Makofi)*.

Mhe. Spika, katika kijifungu cha 9(2) mstari wa kwanza kutoka chini maneno “zilizokubali au zilizokataa” yamependekezwa yasomeke “za ndiyo, hapana na zilizoharibika”. Hii ni kutokana na kuwa kwenye zoezi la kupiga kura mara nyingi matokeo ya kura huwa katika hali zote tatu na sio kujitokeza kura “zilizokubalia au kukataliwa” pekee.

Aidha, kijifungu cha 9(4)(b) kimependekezwa kisomeke;- “idadi ya kura za ndio, hapana na zilizoharibika kuhusiana na suala au hoja iliyotakiwa kuamuliwa katika kura ya maoni”. Kamati imependekeza hivyo kutokana na maelezo niliyoyatoa hapo kabla.

Mhe. Spika, katika kijfungu cha 10(1) kamati imependekeza kisomeke kama ifuatavyo;- “Mwenyekiti wa Tume atatangaza matokeo ya kura ya maoni ndani ya masaa 48 baada ya kufungwa kwa upigaji kura na matokeo hayo yatajulikana kama ni matokeo rasmi yaliyotangazwa, hayatoruhusiwa kutiliwa shaka kwa namna yoyote isipokuwa kwa kupeleka hati ya kuhoji matokeo ya kura ya maoni Mahkama Kuu”. Kamati ilipendekeza hili baada ya kubaini kuwa nakala ya tafsiri ya Kiingereza umeandikwa hivyo, sambamba na kuweka mpangilio wa sarufi vizuri.

Kutokana na kadhia hii, kamati yetu inazidi kusisitiza kuwa kupatikana kwa nakala ya Mswada wa Kiingereza wakati kamati zinapitia mswada ni muhimu, kutokana na kuwa mara nyingi Mswada wa Kiswahili huwa na mapungufu, ingawa kifungu cha 87 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinautambua zaidi Mswada wa Kiswahili kuliko wa Kiingereza. Hii ni kutokana na kuwa kifungu hicho kimeelekeza kuwa Mswada wa Kiingereza utaandikwa ukihitajika.

Mhe. Spika, tatizo kama hili limejitokeza pia, kwenye kifungu cha 12 ukurasa wa 5 wa Mswada husika, ambapo kwenye Mswada wa Kiswahili maneno “Baada ya kuchunguza, Mahakama Kuu inaweza ama:-” yamekosekana wakati ule wa Kiingereza maneno hayo yanapatikana.

Katika kijifungu cha 11(2) mstari wa kwanza kutoka juu kamati imependekeza maneno “zilizokubali na zilizokataa” yasomeke “za ndiyo na hapana”, ili kijifungu hichi kilingane na vijifungu vya 3(3)(a) na 7(2) vya mswada huu.

Mhe. Spika, katika kijifungu cha 12(1)(b) mstari wa kwanza neno “Tano” limependekezwa lisomeke “Tatu”. Kamati imependekeza hili kutokana na kuwa kiwango kilichotajwa ni kikubwa kwa mwananchi wa kawaida kuweza kugharamia.

Mhe. Spika, tuliona idadi ya dhamana ya kuweka kwenye Mahakama wakati mwananchi anataka kuhoji swali hili ni kikubwa mno. Kwa hivyo, tumeweka shilingi milioni 3 bada ya milioni 5.

Kijifungu cha 17(1) kamati imependekeza kisomeke kama ifuatavyo:-

“Bila kuathiri masharti ya Sheria hii, Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya 1984 pamoja na Kanunu zake itatumika kwa kiwango kile ambacho matakwa ya sheria hii yataruhusu pamoja na marekebisho yatakayohitajika”.

Aidha, kijifungu cha 17(2) Kamati imependekeza kisomeke:-

“Tume ya Uchaguzi inaweza, kwa kutoa tangazo katika Gazeti la Serikali, kutumia sehemu yoyote ya Sheria ya Uchaguzi au Kanuni zake, kwa ajili ya shughuli za kura ya maoni kwa kadri ya vile ambavyo Tume itaona inafaa kwa ajili hio”. Hii ni kutokana na utata uliokuwepo kwenye vijifungu hivi kuhusu utumikaji wa Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya 1984.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 18 mstari wa kwanza kutoka juu kamati imependekeza yaongezwe maneno yafuatayo “ambapo hakuna adhabu maalum iliyowekwa” baina ya maneno “hii” na “na”, ili kuepusha mgongano wa vifungu ndani ya mswada huu wa sheria.

Mhe. Spika, kamati pia, imependekeza kufutwa kwa kijifungu cha 19(2)(c) hii ni kutokana na kuwa kijifungu hicho tayari kimekwisha fafanuliwa kwenye Sheria ya Uchaguzi. Hivyo, vijifungu vyote vinavyofuata vitaathirika kutokana na mabadilko hayo.

Vile vile, kamati imependekeza marekebisho yafuatayo kwenye Jadweli. liongezwe neno “ya” baina ya neno “Tume” na “Zanzibar”. Aidha neno “aliopewa” liliopo baina ya neno “uwezo” na “chini” lisomeke “niliopewa”. Pia, neno “Mhe.” limefutwa na badala yake lisomeke neno “Mimi”. Vile vile , neno “anakuagiza” lisomeke “ninakuagiza”.

Hii ni pale pahala Rais anamuagiza Mwenyekiti wa Tume, kwenye Rais lilikuwa limewekwa neno Mheshimiwa, sawa lazima liwe hivyo. Lakini lazima liseme kwamba mimi Rais ninakuagiza Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi kuitisha Kura ya Maoni (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, ni mfano wa Rais atakavyotoa hiyo amri. Naona mnampigia makofi kama vile yeye ndio Rais *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kwa kuhitimisha, haya ndio maelezo ya uchambuzi wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa muhtasari. Kama yapo maeneo mengine ambayo kwa bahati mbaya sikuweza kuyagusia, natumai Waheshimwa Wajumbe wengine wa Kamati hii watayazungumzia pindi watakapopata fursa ya kuchangia katika mswada huu.

Mhe. Spika, baada ya mchango wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala sasa naomba nitoe mchango wangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tumbatu.

Mhe. Spika, wananchi wa Jimbo la Tumbatu wanayo haki ya kuunga mkono sheria hii ya kuanzisha utaratibu wa kura ya maoni yenye lengo la kuwapa nafasi wananchi kutumia utaratibu wa kilimwengu kwa kutumia demokrasia yao ya kuchagua mfumo na muundo wa serikali yao baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010.

Mhe. Spika, mimi ni kiongozi mwakilishi ninayewakilishi wananchi wa Jimbo la Tumbatu. Nipo hapa kwa kipindi cha tatu sasa ni miaka 15. Nimekuwa nikishuhudia mizozo na mifarakano isiyo na msingi, ndugu wenyewe kwa wenyewe tumekuwa tukihasimiana, tumekuwa hatuzikani, hatuendeani kwenye shughuli mbali mbali za kijamii.

Mhe. Spika, kuna mithali ya Kiswahili inayosema “Kila lenye mwanzo lina mwisho”. Mwanzo wa mifarakano ya watu wa Tumbatu ni uchaguzi wa 1995, inshaallah kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu mwisho wa mifarakano ya kisiasa kwa Watumbatu ni mwaka 2009 na mwaka huu wa 2010 iwe ni mwisho isiendelee tena.

Mhe. Spika, mimi Haji Omar Kheir ninayewakilishi Watumbatu nimeshachoka na mifarakano na kama mimi nimeshachoka na mifarakano hii, ni imani yangu na wananchi walionichagua wameshachoka na uhasama na mifarakano ya kisiasa.

Mhe. Spika, katika hili ninayo haki na wajibu nikiwa kama kiongozi wa kujali maslahi ya watu na sio ya maslahi yangu binafsi. Kwa msingi huu, kupitia Baraza hili naahidi kushirikiana na wananchi walionichagua kurejesha mila na desturi za Watumbatu na umoja na mshikamano na upendo wa wananchi wa Tumbatu kama sera na ilani ya CCM ya mwaka 2005-2010 inavyoeleza kwenye ukurasa wa 124 kifungu cha 101.

Mhe. Spika, hapa naomba kunukuu

Kifungu cha 101 “Sera ya kuwaunganisha na kuwashirikisha wananchi wa Zanzibar katika harakati za ujenzi wa taifa lao kwa amani na utulivu zilipewa umuhimu mkubwa katika kipindi kilichopita, kufikiwa kwa muafaka wa kisiasa tarehe 10 Oktoba, 2001 kati ya CCM na CUF ni uthibitisho tosha wa usahihi wa Sera za CCM ili kuimarisha mafanikio hayo ya kujivunia CCM katika kipindi hiki itatekeleza yafuatayo:-

- Kuendeleza matunda ya muafaka kwa faida na maslahi ya Wazanzibari wote.
- Kuendelea kupiga vita kwa nguvu zote ubaguzi wa dini, kabila, jinsia, akili au mtu katika utoaji wa huduma na fursa mbali mbali za kiuchumi na kijamii.
- Kuendeleza umoja, mashirikiano, amani, utulivu miongoni mwa wananchi wote na kuimarisha jumuiya mbali mbali za maendeleo za kiuchumi na kijamii”.

Mhe. Spika, kwa sababu siendi kinyume na sera na ilani ya chama changu cha CCM nitatumia uwezo wangu wote alionijalia Mwenyezi Mungu kuwaelimisha wananchi wa Jimbo la Tumbatu umuhimu wa jambo la kuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa iwapo sheria hii itapitishwa rasmi na Baraza la Wawakilishi na hatimae kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, wapo watakaohoji uwezo wa kusema haya nimeupata wapi? Wasipate tabu kifungu cha 18 (1) na (2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na kifungu cha 66 (b) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi pamoja na ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 ambacho ndio chama changu zinaniwezesha kufanya haya niliyoyasema, lakini kama hayo ya vipengele vya sheria havitoshi basi niseme yafuatayo:

Mimi ni kiongozi wa watu niliyechaguliwa na watu natakiwa nijali maslahi ya watu na maslahi ya taifa kwa ujumla na sio maslahi yangu binafsi.

Mhe. Spika, napenda nimalize kwa kusema kuwa mimi Mtumbatu hivyo sitokuwa tayari kupoteza utamaduni wa Watumbatu kwa kuendeleza mifarakano na uhasama wa Watumbatu wenyewe kwa wenyewe nitaulinda, nitauendeleza, nitaudumisha mpaka mwisho wa maisha yangu naendelea

kuwaomba Watumbatu wenzangu waniunge mkono kwa maslahi ya nchi yetu. Mwenyezi Mungu mwenye uwezo wa kila jambo tunakuomba utusaidie. Amin.

Mhe. Spika, mimi ni kiongozi nikiwa kama kiongozi basi natakiwa niwe kioo cha jamii, sitochelea kueleza jambo jema kwa ninaowaongoza ili Mwenyezi Mungu apate kesho siku ya siku anihukumu kwa kile nitakachowaelekeza. Kiongozi ambaye anaogopa kuwaeleza watu waliomchagua bila shaka ameanza kupoteza umaarufu wa uhalali wake.

Kiongozi yeyote aliyechaguliwa na watu na anayekubaliwa na watu hatoacha kwenda kifua mbele kuwaeleza wananchi wake juu ya umuhimu wa jambo lenye maslahi ya nchi na maslahi yao wenyewe. Mimi nikiwa kiongozi niliyechaguliwa na watu nitakwenda kifua mbele, sasa kama wapo watakaonihukumu kwa hayo basi malipo yangu nitayasubiri kesho mbele ya Mwenyezi Mungu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wangu pia tunaunga mkono Mswada wa Sheria ya Masharti ya Kufanyika Kura ya Maoni na mambo mengine yanayohusiana na hayo kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Nimewaona Waheshimiwa Wajumbe wakinyanyuka pengine wanataka kuchangia lakini hapa walikuwa wanaunga mkono maneno haya.

Mhe. Zahra Ali Hamad (Kny: Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, naomba na mimi kwa upande wa kambi yetu nitoe maoni kuhusiana na Mswada wa Kura ya Maoni.

Mhe. Spika, naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sisi tuliopo hapa kuwa wazima na wenye afya. Naomba pia nikushukuru wewe kwa kunipa mimi nafasi hii ya kutoa mchango wangu kuhusu kuwepo kwa suala la kura ya maoni.

Mhe, Spika, mimi nimebahatika kuwa mswada huu ulipopita katika kamati inayohusika, mimi nilihudhuria. Hata hivyo, nathubutu kusema kuwa mswada huu tumeukubali kuanzia kwenye kamati hiyo na mpaka hapa katika Baraza pamoja na marekebisho yake yote.

Mhe, Spika, hata hivyo, kwa niaba ya kambi yetu na kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mgogoni tunasema kwamba mswada huu ni kwa maslahi ya taifa la Zanzibar na sisi tunaukubali.

Mhe. Spika, hata hivyo, kuna baadhi ya vifungu ambavyo hata kama tumevipitisha lakini ni wajibu wetu kuviwekea mkazo kwa ajili ya umuhimu wake, na kwa maana hiyo kumtaka Mhe. Waziri atuhakikishie utekelezaji wake jinsi utavyokuwa. Kwa mfano, kifungu cha 8 kinaelezea wazi kuwa mtu yeyote ambaye wakati wa kura ya maoni atakuwa ameandikishwa katika daftari la kupigia kura basi atakuwa na uwezo wa kupiga kura ya maoni. Mhe. Spika, hili ni jambo zuri na kwa ukweli ndivyo inavyofanyika ulimwengu mzima. Kila nchi huwa na daftari moja tu la wapiga kura, iwe kura ya maoni au kura katika uchaguzi wa kawaida.

Mhe. Spika, lakini suala zima liliopo hapa ni suala la kura ya maoni ambayo kila Mzanzibari anatakiwa aeleze hisia yake kuhusu suala fulani ambalo linawekwa kwa wakati ule.

Mhe. Spika, hivi sasa tatizo liko kidogo ni kwamba baadhi ya Wazanzibari hawajapata kusajiliwa kutokana na sababu mbali mbali. Naamini kuwa Mhe Waziri atafanya jitihada zake zote kuona kuwa wale waliokuwa hawajaandikishwa basi waandikishwe ili wasipoteze fursa hii muhimu na ya kihistoria, ninaamini hivyo hasa ukitilia maanani Mhe. Waziri ambaye kuanzia katika kamati mpaka hapa amesisitiza umuhimu huu na umuhimu wa kila Mzanzibari kupata haki yake. Kwa hivyo, na mimi naungana mkono naye kwamba tutajitahidi kuendeleza ili wote wale wanaohusika waweze kuandikishwa.

Mhe, Spika, kifungu 9(3) nacho kinahitaji kutazamwa katika utekelezaji wake. Ni vyema Tume iwe na uwezo wa kumruhusu mtu yeyote kuwepo kwenye vituo, kwa utaratibu wataouandaa kuliko kuweka lile neno la kuipa Tume uhiari wa kuweza kumruhusu mtu au la.

Mwisho kabisa chini ya kifungu cha 19 Tume ielezewe umuhimu wa kuweka Kanuni za kuwataja watu ambao wataingia au kuruhusika kuwepo katika vituo vya upigaji kura katika vituo vya upigaji kura na uhesabuji kura.

Mhe. Spika, haya niliyokuwa nikitaka kuyasema kwa bahati nzuri Mhe. Haji Omar Kheir ameyazungumza sana na kwa kina kabisa, sina haja tena ya kuyarejea mimi binafsi naunga mkono maelezo yake yote aliyoyasema kwamba suala hili ni suala la kitaifa, ni suala ambalo lina umuhimu wake katika nchi, pia ni suala ambalo linatuunganisha. Kwa hivyo, mimi kwa niaba ya kambi yetu ya upinzani na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mgogoni tunaunga mkono asilimia mia kwa mia suala hili na mswada huu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kuzungumzia mswada muhimu sana katika historia ya nchi yetu. Naomba nianze kwa kuipongeza sana serikali kwa kuleta mswada huu. Naipongeza kwa sababu mswada huu umekuja kufuatia azimio la Baraza lako Mhe. Spika, kwa hiyo serikali pamoja na kazi zake nyingi na kubwa lakini ikaona kutuheshimu na kutupa nafasi kama ambavyo tuliazimia katika kikao kilichopita kwa kweli inastahiki kupongezwa sana. Kwa maana hiyo ndio nikaamua kuanza na hilo.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba kupitishwa kwa sheria hii kunafungua historia nyengine katika demokrasia ya nchi yetu kwamba sasa wananchi wetu watakuwa na sauti pana zaidi ya kufanya maamuzi katika mambo mazito ya nchi yetu. Kwa sababu kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba sheria hii ndio itakuwepo, kwa maana haipo kwa sababu ya suala ambalo lilitokana na azimio tu lakini ni suala ambalo ni endelevu.

Kwa hivyo, wananchi wetu kupata fursa hii Mhe. Spika, ni jambo kubwa na pia ni heshima ya Baraza lako kuwa linaweka historia katika maamuzi kwamba angalau kesho na keshokutwa kama wengine hatutarudi katika Baraza hili basi tutaweza kujipiga mitaani kwamba ni sisi ndio ambao tumeweka sheria wananchi wawe na uwezo wa kupiga kura ya maoni. Mhe. Spika, hili ni jambo kubwa sana na sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi turekebisheni hii sheria kwa sababu inatupa kujigamba zaidi na wananchi wetu tumewapa fursa kubwa sana.

Mhe. Spika, mswada huu sio mkubwa sana na kwa hivyo mchango wangu mimi hautakuwa mkubwa ila nitatoa na mimi kidogo pale ambapo nahisi tujaribu kuimarisha au kuufanya bora huu mswada. Mhe. Spika, katika kifungu cha 4 kuna suala la kura ya maoni kupewa Tume ya Uchaguzi kama ni dhamana.

Mimi sina tatizo na hilo na kwa kweli ndio wenyewe, ila tatizo langu ni kuwa hili jambo letu mwaka huu kwa sababu tunategemea baada ya mswada huu kupita mambo yakenda kama tunavyokwenda kutokana na azimio letu basi kabla ya uchaguzi ifanyike kura ya maoni. Inshaallah itakuwa hivyo na itakuwa ya ndio kwa Wazanzibari wengi.

Mhe. Spika, ikiwa ni hivyo Tume ya Uchaguzi mwaka huu nayo imo katika maandalizi ya uchaguzi mkuu. Kwa hivyo, sekreteri ya Tume ya Uchaguzi itakuwa na mambo mawili makubwa. Kwanza imo katika utaratibu wa maandalizi ya uchaguzi mkuu, halafu tunaipa jukumu la kufanya maandalizi ya kura ya maoni, ni jambo jipya na linahitaji uwezo na linahitaji utaalamu. Kwa hivyo, ushauri wangu mimi nataka hili la mwaka huu ningemuomba Mhe.

Waziri akashauriana na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi pawe na sekreteriati ndogo ya kusimamia suala hili la kura ya maoni ya mwaka huu. Ile sekreteriati tuliyonayo iachwe ishughulikie suala la uchaguzi mkuu bila ya kufanya *interference* na suala la kura ya maoni.

Mhe. Spika, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi akishirikiana na Mhe. Waziri au kwa utaratibu ambao Katiba na sheria inaruhusu awe na mamlaka ya kuunda sekreteriati nyengine ndogo ya muda ya kusimamia suala hili ili kuona kwamba jambo hili limekwenda kwa ufanisi bila ya kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi aliyepo au wasaidizi wake wakashughulishwa na mambo mawili. Huku kuna daftari linaendelea, kuna matatizo yake halafu na huku kuna suala la kura ya maoni. Kwa hivyo, nahisi kwamba wanaweza wakaingia katika hali ambayo inaweza ikawapa ufanisi ambao ukawa sio mzuri. Hili ndilo ambalo nilitaka nilishauri kidogo.

Mhe. Spika, kipengele chengine ambacho na mimi nataka nizungumzie ni kipengele cha nambari 8. Mtu yeyote wakati wa kura ya maoni atakuwa ameandikishwa katika daftari la kudumu atakuwa na haki ya kupiga kura katika kura ya maoni. Hili nalo silipingi na ndio hasa inavyotakiwa iwe.

Mhe. Spika, lakini tuna tatizo ambalo nalo linahitaji ufumbuzi kwamba watu wetu wengi wanaweza wakakosa fursa hii ya kihistoria, kila mtu anataka ajigambe na hili kwamba na mimi nilishiriki kutoa maamuzi. Kwa hivyo, ningeshauri taasisi zinazohusiana na suala la kumfanya Mzanzibari awe mpiga kura basi ziandae mazingira ambayo yatarahisisha kuona kwamba watu wetu wengi kabla ya wakati huo wamepata fursa ya kuwa wapiga kura.

Mhe. Spika, mara moja mwezi wa kumi mwanzoni niliwahi kufanya mazungumzo pale katika Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Wete, alikuwepo pia Mkuu wa Wilaya ya Micheweni na baadhi ya viongozi na Mkurugenzi wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, hapo tulikuwa tunabadilishana mawazo ya kikazi juu ya suala hili. Mhe. Spika, hapo tukakubaliana kwamba Wazanzibari wengi wanakosa kuwa na kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi tu kwa sababu hawana cheti cha kuzaliwa, maana huwezi kuwa na kitambulisho kama huna cheti cha kuzaliwa.

Pia kuna baadhi ya watu wetu mpaka hivi leo ndio sasa wanaanza kuzinduka kwamba kumbe cheti cha kuzaliwa ni muhimu sana. Kwa hivyo, tukakubaliana na Mkurugenzi mbele ya Wakuu wa Wilaya wote wawili kwamba kuna umuhimu wa watu wetu wapate vyeti vya kuzaliwa ili iwe rahisi kwao kupata *ID*, kwa sababu *ID* si tu ni muhimu katika suala la kupiga kura lakini kuna *application* nyingi katika sera na katika mambo mengine.

Mhe. Spika, tuligundua kwamba tatizo kubwa la watu ambalo hawana vyeti vya kuzaliwa ni ule utaratibu lakini zaidi ile faini iliyowekwa ili mtu ambaye hana awe na cheti cha kuzaliwa. Yaani inaanza kwa Sheha, Mahakamani, kwa Mkuu wa Wilaya, hayo mtu anaweza kujipiga lakini sasa ile fedha Shs.40,000/=. Kwa hivyo, kama ndani ya nyumba mna watu hawana vyeti vya kuzaliwa kwa hiyo itakuwa ni shilingi arubaini mara tano itakuwa ni shilingi laki mbili. Kwa mtu mnyonge wa Gando anayelima muhogo akauza kidogo akapata *life* kumwambia atafute shilingi laki mbili aende akagomboe vyeti, jambo hilo si rahisi hata kidogo.

Kwa hivyo, tulikubaliana na mkurugenzi kwamba arudi serikalini afanye mambo mawili kwanza. Kwa sababu hili la faini ni suala la kanuni sio suala la sheria ya Baraza ni suala ambalo limetungwa na waziri. Kwa hivyo, hili linaweza likapunguzwa angalau likawa shilingi 10,000 lakini kwa shilingi arubaini elfu sio rahisi.

Kwa hivyo, tukakubaliana kwamba atarudi serikalini awaone mawaziri wanaohusiana na masuala haya wajaribu kupunguza ile faini kubwa ya wananchi ili wawe na uwezo wa kumiliki vyeti vya kuzaliwa. Pili ile *process* ya kufuata Unguja nayo ni shida, kwamba mwananchi hata akishapata hizo shilingi arubaini elfu inabidi naye atafute tena shilingi sitini elfu aje Unguja halafu arudi.

Kwa hivyo, tulikubaliana azungumze na waziri kuifanya afisi ilioko Pemba iwe na uwezo wa kufanya mambo haya. Mhe. Spika, lakini bahati mbaya muda mrefu umepita bado suala hili halijapatiwa ufumbuzi. Mhe. Spika, naamini Mkurugenzi maelezo yale aliyafanya kwa nia njema. Kwa hivyo, makubaliano yetu nawaomba Waheshimiwa Mawaziri anayehusika kwamba tuandae utaratibu ili wananchi wetu waweze kupata vyeti vya kuzaliwa ambavyo navyo viwawezeshe kupata vitambulisho ili iwe rahisi kuandikishwa katika daftari la wapiga kura.

Mhe. Spika, njia nyengine ambayo tulizungumza na yeye ilikuwa ni ngumu kwake ni kwamba suala la cheti cha kuzaliwa ni lazima awe nacho mtu ili aweze kupata kitambulisho nalo ni suala la kanuni sio suala la sheria ya vitambulisho. Kwa hivyo, nalo hili ni suala la kuliangalia kwamba tatizo hili limekuwa likizugumzwa na Wazanzibari sana. Hivyo nalo ni suala la kuliangalia ili tukalifanyia kazi na tujue je, kanuni hii ni kiasi gani inawasumbua wananchi wetu katika kupata haki hii muhimu ya msingi.

Mhe. Spika, kifungu chengine ambacho naomba nikizungumze kidogo ni suala la kutiliwa shaka kwamba tume itatangaza matokeo ya kura ya maoni na matokeo hayo hayatoruhusiwa kutiliwa shaka kwa namna yoyote isipokuwa

kwa kupeleka hati ya kuhoji matokeo ya kura ya maoni Mahakama Kuu. Mimi nahisi hii lugha iliyotumika hapa kidogo itafutiwe utaratibu zaidi kwa sababu mtu mpaka akifanya *process* ya kupeleka kesi Mahakama Kuu basi huyu mtu ameshakuwa na shaka, haiji tu hivi kama homa itakuwa mtu amekaa matokeo haya akayapima akayatilia shaka kwanza halafu ndio akafanya maamuzi ya kutafuta hati na mambo mengine ya kupeleka Mahkama Kuu. Kwa hivyo, hii lugha ya kwamba hayataruhusiwa kutiliwa shaka naona itafutiwe utaratibu mwengine, mtu hawezi kupeleka kesi Mhkamani kama hana shaka ya jambo. Suala hili naomba lifanyiwe kazi kidogo.

Eneo jengine ambalo nataka nizungumzie Mhe. Spika, nilikuwa naangalia sharti la mtu kuhoji matokeo ya maoni, ile amepata dhamana ya angalau idadi ya asilimia kumi ya wapiga kura wote katika kila mkoa sina tatizo nalo, lakini nilikuwa naangalia hii shilingi milioni tatu, niliona nyingi. Mimi bado nahisi kwamba zingelikuwa angalau shilingi milioni moja, moja na nusu au mbili basi ingewafanya watu wetu wawe na uwezo zaidi. Huo ndio *observation* yangu.

Lakini katika kifungu cha 11 pia kuna jambo ambalo naomba nipate ufafanuzi, naomba kunukuu Mhe. Spika, "Wingi wa kura katika kura ya maoni utachukuliwa kuwa ndio uamuzi wa mpiga kura katika suala au hoja ya kura ya maoni na matokeo yatakayotangazwa na tume yatalazimika kufuatwa na serikali".

Sasa hapa mimi nilikuwa nina wasi wasi kwamba serikali nayo itakuwa tumeifunga mikono, kwamba yenyewe lazima tuikubali, yenyewe itakuwa haina uwezo wa kuona kwamba labda kuna ghilba au jambo limefanywa na serikali yenyewe ikaamua kukata rufaa au kupeleka kesi Mahkama Kuu. Sasa nilikuwa nataka ufafanuzi kutoka kwa Mhe. Waziri je, serikali tuna maana ya kuifunga mikono au kuifanyaje katika suala hili.

Ni kweli tume imeshatangaza lakini matokeo yaliyotangazwa serikali inaona kwamba kuna ghilba ndani yake au jambo jengine ambalo serikali inaona halikubaliani nalo. Je, serikali ndio ifuate tu au wenyewe watakuwa hawana uwezo wa ku-*challenge* matokeo hayo Mahkama Kuu. Wananchi wamepewa nafasi hiyo, lakini je, serikali kama serikali nayo haikupewa nafasi yoyote?

Mhe. Spika, kifungu chengine ambacho nakitilia wasi wasi ni masuala ya *observers*. Mimi ningeshauri katika suala hili kama ambavyo imo katika utaratibu wa kura ya kawaida, basi tume ipewe jukumu la kuwaweka waangalizi maalum katika masuala haya kuhakikisha kwamba kumekuwa na uwazi katika suala zima la kura yenyewe. Vyenginevyo wananchi na hata dunia inaweza ikatulalamikia kwamba kura au utaratibu wetu umegubikwa na siri kubwa.

Mhe. Spika, kama nilivyosema awali kwamba mimi sina mchango mkubwa katika suala hili, nilikuwa nitoe ushauri wangu katika vipengele ambavyo nimevitaja. Lakini kimsingi suala hili ni muhimu na kwa kweli kama alivyosema Alhaji Haji Omar Kheir, alhaji wa muda mrefu na amekuwa endelevu kila mwaka anajitahidi kwenda kuona mwahala mutukufu. Kwa hivyo, kama alivyosema yeye na mimi namuunga mkono na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando naunga mkono hoja. Nakushukuru Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru sana. Kwanza nataka nitamke kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na pili nataka niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuleta hoja hii ambayo inatokana na azimio letu la Baraza. Hoja hii imezaliwa ndani ya Baraza lako tukufu, serikali ikaikubali na leo imeileta kwa maana hiyo sina sababu mimi ya kuikataa.

Mhe. Spika, naomba mwenyewe aniruhusu Mhe. Ali Haji Ali nimnukuu maneno aliyoyatoa katika kamati tulipokuwa tukipitia mswada wa Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo hivi juzi. Aliwauliza yeye na wenzake Naibu Waziri pamoja na watendaji wake, yeye alitaka kujua *legacy* yao nini katika kipindi ambacho wapo kwenye uongozi wa wizara hii. Na akawauliza kitu gani kinawanyima usingizi, yaani mambo gani ambayo watayaacha ya kujivunia katika uongozi wao, mambo gani ambayo muhimu wameyafanya na ya kujivunia na ambayo yatakuwa wamewaachia Wazanzibari katika utawala wao.

Akawauliza swali la pili ni mambo gani ambayo yanawanyima usingizi? Lakini Mhe. Waziri ni mtu mahiri kwa kujibu maswali na watendaji wake kwa kweli walimjibu Mhe. Ali Haji alifurahi. Walieleza sitaki kuyanukuu hapa hakuna haja, waliyoyafanya na vile vile wakayataja mambo ambayo yanawanyima usingizi.

Sasa mimi nasema katika jambo ambalo lilikuwa linanyima usingizi ni vyama vyetu vya *CUF* na CCM kwa muda mrefu vina mifarakano. Mimi najua kwamba viongozi wetu wote mifarakano ilikuwa inawanyima usingizi. Hili alilithibitisha Rais Benjamin William Mkapa wakati wa kutia saini muwafaka wa pili tarahe 10/10/2001 Ikulu Zanzibar. Alisema kwamba, nilikuwa sipati usingizi lakini kuanzia leo nitalala. Kwa maana hiyo, mifarakano inawanyima viongozi wetu usingizi.

Mimi nimsifu sana Mhe. Amani Abeid Karume kwa jambo moja, hana tabia ya Kigunya kwa sababu Mgunya akiumia hutaka na mwenzake aumie. Kuna

hadithi ya Kigunya, Mgunya mmoja alitia pahala mkono hivi, akakatwa mkono basi hakusema kama anaumia, alicheka ili na wenzake watie nao wakatwe. Sasa kama Mhe. Amani Abeid angekuwa na tabia ya Kigunya asingetatua matatizo ya Zanzibar hivi sasa, angewaachia Marais wajao hivi hivi na wao wakaja wakakuta matatizo kama waliyoyapata Marais waliopita ambapo na yeye vile vile aliyapata katika awamu ya mwanzo ya uongozi wake, lakini inaonekana huyu hana tabia za Kigunya, yeye kwa sababu kapata matatizo na wenzake wote wajao wapate matatizo.

Kwa hivyo, nadhani kama kuna watu wa kumpongeza Mhe. Amani kwanza ni Wazanzibari wote lakini pili wale watu wenye nia ya kugombea Urais wa Zanzibar. Ndio Mhe. Spika, kwa sababu yeye tayari anataka kuwaachia nchi safi, yenye umoja kama inavyozungumza Katiba haina matatizo, kama angekuwa mchoyo na mbinafsi basi angesema aah! wacha twende hivi hivi na wajao wapate adabu kidogo. Namsifu sana kwa hilo.(*Makofi*).

Mimi Mhe. Rais wa Zanzibar hajapatapo kunikosa katika maisha yangu yote, lakini kama angenikosea binafsi kama Haji Faki ningemsamehe kwa hili, lakini nashukuru mimi kama yeye na mtu binafsi hatujakosana. Lakini hata hivyo, kwa sababu ya migogoro iliyotokezea baina ya vyama basi pia nasema kwa niaba ya chama changu wanachama wa *CUF* tuna haki ya kumsamehe kwa hili.

Mhe. Spika, mkulima mzoefu akilima hatizami nyuma, ukiona mtu analima halafu anatizama nyuma hivi huyo si mkulima, mkulima mzoefu akilima huangalia mbele, lakini mkulima ukiona analima anaangalia nyuma anaona loh! Nilipopata pakubwa hapa sasa niende zangu si mkulima huyo. Hiyo ni *principle* ya mkulima.

Bahati nzuri mimi nimezaliwa katika ukoo wa kimaskini wa wakulima na nilikuwa nalima na mpaka hivi sasa Mhe. Spika, mimi ninao muhogo wa mwari ukiutaka nitakuletea, ujue kwamba mimi ni mkulima, ukiniambia Mhe. Haji Faki Shaali niletee mtwike nitakuletea, mimi kama kaka yangu Dr. Mwinyihaji Makame bwana nalima. Sasa hiyo ndio *principle* ya mkulima.

Mhe. Spika, ukiona mkulima analima anaangalia nyuma akaona aa sehemu niliyopata kubwa sasa hivi niende zangu si mkulima huyo, mkulima anaangalia mbele na akichoka basi anatafuta kibiriti anawasha moto yale mabiwi kutayarisha ucheu wake wa kesho. Sasa Mhe. Spika, na sisi tuige nadharia ya wakulima. Baraza lililopita tumefyeka pori, mara hii tunaanza kuchimbua, sasa tuwe na malengo ya kwenda mbele sio kurudi nyuma. Nadhani itakuwa nimeeleweka wala haihitaji ufafanuzi mkubwa zaidi.

Mhe. Spika, baada ya tarehe 5 Novemba, walipokutana Maalim Seif Sharrif Hamad na Rais wa Zanzibar Ikulu, Mhe. Amani Abeid Karume kwanza kwa upande weti sisi wana *CUF* hapakuwa na furaha na yaliyojitokeza sote mashahidi. Katika mkutano wa Kibanda Maiti, Maalim Seif alidhalilishwa, alizomewa, lakini baadae kidogo kidogo baada ya watu kufahamishwa wakafahamu wakatulia.

Inawezekana sina hakika ikawa wako wana *CUF* wasioridhishwa na mambo haya, mimi sina ushahidi kwamba wapo lakini ikiwa wapo sishangai ni khulka ya binadamu si watu wote wanaopenda mema. Kwa sababu kama wapo wapenda mema bangi isingenunuliwa, Misikiti yote iliyopo Unguja kuna haja ya mtu kununua bangi?

Lakini bangi inanunuliwa, unga unanunuliwa, gongo linanunuliwa, kwa maana hiyo, si watu wote wanaopenda mema. Kwa hivyo, mimi nawahesabu wasiounga mkono kura hii kwamba ni haki yao ya kidemokrasia lakini kwa kuzingatia vile vile kwamba si watu wote duniani watakaopenda jambo jema.

Mimi siwezi kufikiria kwamba Wazanzibari wote kwa asilimia mia moja wataunga mkono hili jambo. Kwa sababu hiyo Mwenyezi Mungu ndivyo alivyoweka si watu wote wanaopenda mema iwe ya kidunia au kiakhera na usingeumbwa moto ati. Lakini imani yangu kuwa humu ndani hatatokea mtu akaikataa, hiyo ndio imani yangu. Kwa nini Mhe. Spika, nikajipa imani hiyo? Mhe. Haji Omar Kheir kwa kweli kazungumza mambo *very philosophical*.

Lakini Mhe. Spika, ukija katika Katiba ya Zanzibar, kifungu cha 9(1) kinasomeka hivi:-

> Kifungu cha 9(1) "Zanzibar itakuwa ni nchi ya kidemokrasia na haki za kijamii".

Kwa hivyo, hapa inaelezwa rasmi kwamba mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa serikali kufuatana na Katiba utatokana kwa wananchi wenyewe. Sipo ninapopataka hapo.

Kifungu cha 9(1)(b) kinasema,

> "Usalama na hali nzuri kwa wananchi itakuwa ndio lengo kubwa la serikali".

Hapa ndipo ninapopataka. Sasa Mhe. Spika, ikiwa usalama na hali nzuri kwa wananchi itakuwa ndio lengo kubwa la serikali, sasa vipi mtu akatae kura ya maoni, au vipi mtu akatae dhamira nzuri ya Chama cha Mapinduzi na vyama vyetu vyengine ya kuleta umoja katika nchi. Ndio nikasema kwamba sitegemei

kwa humu ndani kwamba atatokea mtu kuwa atapinga, kwa sababu hii Katiba yetu inaeleza wazi wazi kuwa usalama na hali nzuri kwa wananchi itakuwa ndio lengo kubwa la serikali.

Kukataa haya ina maana wewe hukubaliani na usalama na hali nzuri katika nchi, ndio nikaamini basi kwa *spirit* hii ya Katiba hatatokea mtu humu ndani akakataa hili, kwa sababu sisi lengo letu ni moja tu, sio Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya tu, tukafikiria kwamba ndio wenye jukumu la kulinda amani hapana.

Sisi sote tuna jukumu la kulinda usalama na amani katika nchi na sote tuna jukumu la kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaishi bila ya bughudha, fitna, kwa sababu wananchi wanapohasimiana ikawa hawazikani sababu ipi tunayoipata? Haipo isipokuwa matatizo tu yanayotukumba. Kwa maana hiyo sina sababu nisiunge mkono mswada huu na hata hapo itakapokuja nitakuwa sina sababu ya kuwaelimisha wananchi wakaunga mkono azma nzima hii ya Chama cha Mapinduzi na serikali ya kutaka kuleta umoja kwa watu wetu.

Mhe. Spika, Mhe. Said Ali Mbarouk amejaribu kueleza baadhi ya changamoto ndogo ndogo ziliopo. Mimi nasema Mhe. Spika, hata serikali ikawa chama kimoja changamoto ndogo ndogo lazima zitakuwepo, ikiwa ya vyama vingi pia zitakuwepo, tukiwa katika hali hii ya maridhiano tuliyonayo siku moja hatuwezi kulala na kuamka ikawa tumemaliza mambo yote nasema hilo haliwezekani.

Ndani ya chama chenyewe kila chama lazima kitakuwa na changamoto, CCM watakuwa na changamoto zao ndani ya chama chao, *CUF* hivyo hivyo, CHADEMA hivyo hivyo. Kwa hivyo, changamoto lazima ziwepo. Lakini mimi imani yangu ni kwamba haya matatizo madogo madogo serikali kwa sababu imedhamiria kweli kweli na sio masikhara katika suala hili, basi imani yangu kwamba yale aliyoyazungumza Mhe. Said kwamba yatapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, ndio jambo lolote linavyoanza, siku zote jambo lolote jema kwanza hupokelewa na juu, mlipokee nyinyi viongozi juu ikisha na waliokuweko chini ndio watalipokea. Sasa tusitegemee waheshimiwa hasa sisi tunaotoka katika kambi ya upinzani kwa sababu Rais wa Zanzibar suala hili kishalipokea vizuri, Waziri Kiongozi kishalipokea vizuri, Naibu Waziri Kiongozi kishalipokea vizuri, Mawaziri na Wawakilishi wote wameshalipokea vizuri, tusitegemee kwamba hawa walioko chini na wao siku moja watalala na kuamka watalipokea vizuri. Kwa sababu *main set,* kubadilika yangu mimi na Mhe. Naibu Waziri Kiongozi mara moja unaweza ukaibadilisha, lakini huyu wa chini si rahisi. Sasa nasema hiyo ni changamoto iliyopo. Lakini mimi imani yangu kwamba na hawa wenzetu walioko chini watabadilika.

Mhe. Spika, unajua katika masuala haya ya ulinzi na usalama kuna istillahi wenzetu wanatwambia kuna watu wanaitwa *passive enemies* yaani maadui waliokuwa si wa moja kwa moja, anaweza akaweko mwana-*CUF* mzuri sana akafanya matendo lakini yale matendo yanakihujumu chama chake yeye mwenyewe hajui, huyu anaitwa ni *passive enemies* au anaweza akaweko mwana-CCM mzuri sana au mfanyakazi wa serikali mzuri sana mtiifu wa Chama cha Mapinduzi akafanya matendo lakini yale matendo yanaidhalilisha serikali yake lakini mwenyewe hajui, sasa huyu ni *passive enemies*.

Sasa nasema *passive enemies* kila pahala lazima atakuwepo. Mtu unaweza kumhangaisha kwa haki yake ukaona wewe labda ndio unakijengea uhalali chama chako lakini kumbe unakibomoa chama chako. Sasa watu kama hao mimi natarajia hatuwezi kuwamaliza kwa siku moja, yaani watu waliokuwa maadui lakini hawajui kama wanakifanyia uadui au serikali yao, hawa Mhe. Spika, lazima wawepo.

Hata mimi jana nimepata kesi kama hii lakini nikamwambia mtu usishughulike haya mambo yatamalizika. Kuna mkwe wangu kaowa mtoto wa mke wangu mdogo, alikuwa anaishi Michenzani akahama mwaka 2004 kajenga nyumba yake Mwanakwerekwe. Sasa alipokwenda katika daftari; jimbo la Mhe. Waziri Kiongozi nadhani lile Mwanakwerekwe karibu na ile skuli ya sekondari ya Kiislamu. Sasa alipokwenda katika daftari wakanyimwa haki yao.

Lakini bahati nzuri basi, walipohama Michenzani walichukau barua ya Sheha na walipokwenda kule wakaripoti kwa Sheha mpya Mwanakwerekwe, na ile barua ya Sheha wa Michenzani kwenda kule bahati nzuri waliitoa *photocopy*, sasa walipokwenda kujiandikisha katika daftari wakaambiwa kwamba nyinyi hatuwatambui hapa, lakini huyu mtu nyumba hajakodi ni yake mwenyewe na ipo karibu na ile skuli ya sekondari ya wanawake pale, kwa kweli akakosa.

Sasa mimi aliponisikitikia nikamwambia basi akasema haya ni maridhiano gani? Nikamwambia maridhiano yapo kwa sababu umekosa haki wewe mtu mmoja ndio hapana maridhiano? Nikamwambia haya ni mambo madogo madogo ambayo yanaweza yakashughulikiwa na nina imani kwamba haki yake atapatiwa. Kwa sababu nyumba ni yake mwenyewe kajenga, anaishi pale miaka sita, alipohama barua ya Sheha kachukua, sasa nikajua hawa aliokumbana nao ni hawa niliowazungumza hapa *passive enemies*, wale watu ambao wanaona labda nikifanya hivi, labda chama changu kitanisifu, serikali yangu itanisifu kumbe anaiharibia serikali yake bila ya yeye mwenyewe kujua.

Sasa mimi nasema *passive anemies* serikali itafute namna yaku-*deal* nao nakusawazisha changamoto ndogo ndogo kama hizi, lakini nafikiri kwa *spirit* tuliyoiupata sasa hivi hii mimi hainikatishi tamaa nina imani kwamba watu

wote waliokuwa hawajapatiwa haki zao hizi serikali itawapatia kabla ya kuingia katika mchakato huu wa kura ya maoni na uchaguzi mkuu.

Kwa hivyo, mimi nasema hizi ni changamoto ndogo ndogo zisitukatishe tamaa na wala wananchi wasikate tamaa, lakini nafikiri tuwahamasishe wananchi wetu waendelee kutafuta haki zao kwa njia za amani ili tusirejee tena katika migogoro iliyokuwa haina maana, tuhamasishe wananchi wetu waliokuwa hawajapata vitambulisho watafute njia muwafaka za kutafuta haki zao ili wazipate na nina imani kwa serikali sasa hivi haitaki tena kuzungumzwa vibaya hili watalirekebisha.

Mhe. Spika, nina imani kwamba kadri elimu itakavyoteremka chini kidogo kidogo basi wananchi wetu wote pande zote mbili wataelimika na kuliunga mkono suala hili.

La mwisho Mhe. Spika, mimi nina salamu za watu wa Mkanyageni, baada ya Baraza lililopita mimi nikarudi katika jimbo langu, kwa kweli Mhe. Spika, watu walifurahi sana, watu wa vyama vyote viwili kwa sababu mimi jimbo langu sijawa na wanachama wa CHADEMA, sijui wamejificha lakini naona ni vyama viwili tu, *CUF* na CCM.

Kwa bahati nzuri katika jimbo la Pemba ambalo CCM kidogo wapo ni jimbo langu, ndio ukweli ati, kwa sababu mimi nina Shehia tano. Shehia ya Michenzani ambayo ndio kubwa kwa *population* asilimia 90 *CUF*, Kisiwa Panza asilimia 90 *CUF*, Mkanyageni asilimia 65 *CUF*, Shidi asilimia 65 *CUF*, lakini Chokocho asilimia 60 CCM. Kwa hivyo, hata Diwani mmoja mimi sipati chama changu. Kwa hivyo, lazima niishi kwa heshima na adabu kwa sababu kule kuna watu wa chama chengine, lazima niwaheshimu niwape haki yao na mimi wanipe haki yangu.

Lakini Mhe. Spika, nililogundua baada ya kupita lile azimio tulilolipitisha katika Baraza lilipokwenda kule kwetu kwa kweli nilifurahi sana, kwa sababu niliwakuta wananchi wamefurahi na wananchi nilivyogundua ni kuwa hawataki kurudishwa nyuma. Kama kuna mtu anayetaka ajimalize kisiasa awe *CUF* awe CCM ajaribu sasa hivi kupingana na mambo haya.

Mhe. Spika, mimi nina hakika mapenzi yote niliyonayo kwa wananchi wangu kama nitalipinga suala hili watanikataa. Lakini vile vile nina hakika kama atatokea mwana CCM yeyote akatumia labda jukwaa la kupinga suala hili apate uhalali wa kisiasa atakwenda na maji. Kwa hivyo sasa hivi nataka niungane na somo yangu, mwanasiasa atakayetumia uhalali wa kisiasa kwa kupinga hili anajimaliza. Kwa hivyo, sitegemei kwa sababu wanasiasa ni watu

wanaoangalia maslahi yao pia kwamba hakuna sasa hivi mtu atakayekataa mwelekeo mpya wa mageuzi tunaokwendanao.

Mhe. Spika, nakushukuru ahsante na naunga mkono hoja.
Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Bismilah Rahman Rahiym. Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia mswada huu muhimu wa historia katika nchi yetu.

Kwanza kabisa naomba fursa hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutokana na kutekeleza yale ambayo yaliamuliwa Barazani hapa kwa kutuletea sheria hii kwa wakati unaofaa kabisa.

Pili naomba kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa hapa katika kuwasilisha hoja hii. Lakini tatu nataka nimpongeze ndugu yangu Mhe. Haji Omar Kheir kwa namna alivyoweza kueleza yale yote ambayo yamo katika moyo wake wa haki kabisa na kuunga mkono hoja hii kwa umakini mkubwa sana.

Mhe. Spika, kwa kweli hoja hii imeandikwa vizuri na yale marekebisho kuwa yamerekebishwa. Vile vile mazuri kabisa isipokuwa tu katika ukurasa wa pili wa marekebisho ningeomba irekebishwe tena kwenye kifungu cha 10(1), matokeo hayendi kusomeke basi. Lakini kwa kweli sheria imetungwa ikatungika na mambo mengi ambayo yameathiri kwa njia moja au nyengine yamewekwa sawa. Kwa hivyo, shaka imepungua kwa kiasi kikubwa sana kwa sheria hii.

Isipokuwa ningeomba kidogo tu kuchangia katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza katika kifungu cha 4, Haki ya Kupiga Kura ya Maoni. Mtu yeyote wakati wa kura ya maoni atakayekuwa ameandikishwa katika daftari la kudumu la wapiga kura atakuwa na haki ya kupiga kura katika kura ya maoni. Hapa Mhe. Spika, ndio penye shaka juu yangu kuhusu hili daftari la kudumu.

Daftari la kudumu limeandikwa na linaendelea kuandikwa lakini lina utata mdogo ambao mimi nina imani kabisa kwamba serikali ikilivalia njuga suala hili litaondoka kabisa. Tukiangalia Katiba ya Zanzibar imesema wazi. Kifungu cha 6(2):-

Kifungu cha 6(2)

> "Kila Mzanzibari, kwa misingi ya Katiba hii, ataweza kufaidi haki na fursa zote anazostahiki Mzanzibari, na atapaswa kutekeleza wajibu, majukumu na dhamana za Mzanzibari kama ilivyo kwenye Katiba hii au kwenye sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi".

Kifungu cha 7(1) kinasema:
Kifungu cha 7(1)

> "Kila Mzanzibari aliyetimiza umri wa miaka kumi na nane anayoa haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Zanzibar na wananchi. Na haki hii itatumiwa kwa kufuata masharti ya kijifungu cha (2), cha kifungu hiki…" na kuendelea.

Ukienda mbele katika ukurasa wa 5 kunasema kwamba, "mbali na sababu zilizoelezwa katika kifungu hiki hakuna sababu nyengine yoyote inayoweza kumzuia Mzanzibari asitumie haki yake ya kupiga kura".

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ukiangalia haki za kikatiba kila Mzanzibari apate fursa ya kupiga kura na kuweza kusema ndio au hapana juu ya kura hii ya maoni inayofuata.

Ukienda katika Sura ya Tatu ya Katiba yetu, ni usawa mbele ya sheria. Vile vile inasema kwamba, "Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria". Ikiendelea inasema "Hakuna sheria itakayokuwa na kifungu chochote ambacho ni cha ubaguzi wa moja kwa moja au kwa taathira yake". "Hakuna mtu atakayebaguliwa na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya sheria yoyote au katika utekelezaji wa kazi ya ofisi yoyote ya serikali au uongozi mwengine wa chama chochote na vyombo vyake".

Baada ya kunukuu vipengele hivyo vya Katiba utakuta zoezi la kuandikwa daftari kuna baadhi ya watendaji hawaviangalii vipengele hivi na kwa hivyo wanawanyima fursa baadhi ya Wazanzibari ya kuandikishwa katika daftari hili. Daftari ambalo litawapa nafasi waweze kupiga kura ya maoni na kuweza kusema kauli yao pamoja na Wazanzibari wenzao wakajumuika kwa pamoja juu ya hoja hii.

Mhe. Spika, huo ndio wasi wasi wangu mkubwa. Kwa hiyo, naomba vyombo vyote vinavyohusika kuzingatia masuala haya kwa kina na kuona kwamba kila Mzanzibari anastahiki kupiga kura apewe fursa hiyo ili aweze kushiriki moja kwa moja bila ya pingamizi yoyote katika kusema kwamba anataka Serikali ya Umoja wa Kitaifa au la. Hiyo ndio itakuwa sheria na katiba zetu tunazifuata.

Mhe. Spika, kuwa na kura ya maoni katika Zanzibar ni suala kubwa sana, ni suala la kihistoria, si Tanzania tu, lakini katika Afrika nzima. Hii itatupa sifa kubwa kwamba Zanzibar sasa hivi imetanuka kidemokrasia. Kama katiba yetu inavyoeleza katika ukurasa wa 3 kifungu cha 5 kwamba "Zanzibar itafuata mfumo wa kidemokrasia wa vyama vingi vya siasa vyenye kuheshimu utawala wa sheria, haki za binadamu, usawa, amani, haki na uadilifu". Vile vile katika

ukurasa wa 6 kifungu cha 9 “Zanzibar itakuwa ni nchi ya kidemokrasia na haki za kijamii”.

Kuweza kuweka sheria hii katika sheria zetu kutatanua wigo mpana zaidi na mkubwa zaidi wa demokrasia katika nchi yetu na tutakuwa mfano bora wa kuigwa na nchi mbali mbali za Afrika. Wananchi wote wa Zanzibar, wa Tanzania, wa Afrika na dunia nzima wataangalia kwa macho yote kuona kwamba kura hii itakapopigwa ya maoni Zanzibar inafanikiwa au la. Sisi wajibu wetu ni kutunga sheria, kuziweka sheria safi kabisa ambazo zinatekelezeka, ili zitekelezwe tuweze kupata sifa hiyo kwamba sheria imetungwa na sheria imefuatwa.

Kwa sababu kutunga sheria ni suala moja na kufuata sheria ni suala jengine. Sisi tunaweza tukatunga sheria lakini wakatokea watu ambao ile sheria wakaanza kuwa hawaifuati. Kwa hivyo, kutunga sheria ni suala moja na kufuata sheria ni suala jengine.

Mhe. Spika, ninavyosisitiza mimi kwamba tunatunga sheria vile vile tuweze kuangalia sheria tunazozitunga zinatimizwa ipasavyo. Kuona kwamba kila mwananchi mwenye haki aliyefika miaka 18 anapiga kura ya maoni na matokeo yatakayotokea yataheshimiwa na yatatoa sura kamili ya jawabu ya suala lenyewe na vile vile itatupa sifa dunia nzima kwamba Zanzibar ni nchi kweli yenye utawala bora na yenye kuelimika na kutanuka kwenye masuala ya kidemokrasia.

Mhe. Spika, hili ndio suala muhimu ndio nikasema kwamba wasi wasi wangu mimi ni kwenye daftari la kupiga kura, vitambulisho vya Mzanzibari, haya ni masuala ya kuangaliwa na kuona kwamba yanarekebishwa. Ninaamini kwamba yanarekebishika na nia hiyo kwa serikali ipo na *inshaallah* utekelezaji wake utafanikiwa, ili twende katika kupiga kura hii bila ya kuwa na manung’uniko ya aina yoyote kutoka kwa mtu yeyote. Ninaamini kwamba daftari likiwa safi na ikiwa kila mwananchi anapata fursa hii manung’uniko itakuwa hakuna na kitakachokuja katika matokeo hayo kila Mzanzibari atayaamini na atayakubali na hakutakuwa na matatizo yoyote yatakayofuatia. Mhe. Spika, huo ndio ulikuwa wasi wasi nafikiri utazingatiwa.

Mhe. Spika, tukiendelea mbele katika kuchangia hoja hii ukurasa wa 7 kifungu cha 19 (2) naomba kunukuu. “Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu cha (1) cha kifungu hiki, Tume inaweza kutunga kanuni kueleza yote au baadhi ya mambo yafuatayo:”

Mimi ningesema hapa Tume sio inaweza, ningeomba hili neno inaweza liondoke ije Tume itawajibika kutunga kanuni kueleza yote au baadhi ya

mambo yafuatayo ambayo hapo yamo katika mtiririko wake chini kama ilivyoelezwa katika sheria hii.

Mhe. Spika, baada ya kuchangia hayo, baada ya kusema hayo na baada ya kuzingua hayo, naomba kwa moyo mkunjufu kabisa kutamka rasmi kwamba hoja hii naiunga mkono mia fil mia na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atatuwafikisha.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu pamoja na kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja hii iliyokuwa mbele yetu, moja katika hoja muhimu sana kwa mustakbali wa nchi yetu katika miaka ijayo.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii tena kumshukuru Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, Mhe. Hamza Hassan Juma kwa uwasilishaji mzuri na ulioeleweka.

Nampongeza sana na kumshukuru sana Mnadhim na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mhe. Haji Omar Kheri, kwa kweli ameifanya kazi yetu kuwa rahisi, ametoa ufafanuzi mzuri, ameeleza vizuri, tulichobakia sisi ni kumaliza maliza hapa na pale au kuongeza vitu vidogo vidogo tu.

Mhe. Spika, nitatoa hadithi ndogo kabla sijaendelea. Kuna wakati kulikuwa kidogo na upungufu wa vyakula huko miaka nyuma. Sasa kuna mzee wetu mmoja kule Makunduchi alikuwa anatusaidia kwa njia zake anazozijua yeye mwenyewe. Bahati mbaya siku hiyo hakufanikiwa kupata vile vyakula, yaani vyakula anakusudia kule ni mchele, unga na sukari, akasema leo bahati mbaya nisameheni nimekuja na *fruit* tu.

Sasa tukasema labda ndizi, mapapai, machungwa, kumbe leo sikupata nimekuja na *fruit* tu maana yake kengele, spoki za baiskeli na hizi ndio *fruit* zenyewe. Sasa Mhe. Spika, Mhe. Haji Omar Kheri kamaliza kila kitu sisi tutaweka hizo *fruit* tu za juu lakini sio kengele za baiskeli, ni maneno.

Lakini Mhe. Spika, nichukue nafasi hii maalum kumshukuru kwa dhati kabisa na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Amani Abeid Karume. Mwenyezi Mungu amemjaalia ana kipaji cha aina yake, ana *vision*, mkweli, muadilifu na anawapenda sana Wazanzibari. Naomba tumshukuru kwa dhati kabisa kwa imani hiyo aliyokuwa nayo Rais wetu.

Mhe. Spika, Mhe. Haji Omar Kheri alizungumza kitu cha ushahidi na hali halisi ya Tumbatu. Pengine ukitazama Tumbatu tofauti na Makunduchi katika mazingira ya kisiasa. Makunduchi kule *Alhamdulillahi* mambo mazuri na

yanaendelea kuwa mazuri na yataendelea kuwa mazuri zaidi. Kwa sababu kufika wakati hata wanachama wenzangu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wa 2005 wakasema bwana hatuwekei mgombea ingia tu. Nilikuwa na tamaa hata CUF pengine wasingemuweka mgombea lakini tena ndio akawepo. Yote haya kwa sababu wananchi wa Makunduchi wameshirikiana katika kila ngazi *level* zote na wananchi wote.

Sasa jirani akiwa na matatizo na wewe yanakukera vile vile. Mhe. Spika, nasema kidogo kidogo pengine watu wengine wasisikie, kule nyumbani wakati mwengine mnaweza kutofautiana na mama watoto, sikusudii wewe najitolea mfano mimi, basi unaomba Mungu msijibizane ili jirani akasikia kama kunatokea mambo leo. Lakini pia unashukuru Mungu siku hiyo mkitofautiana kidogo aje mgeni pale nyumbani, akija mgeni unataka asiondoke mnazungumza kama ule ugomvi haupo. Mnazungumza mnafurahi baba yake nani mnaitana, akiondoka tu ehe, tunaanza upya.

Lakini ushwari ule ulipatikana kutokana na kuingia amani pale kuja yule mgeni. Sasa leo Rais wetu amekaa ametuletea amani katika nchi yetu sana. Mimi kipindi kifupi hiki nimefanya ziara katika mikoa yetu ya Unguja na Pemba Mhe. Spika, sura niliyoiona ni tofauti kabisa na miaka yote ambayo nimewahi kufanya ziara huko Pemba. Tumekusanyika Walimu Wakuu wa Mikoa, tumeona viongozi wa vyama vyote wameshiriki kwenye mikutano ile tena wamechangia sio kwamba wameshiriki tu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hivi karibuni namshukuru sana swahiba wangu hayupo hapa Sheikh Said Ali Mbarouk na Mhe. Khalifa walinialika nikenda Fundo na nikenda na kisiwa cha Uvinje nimepata mapokezi mazuri sana. Nashukuru mara nyingi nikenda napokewa vizuri lakini safari hii yamezidi kidogo.

Lakini pia nikafanya mkutano pale Mkoa wa Kusini Pemba katika mkutano ule ulihudhuriwa na swahibu wangu Waziri Kivuli Mhe. Mohamed Ali Salim (Mulla), pia alikuwepo rafiki yangu mpya Mhe. Abass Juma Muhunzi. Mhe. Spika, michango iliyokuwa inatolewa pale ilikuwa ni *very constructive*. Kuna mwenyekiti mmoja akataka kutetemesha kidogo ile hali ya pale, kataka kumuandama andama waziri hivi kwa baadhi ya mambo. Kasema waziri mambo hayendi huku kwa sababu ukiweka ahadi haitekelezwi. Umesema utawaongezea mishahara walimu mpaka leo hujafanya, sijui umesema hivi na hivi.

Hakusimama mwengine pale wala mimi sikutaka kujibu, alisimama Mhe. Abass Juma Muhunzi akajibu akamtetea Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Abass Juma Muhunzi alitoa tamko naomba uniruhusu nimnukuu kidogo. “Haya yalikuwa hayatendeki wakati ule kwa sababu ya wasi wasi uliokuwepo wakati ule”. Leo kifua mbele kazungumza pale walimu wakuu wote waliokuwepo pale wakamwona yule mwenyekiti kumbe si mtu makini. Kwa hivyo, inapotokea amani katika kijiji, nyumba au familia nakusudia katika eneo inakuwa ni hali ambayo inatutetemesha sote.

Mhe. Spika, Mhe. Juma Duni Haji ni mwalimu wangu mimi, alipotoka Chuo Kikuu mwaka 1975 ndio walimu wa benchi ya mwanzo iliyotoka kule kama sikosei akapangiwa Nkrumah, kanifundisha Chemistry mimi ipo kidogo imebakia. Sasa mle darasani kasahau mlikuwa na watoto wengine wakorofi kidogo, lakini tunapofanya ukorofi basi siku moja alisema huyo “Mkipiga kelele nyinyi mnawaudhi na wenzenu huku, hebu tulieni”. Tuko kwenye *practical* pale na kwenye *practical* ukiingia *laboratory* unatakiwa uwe mtulivu.

Lakini hii maana yake kama Tumbatu hali si shwari, kama Mkanyageni hali si shwari, kama Mkokotoni hali ni shwari mfano, lakini pale Chaani si shwari, basi ina-*disturb* kila sehemu ambayo ni shwari.

Kwa hivyo, wananchi wa Makunduchi tulikuwa tunahuzunika sana na yale ambayo tunayasikia na mimi ni shahidi nimeyaona mengine kwa macho yangu yaliyokuwa yanatendeka wakati ule. Nilisema hapa Mhe. Spika, wakati ule nachangia hoja hii na leo nasema tena, hatuko tayari kurudi katika karne ile ambayo tumetoka. *(Makofi)*

Niliseme kwa Kiingereza kwa sababu ninacho kidogo. *We are not ready to go back to that error, that error has gone.* Nasema tena kwamba kweli ile *error* imekwenda.

Mhe. Spika, hoja iliyokuwa mbele yetu ni muhimu sana na napenda niwahakikishie kwamba ili hoja hii ifike kwa wahusika yaani wananchi wenyewe sisi tuwe walimu. Mimi *by profession* ni mwalimu *Alhamdullilahi*, kama alivyokuwa Maalim Juma Duni Haji, Mhe. Haji Faki Shaali, Mhe. Mohamed Ali Salim (Mulla) na wengineo. Ninapokwenda darasani nikifundisha siwezi kwenda darasani nikasema hesabu hii ni ngumu. Sasa unakwenda darasani umeshawaambia wanafunzi hesabu ni ngumu, moja kwa moja hesabu ile itakuwa ngumu, nadhani walimu wananielewa vizuri.

Kwa hivyo, unapokwenda kufundisha kitu uwaambie aaaa *it is very simple*, hesabu hii. Mhe. Spika, kweli maadam kitu unakijua utakieleza lakini uwe na *confidence* na ukiamini kile unachokisema kwamba ndicho. Sasa kabla hatujafika kutoa taaluma ile, kwanza wewe unayekwenda kutoa taaluma ile uamini kwamba kile unachokipeleka ndicho.

Mhe. Spika, mimi naamini humu ndani sote tunatakiana mema, tunatakiana kheri na maelewano mazuri sana. Kwa hivyo, kama hivyo ndivyo na mimi ninaamini hivyo, sote waliotangulia wamezungumza wameunga mkono kwa asilimia mia moja, sisi wananchi wa Jimbo la Makunduchi tunaliunga mkono kwa asilimia mia moja suala hili. Kwa sababu wananchi wa Makunduchi hufurahi sana wenzao wakipata amani.

Mhe. Spika, wewe unajua, bahati nzuri na wewe ni mtu wa Makunduchi, huna majivuno, umetulia, mambo yako yanakwenda vizuri na *inshaallah* yanakwenda vizuri zaidi. Kwa sababu unaamini kwamba mimi nikiwa mpole utapenda na wengine wawe wapole, ukiwa mtulivu utataka na wengine wawe watulivu. Sasa huwezi kuwa machachari tu na ukiwa machachari utataka na wenzako wote wawe machachari ili upate wenzako. Mhe. Spika, hiyo haiwezekani, tunahitaji suala hili tuliunge mkono kwa nguvu zetu zote.

Mhe. Spika, kazi iliyofanywa na Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika maridhiano yale na Katibu Mkuu wa CUF yalifungua ukurasa mpya, *speed* ya maendeleo.

Mhe. Spika, kuna gazeti la Mzalendo hili hapa naomba uniruhusu kama mtu hajaliona basi ataliona, mna picha ya mtu kapiga suti huyu Maalim Haroun Ali Suleiman ndio mimi limesema hivi. “Muafaka wa kisiasa Zanzibar umeleta neema ya elimu”. Mimi nasema si elimu tu, bali ya kila kitu. Kasi ya ujenzi wa madarasa inakwenda vizuri.

Mhe. Spika, juzi wananchi wa Jimbo la Gando pale nawaambia anzeni msingi, wamejitolea pale pale mawe tunayo, chokaa tunayo tutafanya sisi waziri. Madogo hayo. Nini maana yake, nchi iko katika hali ya utulivu. Jamani mimi nasema Mhe. Rais wetu tumpongezeni sana na Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu aendelee kutusaidia kwa mawazo, fikra na busara zake vile vile.

Mhe. Spika, sitaki kuchukua muda kwa sababu Mhe. Haji Omar Kheri amelizungumza kwa makini sana na mimi nayaunga mkono yote aliyozungumza Mhe. Haji pamoja na walionitangulia mimi.

Mhe. Spika, narudia tena kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na tuko tayari kwenda kuifanyia kazi kuelimisha jamii. Ahsante sana.
Mhe. Ali Moh’d Bakari: Mhe. Spika, *Bismillahi Majreha Wa Mursaha Inna Rabbi Laghafuru Rahiym.* Mhe. Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala kwa kutuwezesha kufika muda huu tukawa bado tupo hai. Mhe. Spika, pia nikushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii na mimi

kutoa mawazo yangu kutokana na mswada huu ambao sasa hivi hapa tunaujadili.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Tumbe ambao wamenileta hapa kumshukuru na kumpelekea salamu Rais wa nchi Mhe. Amani Abeid Karume, kwa nia yake safi ya kutaka kuwaleta Wazanzibari pamoja, ili kufanya shughuli zao pamoja wakiwa na wajibu mmoja ndani ya nchi yao. Nimshukuru pia Katibu wetu Mkuu Maalim Seif Shariff Hamad kwa kukubali kwake kukaa na Rais wa nchi kuyazungumzia matatizo ambayo yanatusibu na hatimaye leo kuweza kuyatupilia mbali matatizo na kutuweka pamoja kujadili mustakbali wa nchi.

Mhe. Spika, kwanza mimi nataka nichangie mswada huu kwa ujumla, lakini nataka nielezee umuhimu wa umoja. Mhe. Spika, utakumbuka kwamba katika mikutano ambayo imepita nyuma sisi tuna wahisani wetu wengi hapa Mawaziri. Lakini kutokana na mazingira yaliyojitokeza hata kama tulipenda sana kuinua mkono kuunga ama bajeti zao au miswada yao tulishindwa kufanya hivyo kutokana na misimamo ambayo ilikuwepo. Mhe. Spika, hata kama kilichozungumzwa na wao kilikuwa kina ukweli lakini tulishindwa kufanya hivyo kwa sababu ya hali halisi.

Mhe. Spika, kwa mfano Mhe. Haroun Ali Suleiman anasimamia elimu ndie aliyepewa dhamana na Rais ya kuhakikisha mwenendo mzima wa elimu katika visiwa hivi na kuhakikisha kwamba kila mmoja anapata elimu. Lakini ilifika wakati mimi siwezi kuunga mkono bajeti yake na anachokifanya yeye ni kurahisisha ile kazi ili kusudi watoto wetu ndani ya nchi hii wapate elimu. Lakini likija suala la kwamba sasa haya ungeni mkono ili nifanye kitu fulani ilikuwa hatuwezi kuunga mkono. Sasa kwa kweli hii inaletwa na mifarakano na hii ilikuwa ikiletwa na matatizo ambayo yanaweza kutatuka, lakini tukayapa umuhimu na hatimaye yakatupeleka hapa yalipotupeleka.

Mhe. Spika, lakini likatokea jambo moja, kuna Waziri mmoja hapa anaitwa Mansoor Yussuf Himid. Huyu Waziri ilifika wakati sisi tukamuunga mkono. Mhe. Spika, choyo ni kuona, ninaamini kuna baadhi ya wenzake walipenda na wao tuunge mkono kama ambavyo tulimuunga mkono yeye. Lakini yeye alikuwa akipita hapa anajitanua kwa sababu tunamuunga mkono, sasa wengine kwa kweli hata kama ni wenzake, hata kama wanapiga makofi kwa sababu tumeunga mkono, lakini roho na zenyewe zinaona kwa nini huyu anapendelewa.

Sasa hii ndio athari ya kutokuwepo kwa umoja. Lakini ikafika wakati *Alhamdullilahi* leo sasa tunazungumzia suala la umoja kwa ujumla wake. Kwa hivyo, ninaamini kabisa kwamba hakuna waziri yeyote ambaye hatoinuliwa mkono kwa sababu apatiwe bajeti yao au kitu kingine chochote atakachokileta

Barazani. Kwa hiyo Mhe. Spika, mifarakano si kitu kizuri sana katika ustawi wa jambo lolote ulimwenguni.

Mhe. Spika, madhumuni hasa ya mswada huu kama nilivyokwishatangulia kusema ni kuwaweka Wazanzibari pamoja. Kwa hivyo, ipo haja ya kuyafanya yale yote ambayo katika waraka huu yameelezwa. Si kuyafanya tu, lakini kuhakikisha kwamba yanasimamiwa katika hali ilivyo.

Lakini Mhe. Spika, hapa wasi wasi wangu mimi ni suala zima la kuharakia mambo. Hapa limetajwa suala la kura ya maoni, kujiandikisha, halafu Uchaguzi Mkuu ambao upo mbele yetu.

Mhe. Spika, tukijilazimisha kupanda farasi wawili kwa wakati mmoja basi safari hiyo hatutafika na badala yake tutachanika miguu yote miwili. Sasa mimi fikra yangu ni bora tukawie lakini tufike safari hiyo salama ili kila mmoja aridhike.

Mhe. Spika, matatizo yote yanayotokea katika nchi hii husababishwa na uchaguzi. Lakini wakati mwengine kwa uzoefu ulivyokuwa unajionesha pia ilikuwa inasababishwa na Tume ya Uchaguzi kwa kutokusimamia mambo vizuri. Sasa ndani ya Baraza hili tupo tuliotaka kwamba masuala ya hii kura ya maoni yaamuliwe na Wawakilishi, lakini mawazo ya walio wengi humu katika Baraza ikaonekana kwamba hapana wananchi wenyewe kwa sababu ya ukubwa na unyeti wa jambo hili watoe maamuzi wenyewe wananchi.

Mhe. Spika, sasa hivi ili wapate fursa hii wananchi ambayo ni maazimio ya Baraza hili la Wawakilishi, basi ni vyema sana wananchi wote wa Zanzibar ambao wamefikia umri wa kutoa maamuzi na kutoa maoni yao juu ya jambo hili kubwa washiriki katika jambo hilo.

Leo hii kuna watu wengi mno hawajaandikishwa tena katika kila jimbo. Sasa hivi hata hii awamu ya pili iliyopita katika jimbo langu mimi binafsi kuna watu zaidi ya 1,500 vijana ambao wana umri wa kuandikishwa hawajaandikishwa. Sisi tulichokifanya tuna ushahidi tumeandika mabarua tumeorodhesha majina yao wakiwa na kopi za vyeti vile wanavyosema ni vifupi na vitu vyengine vinavyoonesha umri wao, ili kupeleka huko mbele kuthibitisha kwamba hawa walikuwa wanastahili kuandikishwa lakini hawakuandikishwa. Mhe. Spika, kwa kweli yapo matatizo makubwa.

Sasa unapokataa kwamba wawakilishi wanaochaguliwa na wananchi wasiwaamulie watu, lakini watu wenyewe waamue. Halafu unakwenda kuwachukua nusu watu waamue na wengine wasiamue *ilhali* wana uwezo wa kuamua kwa mujibu wa sheria, itakuwa haikusaidia sana kwamba tuwapelekee

wananchi waamue badala yake wapelekewe watu fulani tu wawaamulie watu wengine jambo ambalo si sahihi.

Kwa hiyo, mimi nafikiri kwa sababu suala hili linawahusu Wazanzibari wote, ni vyema sana watu wote wakapata fursa hii kwa nia ile ile njema wakaweza kutoa mawazo yao juu ya nini kifanyike katika nchi yao.

Sasa Mhe. Spika, nadhani tuangalie umuhimu wa mswada wenyewe na azma yenyewe. Mhe. Rais *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu atamaliza muda wake. Lakini kwa sababu ya shamba ambalo limelimwa limeshapandwa, hivyo ingekuwa vyema sana yeye mwenyewe binafsi kulishughulikia, ili kuhakikisha kwamba hawa watakaokuja kama walivyosema wenzangu, basi watakuta shamba ambalo ni zuri na hawatarudia katika shamba ambalo litakuwa limelimwa halafu likaachwa na magugu matokeo yake kilicholimwa hakitaonekana.

Mhe. Spika, nashauri kwamba lazima tujifunze na yale ambayo yamepita nyuma. Kila mmoja ana wajibu na kila mmoja ana haki ya kutoa maamuzi katika nchi hii. Tukishakubali kwamba sisi sote ni ndugu basi hizi athari nyengine zote zitaondoka.

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Haji Faki Shaali kwamba "Si kila penye wema hakuna wabaya". Hapa ni duniani kwa hiyo kuna watu wanafurahishwa na mema sana kutokana na uzuri wa wema huo. Lakini vile vile kuna watu wanafurahishwa na maovu kwa sababu wao ndimo wanamopatia riziki zao.

Sasa katika hali hii, tunaamini walio wengi katika nchi yoyote au popote pale watakuwa wakifurahishwa na mema kwa sababu ya uzuri wa wema ule. Kwa hiyo na sisi kwa sababu tunafurahishwa na mema, ni vyema sana jamii zetu hizi tusiziruhusu pamoja na sisi wenyewe kutumia midomo yetu, kutumia ndimi zetu tukawapotosha watu halafu ikawa ni chanzo cha matatizo. Kila panapojitokeza dalili ya jambo lolote baya ni vyema kuwaelimisha watu vizuri juu ya azma hii na jinsi ya hali ambayo tumetoka nyuma.

Leo tumefika pahala Mhe. Spika, kila mtu anataka uchaguzi usifanyike. Kwa sababu uchaguzi ukishafanyika ile siku ya mwisho hakuna mtu mwenye raha, mwengine akamatwe apigwe, mwengine adhalilishwe na mengineyo.

Sasa kuna sababu gani ya mambo hayo, haya yameletwa na utashi. Lakini leo *Alhamdulillahi* tunazungumzia umoja ninaamini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na kwa sababu ya nia zetu safi haya hayatatokea tena. Kwa kuwa hayatatokea hatutaki tuyazungumzie tena, tunataka tuzungumzie umoja wetu. Kwa hiyo Mhe. Spika, umoja ni jambo zuri sana.

Mhe. Spika, leo hata Mhe. Waziri Kiongozi hapa na Mhe. Haji Omar Kheri wamevaa ki-CUF CUF hivi. Wamevaa tai nzuri na nguo nzuri zile. Kwa hivyo, huku ni kuonesha umoja wetu na ni kuonesha namna gani ambavyo sasa hivi tumekaa katika mustakabali mzuri na mustakabali mwema.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi ninachokisema ni kwamba sisi ni viongozi na kama ni viongozi basi tunawajibu mkubwa wa kusimamia majukumu yetu ambayo yametuleta hapa.

Mhe. Spika, kwa kweli mara nyingi sisi viongozi ndio tunaosababisha matatizo na kwa kuwa ndio tunaosababisha matatizo leo tumeona, watu baada ya viongozi kukaa pamoja tu basi wananchi wetu wote wamejichunga, kila mmoja anajua wajibu wake na analizungumzia suala hili la umoja wetu, hataki turudie kule tena ambako tumetoka.

Mimi bado nasisitiza viongozi wenzangu kwamba tuna wajibu na jukumu kubwa la kuwaelimisha wananchi wetu ili kuwaweka katika upande mzuri ili masuala haya yasitokee tena.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi naunga mkono hoja hii kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe.

Vile vile naendelea kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais pamoja na katibu mkuu wetu kwa jitihada hii wanayoionesha na Mwenyezi Mungu namuomba awajaalie umri na maisha marefu, awape na afya njema ili mambo haya wayasimamie vizuri zaidi wakishirikiana na viongozi wenzao wa serikali ambao wamewateua wao ili wawasaidie shughuliz zao.

Mhe. Spika, vile vile mimi naomba kama alivyosema Mhe. Sheikh Said Ali Mbarouk kwamba hii ni nafasi nzuri zaidi kwa wale ambao wanataka kurithi nafasi yake ya kuukamata mwenendo wake ili kusudi kuhakikisha kwamba wanawaweka watu katika mwenendo mzuri bila jazba. Kwa sababu ukipita katika baadhi ya maeneo watu wanasema maneno mengi tu ya ovyo ya kukejeli mambo haya.

Kwa hivyo, sio kila mtu ana nia safi juu ya jambo hili, watu wengine wana nia safi na wengine hawana nia safi. Lakini la muhimu ni kumuomba Mwenyezi Mungu akatujaalia tukawa wengi, tukafanya kazi hii kwa pamoja na tukaondoka hapa katika ulimwengu huu tukiwa katika hali nzuri. Vile vile tukiwa tumewacha miongozo mizuri ambayo watoto wetu au vijana wetu

watarithi mwenendo huu kutoka katika ile hali ambayo tumekuwa tukiishi nayo.

Mhe. Spika, kwa sababau Mswada huu kila mmoja atapata fursa ya kuuchangia kidogo tu, basi naomba niishie hapo, lakini tuone umuhimu wa umoja kwamba ndio wajibu wetu. Tukiiwacha nchi hii ikimwagika damu kwa sababu ya kutumia midogo yetu vibaya, basi bado tutakuwa tuna jukumu. Ni wajibu wetu kusimamia umoja wetu na kila mmoja aone kwamba ana haki sawa sawa na mwenziwe.

Mhe. Spika, hapa hakuna mbora katika visiwa hivi, hakuna mtu anayetoka Pemba kuwa ni mbora zaidi au aliyekuwa hapa Unguja kuwa ni mbora zaidi kuliko mwengine. Watu wote tuna wajibu mmoja kwa sababu nchi hii yote iende pamoja. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ya kutoa mchango wangu katika hoja hii muhimu sana ilioko mbele yetu. Mhe. Spika, maneno waliyosema wenzangu na hasa mwenyekiti wangu wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala pamoja na Mnadhimu wangu, kwa kweli yangetosha kunifanya mimi nisiseme jengine. Hasa kwa sababu hali yangu leo sio nzuri sana, nilitaka nikae nipumzike nisikilize tu.

Lakini kilichonifanya nisimame Mhe. Spika, ni kwamba wananchi wa Jimbo la Chonga naogopa sana wasije wakanisuta kwamba jambo zuri kama hili hawakusikia sauti yangu angalau ikiunga mkono. Kama unavyojua Mhe. Spika, siku hizi tuna mchakato kule. *(Makofi/Vicheko).*

Kwa hivyo, Mhe. Spika, maelezo ya wenzangu hawa waliotangulia kusema ni mazuri sana na mimi nayaunga mkono mia juu ya mia. Ni kweli Mhe. Spika ni kipindi kirefu sasa nchi yetu haiendi vizuri, tunaathirika kwa kila hali, tunaathirika kiuchumi, tunaathirika kisiasa, lakini tunaathirika hata kiafya kutokana na migongano hii ambayo tumekuwa tukiishi nayo karibu mwaka wa 15 huu sasa. Kila mtu katika sisi ana makovu ya migongano hii tuliyokuwanayo. Ni kiasi mtu afike pahala aseme sasa basi haya yametosha.

Mhe. Spika, nataka nimuunge mkono sana Mhe. Mnadhimu wangu pale alipomsifu Mhe. Karume kwa kusema kwamba kwa kweli anawatakia wenzake watakaomrithi mustakabali mwema, amepania hasa kuwaachia nchi ikiwa katika hali njema. Kwa sababu yeye kalala katika kitanda hiki na kwa hivyo anakijua kunguni wake, akaona si vyema niwaachie wenzangu walale katika kitanda hiki. Kwa hivyo, anawatayarishia mazingira mzuri.

Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kusema kwamba hoja hii walipaswa sana wale waliokuwa na nia ya kumrithi Mhe. Karume waiunge mkono kwa nguvu zao zote.

Mhe. Spika, huu ni mchakato wa kuwanasua Wazanzibari kutoka katika migongano ya kisiasa ambayo imetuathiri kwa muda mrefu. Kwa hivyo, hili ni jambo jema na nafikiri kuwa sisi viongozi ambao kufika kwetu hapa ni kutumia migongo ya wenzetu wananchi, kwa kweli hatutokuwa tunawatendea vyema wananchi, kama tutakuja hapa jambo zuri kama hili ambalo lina maslahi na wananchi waliotufikisha hapa, halafu tuwe hatuko radhi nalo au tutafute lugha ya kupinga.

Nadhani ni jambo la kuliunga mkono kwa nguvu zetu zote, ni jambo la kuliombea dua na kwa kuwa ni dua njema Inshaallah Mwenyezi Mungu ataipokea kwa mikono miwili ili tufike pahali mambo haya tena yawe ni historia tu katika nchi yetu. Maana yake tuje tuwahadithie wajukuu zetu kama kulitokea hivi na hivi, maana yake watushangae kweli kweli. Lakini sio mambo ambayo tunatarajia tuyaone yakitokea tena.

Mhe. Spika, mswada huu unatokana na azimio la Baraza la kikao cha Januari kilichopita. Madhumuni yake makubwa ni kuandaa sheria hii ya kura ya maoni. Moja katika kichocheo kimoja ni lile azimio kubwa la viongozi wetu wawili la kutaka serikali ya umoja wa kitaifa.

Mhe. Spika, mchakato huu pia umeleta heri nyengine kubwa sana, ya kuwa sasa kutakuwa na sheria ya kura ya maoni, jambo ambalo tulikuwa hatunalo katika nchi yetu, ni sheria ambayo itatusaidia sana. Hutokea haja ya kuamua mambo mengi, lakini tulikuwa tunashindwa kufanya kwa sababu tulikuwa hatuna hii sheria. Kwa hivyo, mimi naipongeza serikali sana hasa kupitia afisi ya Mwanasheria Mkuu, kwa kuandaa sheria hii ambayo itakuwa ni suluhisho la matatizo yetu mengi yatakayotokea. Yawe ya kisiasa, yawe ya kiuchumi, yawe mambo mengine yatakayotokea lakini ilimradi tutakuwa tuna chombo muhimu sana cha kukitumia.

Mhe. Spika, nilikuwa naonesha wasi wasi wangu kidogo kuhusiana na muda huu tuliobakia nao na mambo yaliyotukabili mbele. Mhe. Spika, Baraza lako linatarajiwa kuvunjwa baada ya kikao cha bajeti. Hapa tulipo takriban tupo mwezi wa April sasa. Sheria hii ina mambo mengi yakufanya. Kwa mfano, leo tukishaipitisha hapa *Inshaallah* kuna kipindi ambacho atapelekewa Mhe. Rais aitie saini, najua kwa kuwa ana nia njema hatochelewa hata kidogo. Lakini ikishatiwa saini sasa ni jukumu la Tume ya Uchaguzi kuuanza mchakato wa kuitisha kura ya maoni na mchakato huo bila shaka utaanzia na taaluma, sina hakika lakini inaweza kuchukua karibu mwezi mzima kama si kidogo.

Tukimaliza hapo tutapiga kura ya maoni, tukishakupiga kura ya maoni kuna matokeo yanaweza kujitokeza.

Mhe. Spika, inaweza kutokea siku moja kura zikafungana, mimi siombi hivyo. Kwa kuwa watu wote wana mwamko wa kutosha basi watasema ndio wengi, lakini ikitokea kesi hiyo sheria hii imesema kuna mwezi mmoja kwa tume ya uchaguzi kuitisha kura nyengine. Kwa hivyo siku zinakwenda, ukimaliza mwezi mmoja wa kupiga hiyo kura kama zitakuwa zinafungana. Kwa sababu tunajaribu kuangalia zile *possibility* ambazo zinaweza kutokea. Kama tumepiga kura mwenzetu mmoja akasema hapana, mimi siridhiki nakwenda mahakamani ana mwezi mwengine.

Sasa wasi wasi wangu mimi tutakuwa tumefunga Baraza wakati huo, sijui wanasheria watatuelekeza vipi. Mimi nilisema niliseme hili kama angalizo kwamba katika haya mambo tunahitaji kwanza kuwa na nia safi na bila shaka ipo, tunahitaji kuharakisha kidogo, tunahitaji kuepukana na mambo ya kutudhorotesha hapa katikati ili twende kama tulivyokusudia.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, nilisema mimi kwa sababu ya wenzangu waliokwisha kuyasema, sikuwa na haja hata ya kusimama, lakini nilitaka nisimame ili wananchi wangu wa Chonga wasikie kama nimesimama na sasa natamka rasmi, kwamba ikiwa Mhe. Spika, utaniruhusu nataka niunge mkono sio kwa asilimia mia moja, lakini ni kwa asilimia mia moja na hamsini juu ya mia moja, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Kwa kuunga mkono haina wasi wasi, lakini kwa kupiga kura ingekuwa ni hii moja tu. Tunaendelea.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa nafasi kuwa mmoja wa wachangiaji wa mswada huu wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kura ya Maoni na Mambo mengine yanayohusiana na hayo. Aidha, nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, uzima na afya na kuweza kuamka leo Jumatatu ya tarehe 29 mwezi Machi, mwaka 2010 na kuja Baraza la Wawakilishi.

Pia naomba uniruhusu nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na watendaji wake wa Afisi ya Waziri Kiongozi, watendaji wa afisi ya AG na watendaji wa tume ya uchaguzi na wengineo, ambao kwa namna moja au nyengine wameandaa mswada huu na kuuleta katika hali nzuri. Mhe. Spika, wengine mwisho ndio huunga mkono, lakini mimi naanza mwanzo naunga mkono mswada huu. Mhe. Spika, ni ukweli uliowazi kwamba hatukuwa na sheria huko nyuma ambayo inatuelekeza

kwamba ikifika jambo kubwa na muhimu, basi kuwe na tume au kuwa na kura za maoni. Taratibu hizi katika nchi za wenzetu wanafanya na kwa sababu kila jambo na wakati wake.

Mhe. Spika, miaka ya mwanzo hata Baraza la Wawakilishi halikuwepo, lakini viongozi wetu waliopita kwa busara zao wakaona kwamba muda umefika wa kuwa na Baraza la Wawakilishi. Inawezekana lilivyoanzishwa Baraza la Wawakilishi wengine walikuwa na hofu, lakini leo nafikiri tumeona faida na umuhimu wa Baraza la Wawakilishi katika maendeleo ya nchi yetu.

Kwa hivyo, na jambo hili ambalo ni geni lazima kutakuwa na watu wana hofu, lakini sisi wawakilishi wa wananchi ni lazima tuwatowe hofu kwamba jambo hili litasaidia sana nchi yetu ya Zanzibar kusonga mbele katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, hata humu ndani kuna baadhi ya waheshimiwa tunawasikia wanasema tutakwendaje. Mimi nafikiri tukiwa kama ni Waheshimiwa Wawakilishi, tufanye kazi yetu ya kupitisha mswada huu ili Mhe. Rais kwa mamlaka ambayo amepewa na katiba, afanye na yeye wajibu wake kwa mswada huu ili kuwa sheria. Sasa yale mambo ya utekelezaji tusimfikirie Rais au muda ukoje, tumwachie yeye kutokana na mamlaka aliyopewa basi atekeleze majukumu yake kwa jambo hili ambalo liko mbele ya mikono yetu.

Pia nimefurahi kwamba jambo hili lina mnyororo mrefu kidogo, linatokana na mambo ya mazungumzo. Mazungumzo hapa Zanzibar tukisema ya pande mbili au vyama viwili ni CCM ambacho ni chama tawala na kitaendelea kutawala na chama cha upinzani cha CUF, nafikiri pia wataendelea kuwa ndio wapinzani hata miaka ijayo kwamba wao ndio wasaidizi wetu.

Sasa jambo hili limezungumzwa, limejadiliwa mpaka limefikia hapa kwamba sasa tufikie hali hii. Katika mazungumzo yote likaletwa hapa azimio, tukalifanya azimio kwamba jambo hili ni zuri lakini liende kwa wananchi. Kwa mujibu wa katiba Mhe. Haji Faki Shaali alinukuu kifungu cha 9, na mimi naomba nisikinukuu chote, lakini naomba nikiseme tu kwamba kifungu cha 9 cha katiba ya Zanzibar 9(2) ambacho ndio ninataka kukizungumza kinazungumzia nafasi ya wananchi kupewa fursa katika mambo ya maendeleo ya nchi yao.

Mhe. Spika, kwa sababu sisi tuko hapa katika moja ya kazi zetu ni kutoa chachu ya maendeleo ya nchi yetu na kwa sababu katiba hii imetungwa na Baraza hili la Wawakilishi na imetoa fursa kwa wananchi kupewa fursa ya kushiriki katika mambo makubwa, basi mimi naunga mkono kwamba tupitishe

sheria hii, halafu ipelekwe kwa wananchi na wao wakatowe maoni yao kuhusu jambo hili ambalo lina manufaa kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, kazi imefanyika vizuri. Mhe. Hamza Hassan pale na watu wake wamefanya vizuri na imeelezwa humu kwamba watu ambao watapiga kura hii ya maoni ni Wazanzibari ambao wamejiandikisha kwenye daftari la kudumu. Nafikiri hili halina hofu wala mashaka, kwa sababu wanapatikana vipi tutajua kwamba ili uwe mpiga kura uwemo katika daftari la kudumu ni lazima uwe ni Mzanzibari mkaazi. Maana unaweza kuwa ni Mzanzibari, lakini pengine hukai kwa muda mrefu. Mimi nina hakika kwamba kuna watu wako Marekani, lakini mpaka leo ni Wazanzibari lakini hawana sifa ya kuwa katika daftari hili, kwa sababu muda ambao wamekaa nje ya nchi ni mkubwa na kutokana na sheria zetu hawaruhusiki.

Mhe. Spika, kuna wengine wako Marekani, lakini pengine kaondoka juzi na ana kitambulisho chake cha Mzanzibari, kwa hivyo akitaka arudi ajiandikishe, apige kura za maoni. Akitaka ataendelea kubakia au akitaka anaweza akaondoka. Kwa hivyo, nahisi na hili lisitutie hofu Waheshimiwa Wajumbe. Nashukuru kwamba pengine katika huu umri mpya au awamu mpya ya kura tulizopiga na uandikishaji wa daftari, hakuna kipindi ambacho daftari limekwenda vizuri kwa miaka hii kama mwaka huu, yaani kwa utulivu wake katika vituo. Natarajia sote tutavumiliana ili daftari liende vizuri kwa wale wenye haki wapate ili uchaguzi wetu uende vizuri. Jambo hili nalo ni zuri na linastahiki kupewa kipaumbele.

Mhe. Spika, mimi naomba kwa sababu jambo ni jipya na ingawa watu ni wale wale, lakini wanatakiwa wapewa elimu ya kutosha, na kwa sababu sheria imesema humu kwamba tume ya uchaguzi itakuwa na wajibu wa kutoa elimu ya uraia kwa wananchi wetu wa Zanzibar ili waelewe hicho kitu chenyewe ni nini na wanatakiwa wafanye nini. Sasa mimi niwaombe watakaopewa dhamana hii kuifanya kwa uadilifu na kwa umakini.

Pia niwaombe wananchi wenzangu, maana sisi waheshimiwa humu pia ni wananchi ambapo mmoja mmoja naye atapewa fursa ya kupiga kura yake. Basi niwaombe na wananchi wa Zanzibar ile timu ya wataalamu watakapokwenda kutoa hiyo elimu ya uraia, basi wananchi wale wajitokeze kwa wingi wawasikilize na wapate fursa ya kuwauza na kuwahoji yale mambo ambayo bado wanayatilia mashaka. Nafikiri tukishaelewa sote tunaweza kwenda vizuri. Lakini kuna umuhimu wa hii tume kutoa elimu vizuri zaidi ili wananchi waweze kuelewa nini ambacho kimekusudiwa. Vile vile kuwe na upembuzi ambao utatuwezesha kufikia malengo kwa kuwatambua watu wanaohusika. Kwa sababu tusitumie hizi kura tukavunja sheria nyengine, tutumie kura kwa wale ambao wanastahiki kupiga kura. Naona kwa pande zote mbili

tumekubaliana. Watu wamezungumza vitambulisho, lakini hakuna aliyesema kwamba kanyimwa mtu bila kosa, lazima kutakuwa na kasoro moja au mbili ambazo kama zipo basi zitarekebishwa ili watu wote wapate fursa ya kutumia nafasi yao.

Mhe. Spika, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukija humu kwenye Baraza, nina hakika kwamba Chama chetu cha Mapinduzi tunapewa fursa mtu kuchangia mawazo yako, kwa unavyoona wewe bila kushinikizwa na bila kuwekewa vigingi. Lakini kwa wawakilishi nina hakika wote wa pande zote mbili wanaelewa kwamba kuna mambo ya msingi kwa mwakilishi.

Moja ni kuhakikisha kwamba anaitetea nchi yake, unaitetea nchi yako kwa kuwatendea wananchi mambo mema, kuyatekeleza majukumu yako kwa uadilifu, kutenda mambo ambayo yanaleta upendo, mshikamano na kujenga uchumi wa nchi yako. Hiyo ni kazi ya mwakilishi.

Pili, kuhakikisha kwamba unalinda chama chako, maana yake tunatetea nchi kwa pamoja, halafu kila mmoja ana misingi ya chama chake. Sasa mwakilishi pia una haki. Nimemsikia Mhe. Ali Moh'd Bakar, mengine mimi nilikuwa siyajui kwamba kumbe hata ukiwa na bajeti nzuri, basi walikuwa na maagizo kwamba ipinge tu. Sasa wakati mwengine tulikuwa tunahangaika, unajitahidi Mhe. Waziri ufanyakazi vizuri lakini kumbe kule ilikuwa kuna maagizo maalu. Kwa hivyo, sasa wanasema wameshafungua milango, kwa hivyo hii ni nafasi ya serikali kwa upande wake kuonesha uwezo wake, lakini na nafasi kwa wapinzani nao kuonesha upinzani wao kwa kuisaidia serikali kutekeleza wajibu wake.

Kwa hivyo, haya yana misimamo pia wakati mwingine ya kichama, ndio lile jambo la pili la kichama. Lakini jambo la kichama haliwezi likavuruga jambo la nchi. Nina hakika vyama vyote vya siasa lengo lake sio kuvuruga, isipokuwa ni kusaidia maendeleo ya wananchi kwa haraka zaidi. Yaani kama benki zamani ilikuwa ni lazima uende kwenye kidirisha uandike ndio upewe fedha, sasa hivi unaambiwa uende kwenye ATM tu unaweza kupata fedha. Kwa hivyo, hivi vyama vya siasa vinakuwa ndio vinatupeleka haraka zaidi katika maendeleo. Kwa hivyo, hilo nalo ndio jukumu lako la pili.

Lakini jukumu la tatu la mwakilishi pia liko kwenye jimbo lake, kwa kuwasaidia wananchi,kwanza kuwapelekea maendeleo, kuwaelimisha mambo mema na yenye manufaa yao na kushirikiana nao katika kubadilishana nao mawazo kwa maslahi ya nchi yao. Kwa hivyo na hili pia Waheshimiwa Wawakilishi tuna nafasi ya kuzungumza na wananchi wetu ili kuwasikiliza maoni yao na wewe kupeleka ushauri wako kwa wao, hizi pia ni kazi za Mhe. Mwakilishi.

La nne nafikiri ni lile la maslahi yako binafsi. Kwamba fanya yote, tetea nchi ni wajibu wako, tetea chama ni wajibu wako, tetea jimbo ni wajibu wako, lakini mwishowe ni lazima ujitetee mwenyewe na familia yako. Lakini ukiyabadilisha ukianza kutetea la familia ndio mwanzo au lako wewe, halafu ndio yakafuatia hayo mengine na halafu ya nchi mwisho tunaweza tusifike pahala tukatambuana, lengo ni tutambuane.

Mhe. Spika, nafikiri haikuja tu hii hoja ya walioanzisha Baraza la Wawakilishi, hawakufanya tu kwamba iwe sehemu ya kuja watu hapa kukaa vipindi vitano, kupeana maposho na mishahara iwe basi ni lazima kulikuwa na malengo maalum. Bahati nzuri wamefanya kazi vizuri. Nafikiri Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban alikuwepo toka mwanzo, walifanya kazi nzuri, walitunga katiba, walitusaidia kuweka miongozo.

Sisi wengine tumeingia Baraza la Wawakilishi humu kila kitu kigeni, lakini wenzetu tuliowakuta ndani ya Baraza wakatufundisha kwamba hapo usinyanyuke, Spika akisema kule usikatishe mbele yake, yaani taratibu za Baraza na miongozo yake tukazipata humu ndani. Kwa hivyo, tukaelewa na sisi tumewapokea wenzetu na wao wameshaelewa na watakuja wengine na wao ambao watatukuta ndani au hawatukuti, lakini na wao wataelewa na wataheshimu taratibu za uendeshaji wa Baraza.

Kwa hivyo, na sisi ni lazima tuweke msingi wa kuonekana kwamba na sisi tulikuwepo hapa na tulifanya kazi vizuri kwa maslahi ya nchi yetu. Jambo jema au msingi mzuri ni kutuunganisha sisi na wananchi wa Zanzibar, tukiwatenga siku moja watatuuliza kwamba nyinyi kwenye katiba mlisema mtatushirikisha katika mambo mazito ya maendeleo ya nchi yetu, lakini hayo mengine mbona hamkutushirikisha. Kwa hivyo, mimi nafikiri kwamba sisi hatuna kosa kuwashirikisha wananchi na ni jambo jema sana kuwashirikisha wananchi, ili na wao waseme nini tufanye kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, bahati nzuri sheria inasema kwamba uamuzi wa wananchi utaheshimiwa, nafikiri hatokezei binadamu duniani, si taifa, si mtu ambaye atatulaumu kwa uamuzi wa wananchi kwamba uwamuzi umekuwa huu lakini kwa nini nyinyi msifanye hivi, itakuwa tutawashangaa wao, kwa sababu hata wao duniani huko wanafanya kura za maoni, tena kwa mambo mengine madogo kuliko yetu, lakini maamuzi yao yanaheshimiwa.

Mhe. Spika, kuna nchi Ulaya mpaka leo hazitumii sarafu ya *euro*, hazijajiingiza katika Jumuiya ya Ulaka, lakini hawana uhasama kwa sababu ni maamuzi ya wananchi wao. Kwa hivyo na sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili, mimi nawaomba mswada huu ulikuwa ni wetu na ni chanzo chetu, sawa sawa

ni kiatu chetu. Kwa hivyo, leo kimeletwa tukivaeni. Tuvae kiatu soksi tunazo tayari tuendelee mbele tusikwame katika safari yetu.

Mhe. Spika, naomba nimalizie hapo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono mswada huu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana kwa michango hii iliyoendelea, ipo orodha ndefu kidogo. Haidhuru michango inajirudia rudia, naistahamilia kwa sababu ya umuhimu wa hili jambo na kuona kwamba tunalipitisha ikiwa limepata baraka za wajumbe wengi zaidi.

Kwa hivyo, wapo wajumbe wapatao 11 au zaidi na hawajanitosha, kwa sababu tulipanga siku mbili kwa ajili ya mswada huu. Tulifanya hivyo kwa sababu mswada huu una umuhimu wake kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu. Kwa hivyo, ndio tukaona kwamba tuupe nafasi ya kutosha na wajumbe wameitikia, naamini kuna wajumbe zaidi wataitikia ili kukamilisha shughuli hii.

Yanaweza yakatoka mawazo mengine yakasaidia kujipanga vizuri zaidi katika kuufanya uwe bora mswada huu na hatimaye matayarisho mengine huko mbele ya kile ambacho kitapitishwa hapa. Baada ya hayo naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo, ambapo tukiingia tutaanza na Mhe. Sultan Moh'd Mukheir, Mhe. Juma Duni Haji, Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame na wengine wengi tufike mapema kama kawaida. Nawashukuruni.

(Saa 7:00 kamili mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwanza napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu na mimi nizungumze machache kuhusiana na Mswada huu wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kura ya Maoni na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na wala sina tatizo lolote *(Makofi)*.

Pili naomba na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mhe. Haji Omar Kheir Mnadhim wa Chama cha Mapinduzi katika Baraza la Wawakilishi ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa hotuba yake aliyoitoa nzuri sana asubuhi hii ya leo. Kwa kweli Mhe. Mjumbe ameonesha wazi kwamba yeye ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha

Mapinduzi, kwa namna alivyouzungumzia mswada huu, kwa hiyo namuunga mkono *(Makofi)*.

Vile vile napenda kuchukua fursa hii kumuunga mkono Mnadhim wangu wa Chama cha Mapinduzi katika kuadhmisha Siku ya Maulid Tumbatu, nilisema gazeti la Zanzibar Leo na kuona picha za watu aliowaalika. Kwa kweli anadumisha utamaduni wa Tumbatu na Zanzibar kwa jumla, jinsi namna alivyoyaandaa maulid yao, tena maulid mazuri sana. *(Makofi)*.

Mhe. Spika, sasa naomba nikupongeze wewe kwa Baraza lako tukufu, kwa kweli nuru imeanza kuonekana katika Baraza lako hili. Baada ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Amani Abeid Karume kuonana na Katibu Mkuu wa Chama cha CUF na kuzungumza mustakbali wa Zanzibar, imeonekana tokea siku hiyo na kutambuliwa kwa Mhe. Rais basi kumeleta nuru katika Baraza lako tukufu.

Kwanza Waheshimiwa Wajumbe wanaunga mkono Hoja za Serikali bila ya matatizo yoyote. Pili Waheshimiwa Wajumbe wanauliza maswali wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu bila ya matatizo yoyote, japo kwamba wameanza wawili kama vile Mhe. Abass Juma Muhunzi na Mhe. Hija Hassan Hija inshaallah na wengine wataleta maswali kwa ajili ya kuulizwa *(Makofi)*.

Tatu hivi sasa Waheshimiwa Wajumbe wanasimama wakati Mhe. Waziri Kiongozi anapoingia Barazani na kidogo mambo yanakuwa mazuri. Vile vile Mhe. Rashid Seif Suleiman (Waziri Kivuli wa Wizara ya Afya), asubuhi amenilaumu kidogo na kuniambia kwamba Mhe. Waziri wakati unapofanyakazi zako za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii mimi hunialiki kwa nini na mimi ndiye Waziri Kivuli.

Kwa hivyo, namuahidi Mhe. Waziri Kivuli wakati ninapofanya shughuli zangu za Wizara ya Afya. Mhe. Spika, hivi karibuni nitakuwa na shughuli kubwa sana, ambapo nitaletewa gari kubwa na China kwa ajili ya kutoa damu, yaani wanaita *Blood Bank Mobile Vehicle*.

Kwa mfano, litakuja Mwanakwerekwe litakaa tena linavyo vyombo vya kisasa na wananchi wataitwa kwa ajili ya kutoa damu na damu itaingia, tena wataalamu wawili wa kushughulikia gari hiyo kutoka China wataletwa. Kwa hiyo, ni gari ya aina ya pekee kutoka China itakuja na hiyo namuahidi Mhe. Waziri Kivuli nitamualika. Vile vile nitamualika kwenye shughuli yangu nyengine ya ujenzi wa *Out Patient Department* na jiko katika Hospitali ya Wagonjwa wa Akili, hiyo ni ya aina pekee, tena mjenzi yumo humu ndani ya Baraza la Wawakilishi, ambaye ni Mhe. Nassor Ahmed Mazrui *(Makofi)*.

Mhe. Spika, pia nitamualika kwenye nyumba 40, ambazo 20 Unguja na 20 Pemba kwa ajili ya kulala madaktari. Kwa kweli Mhe. Nassor Ahmed Mazrui Mwakilishi wa CUF ndiye aliyejenga nyumba hizo 20 za Pemba.

Sasa yote hayo ni mafahamiano mazuri baina yetu Chama Tawala na Chama cha Upinzani. Kwa sababu sisi hatubaguani Mhe. Spika wakati tunapotoa tenda na kuomba na kufikia kile kiwango cha kupata, basi sisi hatutizami kama ni CUF au ni CCM, isipokuwa tunampa anayestahiki. Kwa kweli hata *ADB* na wao wanachagua hivyo hivyo anayestahiki ndiye mwenye kupewa.

Mhe. Spika, mambo yote haya ni nuru kwenye Baraza lako tukufu hili *(Makofi)*.

Baada ya maelezo hayo sasa niingie moja kwa moja kwenye mswada. Mswada huu utazidi kutuletea amani na utulivu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, juzi nilikuwa na sherehe katika Chuo cha Afya Mbweni na walihudhuria Wajumbe wako tena ni watu wakubwa sana wakiwemo Mhe. Waziri Kiongozi, Mhe. Naibu Waziri Kiongozi, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib, Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii), Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora, Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Chama cha Upinzani.

Katika hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alizungumza kitu kimoja, Mhe. Spika naomba kwa ruhusa yako nikizungumze. Aliwaambia hao wanaotaka urais, kwamba urais si kupanda gari, bendera na ving'ora, isipokuwa urais utatakiwa ulete maendeleo katika nchi.

Mhe. Spika, rafiki yangu Rashid Joe kila siku anataka urais, kwa hiyo namwambia kuwa urais sio kupanda gari, bendera na ving'ora. Lakini urais ni kuleta maendeleo katika nchi na wala maendeleo hayaji bila ya amani na utulivu, sasa ukikabidhiwa nchi ambayo haina amani wala utulivu hutoleta maendeleo *(Kicheko/Makofi)*.

Mazungumzo haya yalikuja vipi ingawa hakunituma lakini kwa ruhusa yako Mhe. Spika naomba nizungumze haya. Mhe. Rais alikwenda Ujarumani, baada ya kwenda Ujarumani akaona mashine. ya *CT Scan* na alimuuliza *Professor* kwenye hospitali, hivi hii mashine ya *CT Scan* katika *population* ya *one million* inaweza kuweka mashine hii, aliambiwa ndio katika *population* ya *one million* inapaswa iwepo na wakati huo yeye si rais na wala hana nia ya urais.

Kwa hivyo, aliporudi hapa aliwaambia wenzake kwamba jamani na pale Unguja katika Hospitali ya Mnazimmoja tuweke mashine ya *CT Scan*. Lakini kumbe malaika mwema anapita na kuchukua akamwambia ngojea nikupe wewe urais na halafu uweke hii mashine ya *CT Scan*, amejaaliwa kupata urais na ametimiza ahadi, yaani ametuekea mashine ya *CT Scan (Makofi)*.

Mhe. Spika, leo amini kwamba wamekuja madaktari wa Hispania wameleta kabati zima la vifaa vipo pale, tena hao madaktari ni *Neuro Surgeon*, yaani wanazifanya *operation* hapa Zanzibar ambazo sisi hatuwezi kuzifanya hata siku moja, kwa sababu ya mashine ya *CT Scan*. Kesho kutwa madaktari wanne wanakwenda Spain kwa ajili ya kusomeshwa zaidi mambo haya na wataongozwa na Dk. Jamala.

Isitoshe wamekuja madaktari kutoka Uholanzi, Ubelgiji, Uingereza na wanafanya mambo ya *plastic surgery*, matatizo ya watoto wadogo wenye kukojoa tundu mbili na mengi mengineyo ambayo hatuyafanyi hata siku moja, lakini kwa sababu tunavyo vifaa vya kisasa. Sasa haya ndio maendeleo katika nchi.

Mhe. Spika, mambo haya hayaji bila ya mswada huu, kwa sababu nchi iwe na amani, itulie Waheshimiwa Wajumbe wa Chama cha Upinzani wanapokuja wacheke, yaani wawe na tabasam, lakini leo watu wamenuna na mtu anapoambiwa aombe radhi anasema haombi ndio hivyo hivyo na kwa kweli haipendezi.

Lakini yote yatatatuka kwa mswada huu tunaoupitisha na mimi Mhe. Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja *(Makofi)*.

Sasa tunayo maendeleo ya kujivunia Zanzibar Mhe. Spika, isipokuwa tunataka tuyaendeleze. Maendeleo haya tutayaendeleza vipi, tutayaendeleza katika utulivu wa nchi yetu pamoja na mafahamiano baina ya sote, yaani wananchi wote tuwe kitu kimoja na tuangalie nchi yetu namna gani ya kuweza kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Leo katika Hospitali ya Mnazimmoja tunayo Idara ya Macho, ambayo inavyo vifaa vyote vya kutibia binadam kwa ajili ya kufanyia *operation* wa macho pamoja na madaktari kutoka China, pia juzi nimepokea vifaa vyengine vya macho.

Vile vile tunayo *Theater* ya *Ear, Nose and Through*. *Theater* ile tunavyo vifaa vya kisasa tena daktari Dk. Naufal Kassim ni daktari bingwa ambaye ni Mzanzibar na Mchina yupo pale anamsaidia *(Makofi)*.

Ukiwa kwenye *theater* iwe ilivyojengwa unaona bahari basi unasahau kama unafanyiwa *operation*, wazungu wanakuja kwenye *theater* ile basi wanaona raha, kwa sababu nchi imetulia na inataka iendelezwe na utulivu huu. Kwa hivyo, nawakaribisha nyote muje muiangalie *Theater* ya *ENT* kama mtataka kutoka nje kwa jinsi ile raha iliomo mule.*(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, *laboratory* ilioko Hospitali ya Mnazimmoja utafikiri uko New York or Washington hivi sasa na wala sio ile *laboratory* ya zamani yaani *microscope*, lakini hivi sasa tunao wafanyakazi wenye *PhD* pale. Kwa hivyo, njoo muangalie Mnazimmoja Hospitali *Laboratory*. Kamati ya Ustawi wa Jamii wanapokuja pale unajua asubuhi hasa wamekuja kuangalia maendeleo hasa *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, leo asubuhi imeulizwa swali kufika tu naambiwa Dk. Salum Ismail amesharudi kutoka Nairob University Daktari Bingwa wa *CT Scan*, *X-ray* na *Ultra Sound*, amesomeshwa na fedha za SMZ na mwenyewe Mhe. Rais ndiye aliyetoa amri tusomeshe madaktari wanne, tayari amesharudi hivi sasa na tumempa wiki mbili za mapumziko *(Makofi)*.

Vile vile tunaye Dk. Marijani *Physiologist*, Dk. Takdir *Pediatrision*, Dk. Mgongo *Gynecologist* wote wanarudi kesho kutwa, sasa wakirudi wakute nchi yenye zahma. Nadhani wakute nchi imetulia kama bahari iliyokuwa shuwari *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, leo Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi amezungumza mambo makubwa sana hapa kwamba alisema ninakujengeeni bandari kubwa tena ya kisasa Mpigaduri, jambo dogo hilo. *(Kicheko/Makofi)*.

Vile vile Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ameweka jiwe la msingi la Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) Tunguu ya aina ya pekee.

Pia Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi tayari ameshatandika umeme Pemba tena tunataka nini. Kwa hivyo, kilichobakia ni kutulia na kujenga nchi yetu na huyu amefika hapa na yule anakwenda pale, basi utaona jinsi Zanzibar itakavyokua kidogo kidogo.

Mhe. Spika, ukifanyakazi na Mhe. Rais Amani Abeid Karume, maana kila wakati anakwambia tulia utafika kidogo kidogo tu, ndivyo anavyotuambia Mhe. Rais wetu wa Zanzibar.
Mhe. Spika, baada ya hayo ninayo mengi lakini nawachia wenzangu waendeleze, isipokuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja *(Makofi)*.

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Spika, na mimi kama kawaida ya wenzangu nikushukuru kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia mswada huu. Kwa hivyo, mimi sitosema mengi kwa sababu tayari wameshayazungumza mengi wenzangu.

Kwanza napenda kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi kwa kutuletea sheria hii katika kutekeleza maagizo ya maamuzi ya Baraza yaliyopita.

Kwa hiyo, naunga mkono mswada huu kwa asilimia moja kwamba mswada huu tuupitishe kwa ajili ya kutekeleza au kusogeza gurudumu la maendeleo la Zanzibar *(Makofi)*.

Mhe. Spika, mimi ninayo bahati kwamba nimekuja Barazani wakati historia ya utendaji wa Baraza na inshaallah utendaji wa serikali unabadilika na mimi nikiwa ni sehemu ya maamuzi ya mabadiliko hayo. Mwenyezi Mungu atubariki tuendelee kusikilizana, kuelewana pamoja na kufahamiana.

Katika Baraza lililopita wakati nilipokuwa nikichangia hoja ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary nilitumia nafasi ya kumnukuu mzee wangu Nelson Mandela ambaye ninampenda sana katika masuala haya na kusema, kwamba wale watu ambao wamehasimiana kwa sababu moja au nyengine kikubwa ni kufika mahala wakazinduka na kusema ala! Tunakwenda wapi?

Mhe. Spika, watu wamekuwa wakitoa mifano ya nyumba hapa, lakini hata ndoa iko hivyo. Kwa kweli si vizuri kusema hivi karibuni nilikuwa na swahibu wangu mmoja alikuwa na matatizo na familia yake. Sasa kasema kwa ajili ya kutoa zile hasira, basi nilimwambia bosi nimeshakusikia inawezakana ikawa kuna makosa na huyo mwenzako, lakini unamjua atakayekuja yuko vipi, maana huyu tayari umeshamjua.

Sasa sisi tumeshafamiana kwa mfano, ukimuuliza Babu Haji Kheir, Juma Duni kisiasa yuko vipi, basi anaweza kuchukua muda mwingi, lakini na mimi Haji Kheir ni Mtumbatu mwenzangu tena akianguka hapa basi wa kwanza nambieni mimi, lakini tukitofautiana sana pengine na hasira pamoja na hasama. Mhe. Spika, pengine hata kama ningeumia angesema ndio *(Kicheko)*.

Lakini ukiuliza sababu nini? Eti ni tofauti ya mawazo. Kwa kweli yeye mawazo yake ni tofauti na yangu basi. Mhe. Spika, hata siku moja haiwezekana sote tuwe na mawazo sawa.

Kwa hivyo, tutaendelea kutofautiana Mhe. Spika na wala haiwezekani kabisa kwamba mara zote tutakubaliana. Isipokuwa mara zote tukitofautiana basi

tuulizane, kwamba tumemaliza mjadala je hili lina faida kwa sote au kwako wewe na mimi tu. Kwa maana hiyo, lazima tufike mahala kwamba lile lenye faida kwa Zanzibar ndilo lenye faida kwa kila mmoja wetu na hayo ndiyo maneno niliyoyasema wakati wa hoja.

Mhe. Spika, Wazungu wa Afrika ya Kusini mwanzo walikuwa wanaamini kwamba lile linalofaida kwa Wazungu ndilo lenye faida kwa Waafrika. Sasa wale Waafrika wa Kusini walisema sisi ndio wengi na lenye faida na sisi ndio lazima liwe hilo. Kwa hiyo, walifika mahala na kusema ala! Kumbe sivyo, lenye faida kwa sote ndilo lenye faida kwa kila mmoja wetu.

Katika shughuli zetu hizi tutaambizana mara nyengine tutakosea maneno, wakati mwengine tutajibizana sivyo, lakini kuna kitu kinaitwa ustahamilivu wa kukubali tofauti hizo.

Kwa bahati nzuri Mhe. Spika sote tufahamu hivyo, maisha Zanzibar yamebadilika, nikimuiga Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii alisema tulivuu kama mgongo wa ngisi, yaani imebaki baridi. Kwa mfano, siku hizi hapa tumekaa na kutaniana kama mara ile nilivyosema hakuna mwenye pembe na sote tuko sawa tena ni wa moja, tunajadili hivi sasa sheria tatu, nne na tumebishana na tunafika mahala na kusema hoja imekubaliwa na sote kwa umoja wetu tunasema ndio *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi atakuwa shahidi, hebu afikirie wakati ule wa CUF na CCM miezi mitatu ambayo hakuna umeme angepata usingizi kwa kishindo cha Babu Duni. Lakini miezi mitatu imepita na tulikuwa tukiambiwa kwamba Babu Duni umekwisha wewe, nilikuwa nikiwaambia maridhiano na umoja ni muhimu. *(Makofi)*.

Kwa sababu tumeyaona matatizo ya umeme na tumeyastahamilia na kukaa gizani, lakini mwisho limepata jibu kwa kuwa ni letu sote na wala si la Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi wala Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Amani Abeid Karume, isipokuwa ni la Wazanzibar na tumelifahamu *(Makofi)*.

Sasa huko tunakokwenda Mhe. Spika matumaini yangu mimi ni hayo tena naona fahari hata kama leo Mwenyezi Mungu anasema ana-*switch off* ile *engine* yangu, basi watu watasema kwamba naye alianza kushiriki katika kujenga Zanzibar mpya.

Mhe. Spika, muda wote kilichokuwa kinanisumbua kwenye siasa hiki kibaki kuwa kumbukumbu, kwamba kwa nini tofauti ya mawazo yangu iwe ndio kutiwa adabu, yaani kwa nini nitiwe adabu kwa sababu mawazo yangu ni tofauti hicho kilikuwa kikinisumbua.

Sasa jambo la msingi Mhe. Spika ni kwamba huko tunakokwenda tujue kuwa sote tunayo haki pamoja na wajibu. Katika masuala ya utawala kuna mambo yanayoitwa *collective responsibility*.

Dhamana ya pamoja ninapokuwa ninaieleza kwa watu ambao ninawafundisha, basi huwaambia usipate tabu kuijua dhamana ya pamoja, hebu jione unapokuwa huna meno hapa usoni tu unasema sawa.

Kwa mfano, badala ya kusema *Assalam Allaykum*, utasema *Ssallam Allaykum*, kwa sababu ya kupungua meno mawili tu, labda ukichukue kipande cha nyama na kukiweka, basi utabugunya badala ya kukata na yamepungua meno mawili tu. Kwa hivyo, mwili wa binadamu sehemu yoyote ikiumwa basi mwili unaumwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ananiangalia anajua akina-Ronaldo wachezaji wa Timu ya Brazil Mhe. Ali Suleiman Ali ndiyo anayoipenda. Wachezaji wale 11 wakati wanapoingia uwanjani Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, basi wale wanasema sisi ni 11, Robert Carlos ni halfback lakini utamkuja yuko chini ya goli la Ujerumani anataka kufunga, ukipigwa mpira kutoka timu ya Ujerumani unamkuta chini ya goli la Brazil anakinga.

Mhe. Spika, wakati nilipofungwa goli na hata kama amefunga Ronaldo, basi imefunga Brazil na inapofungwa Brazil hata kama mlinda mlango ameukwepa kwa sababu shoti nzito, basi imefungwa Brazil. Kwa sababu wote 11 ni sehemu ya mchezo wenyewe na mimi namsifu sana aliyebuni mchezo wa mpira, kwamba wakicheza 11 basi hutaki kwenda kwa mganga kama unauweza utafunga tu *(Kicheko/Makofi)*.

Kwa hivyo, na sisi Wazanzibar tujue kwamba tunao wajibu wa pamoja hata kama mmoja ataona ni peke yake, basi yeye ni sehemu ya sote *(Makofi)*.

Mhe. Spika, ninachotaka kumalizia na kutoa mchango katika hili huko tunakokwenda, tunayo Katiba ambayo ndio muongozo wetu. Lakini Katiba hii ni maandishi, yaani ni kumbukumbu ukitaka kurudia na utekelezaji wa Katiba hii uko kwenye nafsi ya wale waliopewa wajibu kusimamia. Tunapisha sheria hii ambayo mambo yake ni mengi, tutaisahihisha, tutaweka sawa lile ambalo haliko sahihi.
Lakini kama mtu anataka kutuvuruga basi atatuvuruga kwa hii, kwa sababu atafanya anavyotaka kwa ajili ya kukwepa dhamana ya pamoja. Kwa kweli sitegemei kwamba hilo huko tunakokwenda litatokea. Isipokuwa ninaamini kwamba sote tunao wajibu na tunahitaji kutekeleza wajibu wetu.

Mhe. Spika, sheria hii imetupa nafasi kujidhatiti kwamba sasa tunaposema hili hatulitaki, basi hatutakuwa peke yetu watu 75 humu, lakini tunaweza kwenda kwa wenyewe na kutuambia hilo fanyeni na hili msifanye. Katiba hii ilivyoandikwa imesema kwa kuwa sisi wananchi, yaani sisi tunafanya kwa niaba.

Mhe. Spika, wenzangu wamelizungumza sana suala la baadhi ya wananchi kukosa kuandikishwa. Nadhani kunahitaji kufanywa juhudi wale waliokosa haki bila ya sababu za msingi nao waandikwe. Wenzangu wametoa mifano hapa mimi nilikuwa nataka kutoa mfano mmoja. Nina kaka yangu nitamtaja jina kama ananisikia wala asifikirie kama nimemtaja kwa vibaya. Kaka yangu huyu ambaye amenilea anaitwa Juma Moh'd Juma ni kaka yangu wa Baba mmoja.

Mimi huyu amenilea mpaka nimemaliza kusoma, huyu alikwenda kujiandikisha Mhe. Haji Omar Kheir anajua masuala ya Watumbatu kuhusu vyeti vya kuzaliwa. Alikwenda kwa Sheha na wakati huyo Sheha ni mtoto wa dada yetu, alimwambia Sheha nimekuja kuchukua barua niende nikajiandikishe.

Mhe. Spika, Sheha akamuuliza cheti cha kuzaliwa kiko wapi, kaka yangu huyo kidogo ana kigugumizi, basi ile hasira yake maneno yakamganda, juzi alikuwa ananihadithia badala ya kucheka alimwambia yule Sheha mama yako anayo. Yaani anamshangaa kwamba yule mama yake ni mdogo kuliko yeye, wakati yeye amezaliwa anamuona anamuuliza cheti cha kuzaliwa. Mhe. Spika, basi hajaandikwa mpaka leo kwa kuwa hana cheti cha kuzaliwa, mtu wa miaka 70. Nadhani haya yanahitaji kuzingatiwa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nina mambo mawili tu kwenye sheria hii. Kuna kifungu Nam. 3 (1) naomba kusahihisha kitu kidogo tu na naomba niisome hiyo sentensi ili aione Mhe. Waziri. "Rais kwa kutoa amri ya maandishi na kuchapishwa katika gazeti rasmi la serikali ataamrisha tume kufanya kura ya maoni ili kupata mawazo, naomba neno mawazo halistahiki kuwepo hapa, kwa sababu huku kifungu cha 1 mlisahihisha kwamba kura ya maoni maana yake ni utaratibu wa kupeleka suala au hoja kwa wapiga kura ili watoe uamuzi. Mhe. Spika, kama watoe uamuzi tena hapa haiwezi kuwa mawazo. Hicho naomba kisahihishwe.

Mhe. Spika, jambo la pili nililotaka kutoa mchango kwenye sheria hii ni kifungu Nam. 12 (2) kinasema maombi chini ya kijifungu hiki cha 1 cha kifungu hiki yatakuwa kwenye mfumo kama utakavyoelezwa na Jaji Mkuu na yatawasilishwa Mahakamani ndani ya siku 30 baada ya kutangazwa matokeo

ya kura ya maoni. Yaani kwa yule mtu ambaye anataka kuyapinga basi amepewa siku 30. Mawazo yangu mimi binafsi ni kwamba siku 30 ni kidogo mno, ukusanye asilimia 10 kwenye Mikoa yote kwa siku 30 shughuli kama hii unaweza ukamalizika mwezi tu kwanza uko nusu safari. Kwa hivyo, ningeshauri tu kwamba angalau ingekuwa siku 60.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kukupongeza tena wewe kwa kuniruhusu na kunistahamilia kusema yale yaliyokuwa si ya kawaida. Mhe. Spika, naunga mkono sheria hii asilimia mia juu ya mia. Nakushuru sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana kupata wasaa huu kuweza kusema mawili matatu kuhusiana na mswada wetu huu muhimu sana katika mustakbali wa nchi yetu, Mswada unaohusu Sheria ya Kuweka Masharti ya Kura ya Maoni na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kama ulivyosema mengi mazuri yameshazungumzwa na mimi nimpongeze sana na kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi kwa maelezo yake ya ufasaha kabisa alipozungumza kuhusu mswada huu. Vile vile namshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, nafikiri kama walivyotangulia waheshimiwa wengine kwamba yeye alikwishatandika misingi yote, kwa hiyo sisi tena tupige chapuzo kidogo kidogo hapa na pale.

Mhe. Spika, mswada ulioko mbele yetu una lengo kubwa la umoja wetu wa kitaifa na tumepata fursa ya aina yake wananchi wa Zanzibar ya kupata kuja kupiga kura ya maoni. Nafikiri hiyo ni demokrasia kubwa sana kwamba unaulizwa unataka vipi, nchi yetu iende vipi.

Mhe. Spika, hili ni suala muhimu sana tukilinganisha huko tulikotoka maamuzi mengine yalivyokuwa tunayachukua, lakini leo tunapiga kura hii kwa masuala ya msingi na kuulizwa wananchi. Kwa hivyo, mimi nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu na niipongeze serikali yetu kwa kuamua kwa makusudi kuleta suala hili.

Mhe. Spika, mtu atakayekataa akasema kwamba kura ya maoni isipigwe sijui ana mtizamo upi na kinachofurahisha nikinukuu kwenye kifungu cha 3 kinasema. “Amri ya kufanyika kura ya maoni chini ya kifungu cha 1 cha kifungu hiki (a) itahamisha suala au hoja itakayopelekwa kwa wapiga kura katika kura ya maoni kwa namna suala litakavyojibika kuwa ndiyo au hapana”.

Mhe. Spika, lakini kwa mtizamo wetu na mustakabali wetu na tunakoelekea kama nilivyosema waheshimiwa wengi wamezungumza sekta ya elimu mafanikio yake, sekta ya afya na naamini na mimi nikijimwaga sekta ya fedha maana yake naamini mimi ndiye baba wa yote haya. Lakini mimi sitokwenda huko narudi pale pale kwamba kufanikiwa kote haya ni masuala ya umoja, mshikamano na kusikilizana. Hilo ndilo suala la msingi kabisa. Nafikiri yote haya yamejenga kwamba tunaiweka Zanzibar mbele, ubinafsi baadae.

Mhe. Spika, mimi huwa mtundu sana wa kutafuta tafuta vitabu na kuvisoma. Jana nilikwenda kuhangaika nikapata kitabu kimoja ametunga huyu Bwana Pevis Musharaf Rais wa Pakistan. Nafikiri sote tunamjua ujamadari na ukakamavu wa bwana Musharaf na vipi alivyoipeleka Pakistan. Mhe. Spika, haidhuru huyu ana matatizo yake lakini ni vipi alivyosimama kidete kuitetea Pakistan. Mimi nimevutika sana kwenye alivyo-*dedicate* hiki kitabu chake na naomba ninukuu kidogo:-

"I dedicate this book to the people of Pakistan those who toil sacrifice and pray for their country and wait patiently for a better future. They deserve a committed, selfless leadership which can help them realize the aboundless potential".

Mhe. Spika, tunaelekea wapi hili ndio suala la msingi kabisa, mwenzetu Mpakistani huyu ameona mifarakano aliyonayo sitaki kuzungumza madhambi yake, nataka nizungumze mema na alhamdullillah amejitahidi kuipeleka Pakistan pahala pazuri. Mhe. Spika, leo viongozi wetu wawili wamesema wamekutana tarehe 5 ile wakasema jamani, tulipofika tumefika yanatosha tena tusafiane nia na wakaombana radhi kwa niaba yetu.

Mhe. Spika, haitowezekana tungekutanishwa sote labda wajumbe wa CUF na wajumbe wa CCM lakini hawa ndio viongozi wetu na tumewaamini sisi. Kwa hivyo, mazumgumzo yale wameyazungumza kwa mustakabal wa nchi yetu. Leo kuna watu wanazungumza wanasema maridhiano yale ni ya Maalim Seif na Dk. Karume. Mhe. Spika, wale ni viongozi wetu na tumewaamini tukawatuma katufanyieni yale na baadae wakarudi wakaripoti kwetu. Maalim Seif alifanya mkutano mkubwa kabisa na Mhe. Karume akafanya mkutano mkubwa kabisa wote wakaripoti makubaliano yote. Kwa hivyo, wanayoyabeza nafikiri hao hawatutakii mema nchi hii na nafikiri kuna kila haja ya kuwapiga vita kabisa.

Mhe. Spika, mimi wananchi wa Dimani naamini na wengine wote naunga mkono kama alivyosema Mhe. Zakiya Omar Juma asilimia mia moja lazima tufike mahala tujiulize. Mhe. Spika, wenzangu wengi wameyazungumza na ukiyasikiliza maneno yale yanatonesha.

Mhe. Spika, jana tumeanza na daftari kwa upande wa Wadi yangu ya Tomondo, basi nilikwenda kule kukagua hali. Mhe. Spika, ni kwamba wengi wanajitokeza sasa hivi ni wanachama wa chama cha CUF kwa sababu wakati ule nafikiri kulikuwa na amri kwamba wasijitokeze, basi safari hii wamejitokeza na wanakwenda vizuri na kila mmoja anadai haki yake na haki yao wanapewa kwa mujibu wa yule anayestahiki. Kwa hivyo, huu ni mfano mzuri kabisa kuna baadhi ya waheshimiwa walidai kwamba haki wapewe wajiandikishe, mimi nina amini kwamba haki kila anayestahiki anapewa. Mhe. Spika, mfano mzuri ni Tomondo kule lazima nikubali kwamba wadi ile mimi nimezungukwa na wapinzani lakini kwa uchaguzi Mhe. Haji nitakushinda tu.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 6 wa mswada wetu anaelezea kwamba mtu hatotakiwa kueleza jinsi alivyopiga. Mhe. Spika, hili ni suala la msingi kabisa kwamba hili ni suala la siri na heshima itakuwepo na mimi nipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuamua kazi hii kuiachia Tume ya Uchaguzi. Kwa sababu tume tumeiamini kwa mambo yetu ya uchaguzi hapa Zanzibar, kuna wajumbe pale wa pande zote mbili. Kuna wajumbe kutoka upinzani na kuna wajumbe kutoka chama tawala.

Mhe. Spika, naamini kwamba kazi hii kupewa tume kwa kweli tumefanya *home work* yetu vizuri kabisa. Kwa sababu vyenginevyo labda kila upande ungesema mimi sikubaliani na tume hii au sikubaliani na waliochaguliwa kufanya kazi hii. Lakini wamepewa kazi watu ambao tumewaamini na hivi sasa wako kwenye mchakato mzuri kabisa kujiendeleza katika kufanikisha hili suala.

Mhe. Spika, tunajua kwamba kulikuwa na miafaka mingapi iliyotangulia, lakini hiyo ilikuwa na *foreign component* kubwa sana niseme kama tumesuluhishwa. Mhe. Spika, mwenendo wa safari hii ni kwamba hatukusuluhishwa, wenyewe tumesema hebu tukaeni chini tutafakari tatizo ni nini. Nafikiri Mhe. Haroun alisema hata mke mkizozana wakija watu unamwambia taratibu basi muafaka unakuja wakiondoka pale pale mnaanza kuripuka. Nafikiri Mhe. Spika, sisi hatutokwenda huko, sisi nataka tuwe kigezo tuwaoneshe watu kwamba tulikuwa na tofauti zetu, lakini wote tulilenga maendeleo ya nchi hii na kila mmoja alikuwa na njia yake. Kwa hivyo, sasa hivi njia yetu tunaiweka pamoja, naamini Mhe. Spika kwa msimamo huo kila mtu atatuheshimu na ninaamini hivi sasa wameshatuheshimu.

Mhe. Spika, bahati nzuri nafanya kazi zangu Ikulu, Mabalozi mara nyingi wanapokutana na Mhe. Rais huwa ninakuwepo. Mhe. Spika, ni kwamba maneno wanayozungumza ni mazito sana wanasema leo mmefikia hapa hongereni jamani, sisi hatuamini kwa mlivyokuwa nyinyi, lakini mmekaa

mkatafakari na mmeona mnamfanyia nani haya. Mhe. Spika, mimi ninawapongeza sana viongozi wetu na haya waliyoyazungumza wenzangu ni kwamba hayo maendeleo ambao hawa waliokuwa wakitusaidia yangekwenda wapi au tungefikia wapi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nafikiri hili ni suala la msingi na mimi naungana na wenzangu waliosema tutoe taaluma kwa watu wetu ili wafahamu hasa wapi tunaelekea na nini lengo letu. Mhe. Spika, haidhuru tuna imani zetu za chama lakini hizo imani kwa mfano upande wetu wa Chama cha Mapinduzi kinasema umoja, mshikamano, upendo kati yetu ni suala la msingi. Mhe. Spika, hayo ni kwamba bado tunaendeleza.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mimi nilikuwa nataka nizungumze machache tu kuunga mkono sana. Kwa hivyo, nilipokuwa nazungumza kwamba Jimbo la Dimani nasimama pale pale na Mhe. Hamad na Mhe. Abubakar Khamis Bakary asilete mtu, kuna watani wangu wameniletea kikaratasi wananiambia, mzee je sasa Urais basi.

Mhe. Spika, sijawa na nia hiyo lakini kama Mhe. Spika, unaniona nnafaa basi, unaniona nnafaa. Mhe. Spika, naunga mkono hoja asilimia mia juu ya mia. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na nitamshukuru kama vile anavyoshukuriwa kawaida *alhamdulilah rabilaalamin wassalatu wassalamu alaa Rasulillahi Muhammad Salallahu Alayhi wasallam wa radhiallahu taala an ashabi Rasulullahi ajmaiyn Rabbishrahli swadri wayassirli ammri wahluluqdata minlisaani yafqahu qauli amma baadu.*

Mhe. Spika, nimeanza na maneno haya kwa sababu tunazungumzia kitu maalum, kitu ambacho muda mrefu sana kilikuwa kinahitajika lakini ama kweli kama tulivyoambiwa kila kitu kina siku na saa.

Kwa hivyo, siku na saa ya hili lilikuwa halijafika leo ni mwanzo wa kufika siku na saa ya utekelezaji wa jambo hili. Kwa sababu tunaloliandaa hapa tunaandaa mustakabal wa nchi hakuna haja ya kutonesha madonda. Lakini Mhe. Spika, nina hakika unakumbuka na ukifumba macho unaweza ukaiona picha halisi ya Baraza lako lilivyokuwa mwaka 1995 mpaka 2000. Mimi sijasahau Mhe. Spika, nina hakika na wewe pia utakuwa hujasahau.
Mhe. Spika, yote yale lazima tufike pahala iwe ni historia na litakalotupeleka mpaka tukafikisha kuwa yale yalikuwa ni historia ni kwenda katika mustakabal mpya, mustakabal ambao utatuongoza katika lile Mwenyezi Mungu analolipenda. Kwa sababu Mwenyezi Mungu anasema *audhubilahi mina*

shayttaan rajim waataswimu bihablillahi jamiyan walaa tafarraqu, unganeni na wala msifarikiane, muungane kwa kamba ya Mwenyezi Mungu.

Kwa hivyo, hili tunalolifanya sasa Mwenyezi Mungu akilijaaalia akalitia roho likahuika basi tutakuwa tumetekeleza amri hiyo ya Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu kauli yake hayendi kinyume.

Pia Mwenyezi Mungu kasema na kwa kuwa kauli yake hayendi kinyume Mwenyezi Mungu kasema *Innallaha laa yughayyiru maa biqawmin hattaa yughayyiru maa bianfusihim*. Hakika ya Mwenyezi Mungu habadilishi chochote ndani ya kundi la watu mpaka wao wenyewe wabadilishe. Mhe. Spika, hapa tupo katika kubadilisha mwendo uliopita na kwenda mwendo mpya. Kwa kuwa kauli ya Mwenyezi Mungu hairudi nina hakika tukijaaliwa huko mbele kutakuwa kuzuri.

Mhe. Spika, sisi Baraza lako hili kwa umoja wetu ndio tulioikubali hoja binafsi iliyoletwa hapa inayohusiana na suala hili tunalolijadili leo. Katika kuchangia hoja ile kuna mambo mbali mbali tuliyoyazungumza, lakini mwisho tuliiagiza serikali ibadilishe hoja ituletee sheria ili iwe ni mwanzo wa utekelezaji wa hoja ile ambao sisi ndio wenyewe Baraza hili. Naishukuru sana serikali kuwa ililisikiliza Baraza la Wawakilishi na ikachukua ile hoja na ikaandaa sheria ambayo leo ndio tunayoichangia kwa ajili ya maslahi ya mustakabal wa nchi yetu hii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kuwa sisi ndio tuliopitisha hoja hiyo basi sisi ndio tunaostahiki kuilinda hoja hiyo. Kwa hivyo, sheria hii ni sheria yetu na kwa kuwa ni sheria yetu basi tunapaswa kuichangia vizuri na hatimae kuipitisha na badala ya hapo kusimamia utekelezaji wake ulio mzuri. Mhe. Spika, kwa sababu sote hapa tulikubaliana kwamba jamani kuwa katika umoja ni jambo zuri na kwa sababu tumekubaliana kuwa katika umoja basi sote tukausimamie huo umoja uje.

Kwa kweli litakuwa jambo kidogo la kuchekesha au la kinyume cha utaratibu kuwa umepitisha jambo wewe mwenyewe halafu urudi uende ukalipinge. Mhe. Spika, sidhani kama yupo atakayefanya hivyo naamini kabisa *mia fil mia,* kuwa sote humu ndani tutakaporudi kwa wale waliotuleta hapa basi tutawafahamisha vizuri umuhimu wa umoja katika nchi hii, ili watakapotoa maoni yao, watakapotoa uamuzi wao basi wajue wafanye nini.

Mhe. Spika, kuna wananchi wengi huwa wananiuliza dhana yao ya kura ya maoni wanadhani itakuwa kama ile maoni ya vyama vingi na chama kimoja, kuwa tutaitishwa kwenye mikutano ya hadhara waulizwe pale na watu wazungumze ikisha iandikwe, hiyo ndio dhana ya baadhi ya watu ilivyo kwa

sababu ni kwamba hawajapata kuiona kura ya maoni. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nadhani kuna haja kubwa sana yetu sisi Wawakilishi kutoa taaluma kabla ya hiyo tume haijatoa taaluma. Mhe. Spika, tukianza kutoa taaluma vizuri basi tume kazi yake itakujakuwa ni nyepesi na ndogo. Kwa hivyo, hili Mhe. Spika, nadhani nalo ni moja ya miongoni mwa mambo muhimu ambayo yanafaa yafanywe.

Mhe. Spika, nani hasa asiyeitaka raha hii tuliyonayo hivi sasa. Mimi juzi kwa kweli nilifurahi Mhe. Ali Juma Shamuhuna alitoka kifua mbele baada ya kumnyanyulia mkono mswada upite, nani haitaki raha hii? Hakuna tena ile ya kuwa wanaokubali. Mhe. Spika, kwa hivyo Baraza sasa hivi limekuwa lina raha ya aina yake kutokana na michango inavyotolewa, kutokana na michango inavyopokelewa na kutokana na michango inavyofanyiwa kazi. Kwa sababu kila kitu kinakwenda kwa mujibu kinavyotolewa

Kwa hivyo Mhe. Spika, hili mimi naliona ni jambo zuri na wananchi wa Jimbo la Mkoani hili wanalikubali na kila siku napigiwa simu kuulizwa mswada huu utajadiliwa lini? Sasa jana niliwapigia simu nikawaambia mswada utaanza kujadiliwa kesho tukijaaliwa. Najua nikirudi tu, nitapigiwa simu nyingi kuulizwa vipi mambo huko? Lakuwajibu nalijua.

Lakini Mhe. Spika, kutokana na kauli ile niliyoisoma ya Mwenyezi Mungu ya kuwa habadilishi kitu isipokuwa watu wabadilishe wenyewe. Mimi nina hakika tukibadilisha na kwa sababu tumeshakuwa na nia ya kubadilisha, kama tutabadilisha nina hakika kuwa mchemba ulioko huko chini basi tutautoa juu. Mchemba utakujazake juu Mhe. Spika, visiwa vitabadilika, mchemba wa mafuta.

Mhe. Spika, mchemba huo tukiuleta juu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kutokana na kubadilika sisi wenyewe, basi hapo ndipo tujetuone mambo, kilimo kitakuwa na baraka, tutalima kilimo cha umwagiliaji kwa sababu tutakuwa uwezo tunao.

Mhe. Spika, mapungufu ya maradhi yatakuwepo kwa sababu hospitali Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii atakuwa na uwezo wa kuleta mambo mbali mbali ya kutukinga na kututibu, lakini si hilo tu Mhe. Spika, tutakuwa na uwezo wa kuwavua samaki tulioanao kwa sababu tutakuwa na uwezo wa kuleta meli kubwa za kuvulia.

Ustawi wa jamii yetu Mhe. Spika, utakuwa mzuri tena mzuri sana na hapo ndipo tutakapokaa tukajilaumu kwa nini tumechelewa? Lakini bora uchelewe lakini ufike. Kwa hivyo, kuchelewa kwetu bado hakujawa kubaya kwa sababu ile niliyosema ilikuwa siku na saa haijafika. Sasa hivi siku na saa imefika

Mwenyezi Mungu anataka kutukwamua hapa tulipokwama kwa muda mrefu kwa mizozo iliyokuwa haileti faida kwa mtu yeyote kati yetu.

Mhe. Spika, labda kidogo niingie kwenye mswada kwa sababu kuna mambo nahitaji, sijui kama ufafanuzi hivi au nina mapendekezo. Kwanza katika kifungu cha 8, Haki ya Kupiga Kura ya Maoni.

> Kifungu cha 8 "Mtu yeyote wakati wa kura ya maoni atakuwa ameandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura atakuwa na haki ya kupiga kura katika kura ya maoni".

Hapa nilikuwa nina jambo moja dogo nataka niliseme.

Daftari linaandikwa hivi sasa lakini kwa bahati mbaya wanaoandikwa ndani ya daftari hivi sasa ni wale ambao umri wao hivi sasa umeshafikia miaka 18, lakini kuna wengine ambao siku ya kupiga kura umri wao utakuwa umeshafikia au umeshapita miaka 18 watakuwa hawamo katika daftari. Hawa tumeshawanyima fursa hii ya kuweza kupiga kura hii ya maoni.

Sasa pendekezo langu kuwa katika huo uandikishaji basi ilikuwa cheti kiangaliwe mtu atakayekuwa siku ile ya kupiga kura tayari ameshafika miaka 18 basi aandikwe kabisa tu ili ikifika siku ile apige kura yake kama wanavyofanya wenzetu hapo jirani.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kifungu cha 9(1), naomba kunukuu.

> Kifungu cha 9(1) "Katika kura ya maoni, upigaji kura utakuwa wa siri kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Uchaguzi kwa kutumia kisanduku kimoja cha kupiga kura kwenye kila kituo cha kupigia kura".

Sikufahamu kisanduku cha kupigia kura kimekusudiwa nini, kile kituturi ndio kisanduku cha kupigia kura, kile kisanduku kinachotiwa kura, hapa sikufahamu naomba nije nifahamishwe. Kwa sababu kisanduku ninavyofahamu mimi hakiwezi kupigiwa kura, kinaweza kutiwa kura. Sasa hapa nina wasi wasi nije nifahamishwe kidogo.

Lakini Mhe. Spika, katika kifungu hicho hicho cha 9(3) ambacho kimeandikwa, "kwa masharti ya sheria hii, tume inaweza kumruhusu mtu yeyote kama ambavyo itaona inafaa, kuwepo kwenye vituo vya kupigia kura kwa kipindi chote cha upigaji kura, kuhesabu kura na kutangazwa kwa matokeo

ya kura". Hapa nataka niungane na Waziri Kivuli kuwa hawa watu isingekuwa watu wowote, ingelikuwa watu maalum wakajulikana pengine mtu fulani, mtu wa aina hii au hii wakawa wapo pale, kuliko kuiachia tume kuwa ichague mtu yeyote wanayetaka wenyewe tu, nafikiri lisingekuwa jambo la busara sana.

Mhe. Spika, nikija katika ukurasa wa 6 katika kifungu cha 17, kifungu hiki kimefanyiwa marekebisho na kamati na marekebisho yake naomba niyasome.

Kifungu 17(2) "Tume ya Uchaguzi inaweza, kwa kutoa tangazo katika Gazeti la Serikali, kutumia sehemu yoyote ya Sheria ya Uchaguzi au kanuni zake kwa ajili ya shughuli za kura ya maoni kwa kadri ya vile ambavyo Tume itaona inafaa kwa ajili hiyo".

Nililokuwa katika marekebisho haya sijalifahamu Gazeti la Serikali imekusudiwa nini? Gazeti Rasmi au Zanzibar Leo? *(Kicheko).*

Mhe. Spika, katika mswada huu hayo ndio niliyoyaona kidogo nahitaji ufafanuzi. Kwa sababu wengi wetu wameshazungumza habari hii kwa urefu basi naomba tu nimalizie kwa kusema namshukuru sana Mhe. Waziri aliyeleta mswada huu. Lakini pia naishukuru serikali kwa jumla ikiongozwa na Mhe. Rais kukubali mswada huu uletwe katika Baraza la Wawakilishi. Aidha, namshukuru Mwenyekiti wa Kamati iliyouangalia mswada huu na kamati yake nzima kwa kazi nzuri waliyoifanya wakaturahisishia sisi kutotoa makosa mengi. Naomba pia nimshukuru Waziri Kivuli wa wizara hii kwa maoni yetu aliyoyatoa haidhuru machache lakini yenye maana.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu na ukanivumilia kwa muda wote huo ahsante. Mhe. Spika, naomba radhi, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Ahsante Mhe. Spika. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na afya na uzima na kutujaalia kuwa siku ya leo kuwa kwetu ni siku adhimu. Mhe. Spika, nadhani nisingelipenda kusimama kwa sababu mswada huu tangu asubuhi umeshajadiliwa vizuri na hamna kitu kilichobakia. Lakini wakati nimeshaleta maombi yangu imenibidi na mimi kama mwanamke nisimame nitoe mchango wangu katika mswada huu. Imenifanya nisimame kama mimi mwanamke kwa sababu matatizo mengi yanayotokea yanatukuta sisi wanawake.

Kwanza nianze kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi kwa uwasilishaji wake mzuri na ningeliomba nimpe lile jina tulilopewa Kenya Mhe. Saitoti. *(Makofi).*

Mhe. Spika, pia niwashukuru wajumbe waliochangia toka asubuhi katika mswada huu, inaonesha kwamba nia na dhamira zetu zote ziko katika lengo moja. Mhe. Spika, mwanadamu ana siku mbili katika maisha yake ambazo ni siku nzito. Siku ya kwanza ni siku ambayo ya kufunga ndoa, siku ule mwanadamu anakuwa ana siku nzito kwake. Siku ya pili ni siku ambayo mwanadamu anatiwa katika mwanandani, siku ile ni siku mzito kwake.

Mhe. Spika, namaanisha kwamba na sisi Wajumbe wako wa Baraza lako tukufu kuanzia usiku wa leo hadi kesho tuna siku nzito kwetu, kwa maana tuko katika mjadala wa kuleta mustakabali wa nchi yetu. Kwa hivyo, wananchi wote wanasikiliza kuna nini Baraza la Wawakilishi, kuna kauli gani na ndio maana nikasema tuko katika siku nzito.

Mswada huu ni mswada ambao utatupeleka katika njia nzuri, njia iliyonyooka. Kwa sababu Mwenyezi Mungu siku ya Jumatatu hadi Jumatatu basi wanadamu hufutiwa madhambi. Lakini anasema isipokuwa wale waliofarikiana. Tujitizame huko nyuma tulikotoka mifarakano iliyotokea, kwa hivyo, katika watu walioko katika hali ngumu na mimi mmoja nilikuwa niko katika hali ngumu kwa kuona kwamba tuko kwenye ibada siku zote lakini ikifika siku ya Jumatatu Mwenyezi Mungu anasema siku ile tuzipandishe ibada za waja na siku za kufutiwa madhambi yao.

Kwa hivyo, ipo haja ya kuona tumegomboka, ipo haja ya kuona hivi sasa ndio maana nyoyo ya kila mmoja imejaa furaha. Imani yangu mswada huu tutaupitisha wala hatuufanyii mzaha ili kutarajia yale yote yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Mawaziri,

Mhe. Waziri wa Fedha kazungumza maneno mazuri sana kwamba tusiwape nafasi wale wanaopiga vita. Mimi nasema tusiwape nafasi hata kidogo tukaja tukarejea kule tulikotoka na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatusaidia kwa hili.

Mhe. Spika, kwa kweli hata ile nyumba ikiwa ina mifarakano Mwenyezi Mungu pia haitii baraka sikwambii nchi, nyumba ikiwa na ugomvi au migogoro siku zote mwisho baba atakwambia ndio maana nikienda kazini sipati kitu kwa wewe ugomvi wako ndani ya nyumba. Kweli, kwa sababu hakipiti chochote nyinyi mmo ndani ya ugomvi tu. Leo tumedhihirishiwa hapa jinsi tulivyo na sisi wenyewe tunaona.

Kuna usemi mmoja Waarabu wanasema, “Alfarua atbaghul-asli”. Kwa hivyo, yale matawi yanafuata shina. Sasa viongozi tukikaa sawa kila kitu na walio chini yetu basi na wao wanatusikiliza sisi tumekaa vipi na tumejipanga vipi na wao wanafuata mkondo ule ule, hatutoharibikiwa na kitu chochote. Kwa hivyo,

hapa tulipofika mimi naomba tuikamate kamba hii hii tuzidi kwenda mbele ili tufanikiwe na maendeleo yaingie katika nchi yetu.

Mhe. Spika, ombi langu katika mswada huu, nadhani yale yote nilisema kwamba mengi yameshapatiwa ufafanuzi na mengi yamerejeshwa katika marekebisho. Ninadhani sisi tusimame tutie baraka tu katika mswada huu lakini mengi yameshazungumzwa.

Ombi langu Mhe. Spika, kama walivyosema wenzangu taaluma hiki ni kitu muhimu kwa sababu mimi nafsi yangu sijapatapo hata siku moja kuwahi hiki kitu kinachoitwa kura ya maoni. Kwa hivyo, ikiwa mimi kiongozi bado niko hapa sijawahi kuona kura ya maoni nina imani na wananchi wengi hili suala la kura ya maoni hawalijui. Kwa hivyo, taaluma itolewe kwa wananchi kwa uwazi kabisa hususan kwa akinamama. Nawaomba akinamama wenzangu tuliokuweko katika Baraza hili tuchukue jitihada ya kukaa na akinamama wenzetu kuwaelimisha juu ya suala hili.

Mhe. Spika, maana ya kusema hivyo akinamama ndio walimu wakubwa na akinamama ndio wenye kufikisha ujumbe haraka haraka kuliko akinababa.

Mhe. Spika, nirudi pale alipozungumzia Mhe. Haji Omar Kheir. Mhe. Spika, nikwambie ukweli wakati alipokuwa akizungumza Mhe. Haji mimi machozi yalikuwa yakinitoka, nasema ukweli machozi yalinitoka. Mhe. Spika, hii mifarakano iliyokuwepo kwa muda mrefu sisi kijijini kwetu Binguni tulikuwa na Maulid ya Mfunguo Sita basi kila mmoja alikuwa akisoma yake na si kama sote tunapenda iwe vile, Wallahi hatupendi hata kidogo lakini Maulid ya mwaka huu yamesomwa kwa vihoi hoi.

Kwa bahati nzuri siku ya Maulid nilikuwa katika kamati Dar es Salaam, lakini siku niliyoondoka nikapewa taarifa ile na nikaipokea vizuri, nilichojaaliwa nikawasilisha vizuri na wananchi wakaenda. Niliporudi nikapewa salamu kwa hivyo, hiyo ni moja katika faraja.

Mhe. Spika, siku moja nilimuuliza mwalimu wangu nikamwambia hebu nipe siri ya elimu. Akanambia siri ya elimu inapotokea jambo ambalo halipendezi lolote wakati una elimu wewe basi litakukera tu katika nafsi na iko siku utarudi. Mhe. Spika, Wawakilishi kwa nia iliyopo hapa kwa pamoja ndio maana leo tunaunga mkono na Mhe. Rais wa Zanzibar Mhe. Amani Abeid Karume nasema kwamba na yeye anayo elimu pamoja na Maalim Seif Sharrif Hamad, wamekaa pamoja ile elimu imekaa ili kuona yale matatizo ya nyuma wakayarekebisha na sisi leo tuko hapa tunajadili mswada huu wa sheria ili kuona mafanikio yetu tunayatatua.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi tuupitishe mswada huu kwa vihoi hoi ili tupate faida ndani yake na faida hii itakuwa tunaacha historia kwa vizazi vyetu. Kama walivyosema wenzangu mtu yeyote akishafariki anatajwa kwa jema lake. Nina imani na sisi tutakuja kutajwa kwa wema wetu huu tulioufanya, kuacha hali ya nchi kuwa katika utulivu.

Tulikuwa na wenzetu Waheshimiwa ambao Mwenyezi Mungu keshawapeleka mbela ya haki na wao walitamani leo wawepo waungane na sisi katika masuala haya. Lakini nina imani Mwenyezi Mungu atajaalia kwa hili tunalolifanya basi zile fadhila zake na wao watazipata. Kwani inakuwa *"famantwabakan fahuwa minhu",* mwenye kufuata kundi na yeye yumo. Kwa sababu na wao tayari wangekuwemo katika kuchangia haya, lakini wenzetu wametangulia na sisi tunayoyafanya tunaacha kama kumbukumbu tuje tutajwe.

Mhe. Spika, mimi nadhani nione kifungu kimoja tu kwenye mswada naomba nipatiwe ufafanuzi. Kama nilivyosema mengi yameshazungumzwa lakini nije ukurasa wa 7 kifungu nambari 19(f), baada ya yale marekebisho sasa itakuwa (f), ilikuwa (j) lakini sasa ni (f).

Mhe. Spika, kifungu kinasema kwamba, "kupiga kura kwa watu walioajiriwa kwa shughuli za kura ya maoni wakati wa upigaji wa kura". Ningeliomba Mhe. Waziri anipatie ufafanuzi kipengele hiki, labda kwa akili zangu kidogo fupi sijakifahamu vizuri. Naomba nipatiwe ufafanuzi ili nipate ufahamu mzuri katika sehemu hii.

Mhe. Spika, nadhani katika kuzungukazunguka mswada mzuri, mswada umeshazungumza yote hakuna kilichobakia, isipokuwa tutoe nasaha zetu tu kama nilivyosema kuwa elimu ni muhimu wananchi wapatiwe, na sisi tutajitahidi kwa kadri ya ufahamu wetu tutakuwa walimu kwa hili, hatutoliacha tutajitahidi kama alivyosema Mhe. Mohamed Ali Salim tutarudi majimboni, mawilayani ili kwenda kuwapa elimu wananchi wetu mpaka itakapokuja tume wawe tayari wameshafahamu.

Mhe. Spika, naomba kusema kwamba hoja hii na mimi naiunga mkono pamoja na wanawake wote wa Zanzibar. Nina imani hakuna mwanamke hata mmoja atakayelichukia hili kwa sababu haya mambo yote ya matokeo mazito yakitokea yanatugusa sisi wanawake. Kwa hivyo, wanawake wote tunaliunga mkono hili kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Mohamed Ali Salim Mulla alisema kitu hapa ilikuwa kama vile kaniuliza mimi kama ninakumbuka mwaka 1995. Niseme katika watu waliofarajika mno kuliko nyote ni mimi ambaye naendesha mikutano hii nikilinganisha na kule alikoniuliza Mhe. Mulla kama nakumbuka.

Nakumbuka vizuri na jinsi nilivyokuwa siipendi hali ile nakumbuka tarehe 23 Novemba, 1996 kwa siku nne mfululizo nilikwenda kuzungumza na waheshimiwa wangu kutoka Pemba, walikuwa wakali kweli. Wakaniuliza wewe umetumwa na nani? Mhe. Said Ali Mbarouk pia anakumbuka, kuja kuzungumza na sisi ili tufanye kazi kwa pamoja. Majibu yangu ilikuwa nafsi yangu ndio ilinituma hayo. Sasa ndoto yangu ilikuwa ndio hii tuliyonayo.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuweza kutia sehemu ya ubani katika chetezo hiki kilichopo mbele yetu.

Kabla ya kuzungumza Mhe. Spika, hiki nilichokusudia kuzungumza basi na mimi niseme kwamba hayo uliyomalizia kuzungumza na sisi tulikuwa mashahidi ni kweli wala hujasema uongo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie hiyo hali ambayo unayo iendelee na izidi *Inshaallah*.

Mhe. Spika, awali ya mchango wangu napenda nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu (*S.W*), kwani kwa uwezo wake ndio leo tunazungumza haya kwa fahari kubwa. Aidha, nikubaliane na wenzangu wote waliotangulia hususan kuanzia Mhe. Waziri mwenyewe, Mwenyekiti wa Kamati pamoja na kamati yake, Waziri Kivuli pamoja na Wajumbe wote ambao tayari wameshatangulia kuchangia kwa kweli hakuna walichokiacha.

Kama isingekuwa hamu ya kila mmoja kwamba anataka kuzungumza basi ingekuwa tumeshapiga makofi sasa hivi tushakwenda zetu kwamba mswada umekwishamaliza zamani. Kwa kweli mswada ni mfupi na pengine kama nilivyosema ingelikuwa sasa hivi tuko nyumbani kwa kusubiri kuja kufanya jengine kesho Mwenyezi Mungu akitufikisha kutokana na hali halisi ya mswada wenyewe ulivyo. Lakini kwa sababu ya umuhimu, thamani ya mswada huu inashinda almasi. Kama tunavyojua sote almasi kijino kidogo lakini mapesa utakayotajiwa unaweza ukaona kama si kweli lakini ndio hali halisi.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu vile vile ni kwamba wakati umefika, na kufika kwa wakati suala la kura ya maoni kama mwenzangu aliyekaa kitako na mimi sijawahi kuiona, lakini mimi bahati nzuri nimeshasikia. Niliisikia katika hali ambayo ilikuwa ya vuguvugu, kama sikosei mwishoni mwa miaka ya 80, kati ya mwaka 1989/90/91, haya maneno yanayosema kura ya maoni yalikuwa yakivuma sana.

Wakati ule mimi nilikuwa na akili zangu nzuri ingawa sikuwa mwanasiasa, lakini nilikuwa nikifanya kazi katika afisi pale Maruhubi hili neno halikuwa geni sana. Mara tukasikia kwamba kuna suala zima la kutoa maoni ya vyama

vingi. Sasa pale palikuwa na vuguvugu kubwa sana la watu kutaka kura ya maoni ingawa halikuwa official, lakini ni jambo ambalo lilikuwepo.

Sasa pamoja na kuvuma kule basi halikuweza kufanikiwa kuwepo kwa sababu wakati wake ulikuwa haujafika. Pengine ni juzi tu mwaka jana, mwaka juzi lilikuwepo hili likining'inia lakini likawa halikupata nafasi kwa sababu hizo hizo kwamba wakati wake ulikuwa bado. Sasa leo tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba suala hili liko mbele yetu kwa baraka kubwa kabisa za wananchi wa visiwa hivi wakiongozwa na viongozi wetu wakuu wakiwa ni Mhe. Rais Amani Abeid Karume na Mhe. Seif Shariff Hamad kupitia maridhiano.

Mhe. Spika, neno maridhiano linaweza likawa jepesi sana kwa kulisema, lakini kama utakaa utalitafakari basi ni sawa sawa na msingi wa nyumba na sio hizi nyumba za kutupia vidongo, lakini ni misingi ile ya *concrete* wanayoiita jamvi.

Mhe. Spika, kwa upande wa Zanzibar tukitoka kwenye maridhiano kupitia kura ya maoni ndio tunakwenda kule tunakoelekea kunakoitwa kujenga Zanzibar mpya. Kwa sababu kura ya maoni itakuwa na mambo mengi likiwemo hili ambalo tumelielekea mbele yetu la Serikali ya Umoja wa Kitaifa au wengine wanaita Serikali ya Mseto. Mhe. Spika, kila mtu ana tafsiri yake lakini lengo kwamba ni serikali ya pamoja ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, binafsi napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru sana viongozi wetu kwa ujasiri waliochukua, lakini pia na wananchi kwa ujumla kwamba tumeelewa tumefika pahala tumeona kwamba hili ni jambo lenye manufaa na maslahi kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, katika hili mimi nilikuwa na pendekezo. Kule Afrika ya Kusini na wao walipitia mazonge mazonge ya aina nyingi na wakafika pahala wakafikia kwenye maridhiano kama sisi ambavyo tumefikia. Wao katika hili wanaliadhimisha kila mwaka. Sasa kwa heshima ya mambo haya na mimi ningependekeza ikiwa itakuwa imekubalika basi na sisi tuwe na Siku ya Maridhiano ya Kitaifa, iwe kila mwaka tunaadhimisha, iwe ni msingi wa kutukumbusha kwamba hii ndio njia ya kupita.

Mhe. Spika, wenzetu wanaadhimisha kila tarehe 12, lakini nimejaribu ku-*search* kwenye *network* yangu kwa haraka nimeshindwa kupata ni mwezi gani kule Afrika ya Kusini. Lakini nadhani haina umuhimu sana kwangu mimi kuipata tarehe halisi na mwezi wake. Tarehe ni 12, sasa na sisi kwetu tuna tarehe 5 mwezi wa Novemba, kila mwaka ingeadhimishwa ingekuwa vizuri sana. Hata vizazi vyetu vitakapokuja wangeweza kupata mtiririko mzuri wa kihistoria watakapokuwa wanaelezwa siasa za vyama vingi mpaka kufikia

kwenye maendeleo hayo ambayo wakati huo sisi pengine tutakuwa hatupo. Hili lilikuwa ni ombi langu mahsusi kupitia mswada huu wa sheria ambao uko mbele yetu.

Mhe. Spika, sitaki nirejee mambo mengi ambayo wenzangu wameshayapitia na kuyasema sema sana naweza nikayatoa ladha kwa sababu kila jambo haidhuru ni hilo hilo, lakini kila mzungumzaji analizungumza kinamna yake. Sasa unaweza ukalizungumza wewe ukawa umeliweka vizuri zaidi au ukawa umeharibu kitu, mimi nachelea huko kuharibu. Kwa sababu hizo mchango wangu utaendelea kuwa ni mfupi sana.

Mhe. Spika, nikenda katika mswada huu sikusudii kufanya marekebisho ya aina yoyote lakini nilikuwa na mapendekezo hususan nikilenga katika kifungu cha 8 kama ambavyo Mhe. Waziri Kivuli na yeye alikigusia na kukitolea maelezo kama *paragraph* mbili tatu hivi. Mhe. Spika, labda kwa ruhusa yako nifanye kupitia kidogo ili niweze kuweka sawa kile ambacho nimekusudia kukisema.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri Kivuli katika *paragraph* ya nne anasema kwamba "Kifungu cha 8 kinaelezea wazi kuwa mtu yeyote ambaye wakati wa kura ya maoni atakuwa ameandikishwa katika daftari la kupiga kura, basi atakuwa na uwezo wa kupiga kura ya maoni.

Mhe. Spika, hili ni jambo zuri na kwa kweli ndivyo inavyofanyika ulimwengu mzima, kila nchi huwa na daftari moja tu la wapiga kura, iwe kura ya maoni au kura ya uchaguzi wa kawaida. Lakini suala zima lililopo hapa ni suala la kura ya maoni ambayo kila Mzanzibari anatakiwa aeleze hisia yake kuhusu suala fulani ambalo pengine litakuwa liko katika mjadala huo unaohusiana na kupigwa kura hiyo ya maoni".

Sasa Mhe. Spika, tatizo kubwa lililoko hivi sasa ni kuwa vijana wengi sana ambao hawajasajiliwa kutokana na sababu mbali mbali na hiyo inaweza kupelekea wao kukosa hili suala zima la kupiga kura.

Mhe. Spika, kwa sababu katika nchi yetu tuna utaratibu wa kufanya uandikishaji wa daftari kila baada ya miaka mitano, huenda hili likawa ni miongoni mwa tatizo la baadhi ya wananchi wengine kuweza kukosa haki zao. Sasa mimi nilikuwa nadhani tungekuwa na mfumo kama ambao baadhi ya nchi duniani tena nchi zilizoendelea wanaofanya, nalo ni suala zima la kumuorodhesha kila mwananchi wa nchi hiyo pale tu anapozaliwa. Akizaliwa tu anaingia kwenye *register* yao na namba yake inakuwa ndio hiyo hiyo anayoitumia kwenye sehemu nyengine zote, ikiwa ni leseni, ikiwa ni mambo

mengine yoyote anayofanya basi ile namba yake aliyokuwa *registered* kwenye kuzaliwa ndio hiyo hiyo inakuwemo kwenye kitambulisho chake.

Mhe. Spika, hii ina faida nyingi, faida kubwa ya kwanza kwamba inapunguza gharama ambayo serikali zetu inaingia kwa kila miaka mitano kuhitaji mpaka kusaidiwa na wafadhili mbali mbali katika kuliandika tena upya daftari. Ni lazima iwe ni gharama kwa sababu kuna watu inabidi wakae waandike, watoke hapa waende huku, sasa haya yote yanakuwa yanaiingiza serikali katika gharama kubwa. Kwa hiyo, hili litakuwa halipo.

Lakini pia Mhe. Spika, hakutakuwa na suala zima la usumbufu kama ambao sasa hivi upo. Mtu umetimia umri lakini mara hujapata hiki, mara hujapata kile, mara fulani hakutambui. Haya yatakuwa hayapo kwa sababu maelezo yote yatakuwa tayari yameshawekwa.

Bahati nzuri sasa hivi sote tuko katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia tunatumia hizi *database* ambazo zitakuwa zinaonesha kila kitu. Umezaliwa inatoa pale maelekezo yako kama huyu ni Mzanzibari au ni mgeni yumo katika nchi na mambo kama hayo. Sasa yale yote yatakuwa yanatoa *particulars* zote ambazo zinahitajika.

Kwa maana hiyo, itakuwa hakuna suala hata la ku-*forge* kwamba huyu katimia, hakutimia, wewe mwenyewe kitambulisho chako kitakushtaki kwamba kinaonesha tarehe fulani ndio uliyozaliwa, namba yako na kila kitu chako kiko pale. Basi madhali una miaka 16 sidhani kama utakuwa na akili nzuri ya kusema unakwenda kuingia katika masuala ya kura ya maoni au kwenda kufanya uchaguzi wakati wewe bado umri haujatimia kwa mujibu wa katiba zetu.

Sasa hili niliona nijaribu kutoa kama maoni na ushauri kwa serikali kwamba tukienda na mfumo huu tunaweza tukaondosha matatizo mengi likiwemo la kutumia sana, kupoteza gharama nyingi za kila baada ya miaka mitano. Wakati mwengine zinapotokezea *by elections* au vitu vyengine hivyo hivyo vinasababisha kwamba tunatumia sana.

Lakini hata mambo haya ya usumbufu wa kumtazama mtu kwamba katimia au hakutimia, anastahiki au hastahiki, au kwenda kusema uongo kwamba umetimia umri lakini kumbe hujatimia, itakuwa hili linatatuka *automatically*. Sasa huu ulikuwa ni ushauri ambao niupendekeze kwa kupitia kifungu hiki cha 8 cha mswada wetu.

Mhe. Spika, jengine ni suala zima la Wazanzibari ambao wako nje. Kuna mjumbe wako mmoja hapa asubuhi alizungumza kuhusu suala hili. Akasema

kwamba wenye haki wanaweza kurudi nchini wakapiga kura ikiwa ni hiyo ya maoni au ni Uchaguzi Mkuu kwa mfano halafu ataondoka. Kwa hali ambayo pengine labda kaondoka tu kikazi au kimasomo kenda kule lakini yeye kwa kawaida ni mkaazi wetu hapa hakuondoka muda mrefu na sheria zinamruhusu.

Sasa mimi nilikuwa naulizia hivi wakati mtu ameondoka kwa shughuli za aina hiyo, kule aliko Balozi tunazo, haiwezi kutumiwa Balozi kwa ajili hii kama ambavyo wenzetu wanatumia. Tunashuhudia hapa watu wa Msumbiji wanavyopiga kura wakiwa Unguja hapa, hawajarudi Msumbiji hata siku moja. Mhe. Spika, hili nilikuwa napenda pia kuona kama linaweza kupata nafasi Mhe. Waziri akija atatufahamisha vizuri.

Mhe. Spika, pia niendelee kuzungumza kama wenzangu wengine hususan Mjumbe aliyekaa kitako umuhimu wa suala zima la kutoa elimu kwa wananchi wetu. Kwa kweli Mhe. Spika, binadamu ndio binadamu, lakini ni lazima kama viongozi tuwe wakweli, tuwe wakweli wa nafsi zetu mbele ya wenzetu, lakini tuwe wakweli wa nafsi zetu mbele ya Mwenyezi Mungu. Si vizuri leo miongoni mwetu hapa tukae tuzungumze lugha moja, kitu kimoja lakini usikie kama pengine mtu mwengine anasema maneno kinyume chake.
Kwa sababu tatizo inakuwa kwamba unaipotosha jamii.

Kwa maana hiyo, Mhe. Spika, nilikuwa napendelea sana kwamba suala hili la taaluma ni suala muhimu sana pamoja na sheria hii na Waziri mhusika. Lakini nadhani na Mhe. Waziri anayehusika na mambo ya Habari na yeye atakuwa na jukumu kwa upande wake kuona kwamba wananchi wetu wanapata taaluma ya kutosha kuhusiana na masuala haya muhimu ambayo pengine kwa upande mmoja bado ni mageni kama ilivyoelezwa.

Kwa sababu wengine wanafikiri labda wataitwa mkutano wa hadhara, wengine wanaona yatapita makaratasi wajaze, kila mtu na ufahamu wake. Kwa hiyo, suala zima la kutoa elimu muafaka, sahihi, basi bado ni kitu muhimu sana katika masuala yote haya yanayohusiana na maendeleo ya nchi yetu kupitia suala hili la kura ya maoni.

Mhe. Spika, kama wengine walivyotangulia kuelezea, kwanza tushukuru sana hili suala lipo na litakuwa ndani ya sheria, ndani ya katiba ya nchi yetu. Ni jambo ambalo litaweza kutupeleka mbele haraka haraka, ni jambo ambalo litaweza kuisimamisha katiba kama ambavyo inajieleza kwamba wananchi wenyewe ndio wanaoiendesha nchi yao.

Viongozi wanafanya wanayoyafanya kwa matakwa ya wananchi kutimiza matakwa yao. Sasa wanapokuwa wao wana shida ya jambo tukenda tukawauliza kwa mujibu wa katiba, kwa mujibu wa sheria basi ni jambo moja

muhimu sana na ni jambo ambalo litatupelekea kupata maendeleo ya haraka na yenye ridhaa ya watu.

Mhe. Spika, zamani mimi mdogo sijawahi hata siku moja kuhudhuria lakini nikisikia kwamba kulikuwa na mambo ya ujenzi wa taifa. Sidhani kama leo hapa tunyanyuke tu tuseme kuna ujenzi wa taifa hivi hivi tu watu wakaitika mwito huo. Ma-*block* yale pale yamejengwa katika *style* hiyo.

Sasa Mhe. Spika, kimefika kipindi kirefu cha watu kwamba hawaoni kama wao wanawajibika kwa hili na lile kwa sababu wanaona kila linalofanywa wakubwa wameamua. Lakini tutakapokuwa tunafanya yale ambayo wao wameyaamua basi nadhani kila jambo litakuwa jepesi, si kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, si kwa Waheshimiwa Mawaziri, lakini hata kwa viongozi wakubwa. Kwa hiyo, Mhe. Spika, suala zima linalohusiana na taaluma kwa wananchi kuhusiana na suala hili ni muhimu sana. Ningependa kila ambaye anahusika kwa nafasi yake aweze kuitumia vizuri ili tuweze kupata mafanikio.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache na mimi nilitaka tu angalau niseme chochote katika mswada huu. Naunga mkono mswada huu mia fil mia kama Mhe. Waziri Kivuli wangu, hayupo sasa hivi lakini atakuwa ananisikia huko.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipatia nafasi hii kuchangia mswada huu wa Kuweka Masharti ya Kura ya Maoni.

Mhe. Spika, kabla ya yote niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataala kwa kutujaalia kuujadili warka huu muhimu sana na wa kihistoria katika nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kupongeza hatua zote zilizochukuliwa katika ngazi mbali mbali hadi kufikia leo kuwasilishwa na kujadiliwa katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kama alivyomaliza Mhe. Zakiya Omar Juma hapa kwamba kwa kweli na mimi nilikuwa nijadili mengi sana, lakini Waheshimiwa Wajumbe wenzangu waliotangulia wamemaliza kila kitu. Lakini kutokana na umuhimu wake na mimi nimeona kwamba angalau basi japo kidogo niseme machache. Kwa hiyo, mchango wangu zaidi utakuwa ushauri, kusisitiza baadhi ya vifungu au maeneo fulani fulani na hatimaye kuunga mkono hoja.
Mhe. Spika, kwanza kutokana na umuhimu wa suala hili kitaifa hatua za makusudi zichukuliwe na kwa haraka sana kwa kuwaelimisha kwanza wananchi. Hii nasisitiza tu kama wenzangu wengi sana takriban wote

wamesema suala la kuelimishwa wananchi, wafahamu hasa nini kusudio au nini hasa kura ya maoni.

Mhe. Spika, hili mimi natilia mkazo, kwa hivyo hatua zichukuliwe mara moja tu baada ya Mhe. Rais kusaini sheria hii na kuashiria, basi hatua zianze kuchukuliwa haraka.

Lakini vile vile kwa upande mwengine nao wahusika yaani maofisa mbali mbali wa Tume ya Uchaguzi ambao watahusika kusimamia utekelezaji wa sheria hii, basi na wao nafikiri ipo haja waweze kupata elimu vile vile ya kutosha pengine labda kwa njia ya semina, ili waweze kumudu majukumu yao ipasavyo.

Mhe. Spika, jengine ni suala la sheria kusimamiwa ipasavyo na vyombo vyote vinavyohusika, Mahakama, Tume ya Uchaguzi na wale wote ambao wana sifa kwa njia moja au nyengine kusimamia sheria hapa nchini, basi wahusike kusimamia sheria hizi ipasavyo na kwa maadili ya hali ya juu kabisa.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mimi sitokuwa na mengi isipokuwa tu nachukua nafasi hii kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni na wananchi wote wa Zanzibar kwa jumla. Baada ya kufahamishwa vizuri bila shaka waitumie sheria hii, waitumie haki yao vizuri ipasavyo ya kupiga kura ya maoni kwa uhuru kabisa bila ya kuingiliwa, ili watimize ile demokrasia iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni na wananchi wote kwa jumla naunga mkono hoja hii kwa maslahi na maendeleo ya taifa na wananchi wake kijamii, kiuchumi na kisiasa. Ahsante sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi baada ya magharibi hii kuchangia kidogo kuhusiana na mswada huu muhimu na wa historia kwa Zanzibar na kwa Tanzania.

Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai tukawa wazima na tukaweza kupata kauli ya kuzungumza. Pia nawashukuru viongozi wetu. Kwanza Mhe. Rais wa Zanzibar Mhe. Amani Abeid Karume kwa busara zake na uongozi wake kwa kukubali kuacha tofauti kushirikiana na Katibu Mkuu wa CUF Mhe. Seif Shariff Hamad, ili kujenga istilahi nzuri ya Zanzibar.

Mhe. Spika, pamoja na jitihada ya mwanzo, lakini pia natoa pongezi za pekee vile vile kwake yeye kwa kukubali kuliendeleza hili suala. Kwa sababu wazungu wanasema “The end justifies the means”. Yaani pale mwisho wa ile

safari ndio palipo na yale madhumuni yenyewe ya ile safari yenyewe nzima. Kwa hivyo, madhali ni jambo linakwenda katika kuhitimishwa, basi inaonesha kwamba tokea mwanzo nia nzuri ilikuwepo.

Mhe. Spika, mabadiliko yoyote duniani hayatokei bila ya kuwa na nia nzuri *(goodwill).* Kwa sababu kuna kitu mazoea na kuna kitu mabadiliko. Mabadiliko wakati mwingi yanapingana na mazoea na ndio maana hata katika uislamu kulipoletwa sheria za mabadiliko zilipewa muda kwa sababu ya kujenga ule uzoefu mpya katika mabadiliko yale.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa sababu sisi ni binadamu hatuna budi kuwa bado tunabakishwa na suala zima la mazoea. Lakini *inshaallah* siku zitakwenda na mazoea yale tuliyokuwanayo yataondoka na badala yake tutajenga jamii iliyokuwa na mustakbali mwema.

Mhe. Spika, suala la kuwapelekea wananchi kura ya maoni kuweza kueleza yale ambayo wao wanahisi ndio yenye maslahi nayo ni masuala muhimu katika kujenga demokrasia halisi ya uwakilishi. Kwa sababu moja katika vigezo vizuri vya demokrasia ni namna gani wananchi wanavyowakilisha fikra zao.

Sasa kuwa na Bunge au kama sisi Baraza la Wawakilishi ni sehemu moja ya wananchi wanapata kuwachagua viongozi wao moja kwa moja. Lakini suala la kuwapelekea kura ya maoni ni suala la kuwaingiza moja kwa moja waweze kutoa maoni yao kuhusiana na mambo ambayo yangewahusu kwa wakati ule. Kwa hiyo, Mhe. Spika, mimi moja kwa moja kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia.

Lakini Mhe. Spika, napenda nizungumze machache kuhusiana na tahadhari ambazo tungekwenda nazo. Mhe. Spika, si jambo ambalo lingependeza kuona kwamba kuna watu wanaanza kuwaambia vyengine wananchi kwamba labda kura hii ya maoni ni ya mtu fulani, au ni ya jambo fulani. Mhe. Spika, kama siku mbili mimi nimeshawahi kuzungumza katika Baraza hili nikitoa mfano wa nchi zenye jamii nyingi.

Mhe. Spika, ukitazama filamu za Marekani wenyewe wanaita *Hollywood*, hakuna mtu yeyote wanayemtaka wakamkosa katika jamii yao. Wakitaka katika filamu yao kumuingiza Mwarabu wanae, wakitaka kumuingiza Mchina wanae, wakitaka kumuingiza Muhispania wanae, wakitaka kumuingiza labda Mkorea wanae. Sasa ile inawafanya wawe na jamii ambayo kwa kila jambo ambalo wanalitaka liweze kuwanufaisha. Vitabu vingi vimeandika kwamba hata utaalam ambao wanao unatokana na *culture* hiyo. Wanajua kwamba Korea ni wazuri kwa fani fulani basi wanakwenda katika jamii ya Wakorea walioko

pale wanawachukua kwenye fani ile. Wanajua kwamba hawa Black Africans ni wazuri katika fani hii, kwa hivyo wanawachagua wanawachukua katika fani ile.

Sasa Mhe. Spika, sisi bahati nzuri jamii yetu ni *almost mono culture*, kwa maana tuna tofauti ndogo sana katika jamii yetu. Kwa sababu suala la kuoana ni suala kubwa sana lilitokezea katika jamii zetu kwa hivyo ilivyokuwa imetokezea *intermarriage* katika jamii zetu Pemba na kwa upande wa Tanzania Bara tunazungumzia Mafia na tunakwenda maili 200 mpaka kufikia mwisho.

Pia tuje tuzungumzie neno tunaloita maji ya ndani ya nchi. Maji ya nchi yaliopo katika eneo linalotanda kwa umbali wa maili 12 za bahari lililopimwa kwa alama ya mwisho inayofikiwa na maji wakati yanakupwa au yametoka. Kwa hivyo, tunapozungumza katika *map* yetu hapa tunakusudia maji ya nchi ni yale ambayo yanaanzia kuanzia ukanda wa kisiwa, kwa maana ya Mashariki katika mstari huu unaopita wote, hii ndio *base line* yetu. Tuna hesabu 12 *nautical miles* katika mstari huu wa katikati, haya ndio maji yetu ya nchi au ndio *territorial water* yetu ambayo tumepewa au tumeingia katika makubaliano na sisi miongoni mwa nchi zilizokubali maamuzi yaliyopitishwa katika kusainiwa mkataba na *United Nation Convention Law of the Sea*.

Kwa hivyo, hiyo ni sehemu nyengine au ni pande la pili la bahari. *Depending Factors* zilizokuwepo katika EEZ, katika *territorial water* tukizungumzia kwa maana ya uvuvi, tunategemea zaidi *equatorial current* pamoja na lasagulhus , ndizo zinazoleta chimbuko la kusema kwamba maji yanapobiruka biruka, kwa hivyo yale masamaki yanaingia.

Mhe. Spika, lakini tunapokuja kuzungumza maji ya ndani, eneo la maji ya ndani masafa sawa kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Kwa upande wa Mashariki ya Zanzibar ni eneo la maji yaliopo katika alama za mwisho yanayofikiwa wakati maji yamejaa na yanapokupwa. Tuna maana gani? Tuna maana sasa tuna mstari huu wa *base line* ambao unatugawia *on the other side up ward* tunakwenda kwenye EEZ kwa maana ya *territorial water* EEZ. Lakini sasa tunapokuja kutoka hapa kuingia ndani, uoto upo uliokuwemo ndani, hii ndio *distance* tunayozungumza sisi kama ni maji ya ndani. Lakini ndani ya maji haya ya ndani kuna mgawanyiko ambao unasema mgawanyiko sawa, kuna *line* ambayo ni *invisible line*, inapita in between. Mgawanyiko huu unagawa maji baina ya visiwa vya Zanzibar, kwa maana ya kuwa maji ya Zanzibar na maji ya Tanzania Bara, unagawa katikati ya mpaka. Kwa hivyo, ukizuka upande huu ni maji yetu ya ndani na ukienda upande wa pili ni maji yao ya ndani au maji ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kwa maana Tanzania Bara.

Mhe. Spika, turudi tena kule kwenye *EEZ*, tunataka tuzungumze huu uvuvi, tunataka tuwafahamishe wajumbe tunakwenda kwenye utaratibu wa kufanya

maandalizi, maana Mhe. Mgeni Rasmi alivyosema utaratibu wa sheria mpya, kwa nini? Kwa sababu ndani ya hii *EEZ* katika mambo ya msingi yanayofanyika, moja ni la ukataji wa leseni, tutapata *revenue.* Katika leseni zetu tunazozikata, tuna *characters* mbili muhimu.

Tuna *industrial fisheries,* hiyo moja ambayo nitakuja kuielezea na tuna *semi industrial fisheries. Industrial fisheries* ndio ambayo ina-*operate* zaidi kwenye EEZ, hiyo ni meli ambayo ina uwezo wa kutoka ikaenda zake baharini ikakaa miezi sita, ina ma-freezer yake makubwa sana ya kuhifadhia samaki, ina *processing factory* mule mule ndani, kwa maana baharini baada ya samaki kuvuliwa akitiwa kwenye chombo kinachoitwa *industrial fisheries,* mpaka baada ya kile chombo kurudi kwake au kushusha bidhaa ile haijulikani tena kama ni mazao ya baharini, lakini yanajulikana kama ni *product* ambayo ni kamili na iliyokwishakuwa *processed*.

Kwa hivyo, meli itakapokwenda baharini ikaweza kuhifadhi, ikaweza kufanya usarifu wa samaki wale ndani ya meli, *by the way* wanashuka na maboksi tayari *well packed.* hiyo ndio *definition* tunaita sisi kama ni *industrial fisheries,* inamaliza kila kitu chake huko huko.

Lakini tunapokuja katika maji ya mkondo wa katikati huu, ambayo tunasema maji ya nchi katika *territorial water.* Katika namna ambayo sasa hivi tuna-*operate* kwa kasi kubwa zaidi tunatumia meli ambazo hiki ni kigezo tu, lakini ni meli ambazo tunaziita kama ni *trolling inverses,* zile meli ambazo mara nyingi waheshimiwa kwa wale ambao wanasafiri sana kwa boti, wakifika Dar es Salaam huziona pale ufukweni ziko nyingi sana, zile ni *trolling ships* ambazo ni *semi industrial*.

Kwa hivyo, *territorial water* mara nyingi ina *–operate* na *semi industrial*. Nini *semi industrial. Semi industrial,* maana yake ni vyombo ambavyo vina uwezo wa kuhifadhi samaki, lakini havina utaratibu wa kufanya *processing* ndani yake. Kwa hivyo, wanakuwa na ma-*freezer* na ma-*chamber* wanajaribu kupita, wanavua na wakimaliza kuvua wanatia samaki wao kwenye ma-*freezer* wakirudi juu kwenye geti zao wanashusha zile bidhaa ile na kwenda kuwa *processed.*

Hizo ndio *definition* au *differences* tunaposema, *full industry* kwa maana *industrial fisheries* na *semi industrial fisheries.* Hayo ndio maeneo mawili makubwa ya sekta ya uvuvi na ndivyo ambavyo tunakwenda nayo.

Mhe. Spika, na katika maeneo hayo, wingi wa kitu ambacho kila siku kinavuliwa, aina ya samaki wanaovuliwa. Kwa hakika tunazungumzia ni jodari, na jodari kwa maana hasa ya samaki Kiswahili tunazungumzia jodari kama ni

samaki wa aina moja. Lakini kwa Kiingereza tunao wengi sana, tuna *blue turner*, tuna *yellow fine turner* na kuna wengine wengi katika *characters* kama hiyo. Kwa hivyo hiyo yote inaingia katika jodari. Lakini pia tuna sehewa, tuna ndowaro kwa wale ambao wanajua ndowaro, tuna papa hawa na tuna chewa wakubwa kabisa, hao ndio mara nyingi wanakamatwa katika meli hizi za *industrial* na hizi ambazo zinavua kwenye *semi industrial characters.*

Jengine ambalo linafanyika katika *semi industrial* na katika *industrial characters*, ni meli za aina mbili tu ambazo zinakuja nchini kwetu kuvua na ndizo ambazo ziko *worlld wide*, kwa sababu ya nini? Moja ya sababu ambazo amezungumza Mhe. Mgeni Rasmi za kiuchumi. Meli hizi aidha itakuwa na *character* ya kuwa ni meli ya *long liner*, meli ya *long liner* unaifahamu moja kwa moja, kwa sababu inakuwa haina utaratibu wa kuvuta nyavu, hakuna milingoti mirefu ambayo inakuwa inavuta nyavu kama hizo nyengine. Hii ni *long liner person* ambayo inavua kwa mshipi.

Wanachofanya ni kwamba wanachukua mshipi mmoja mrefu sana, tokea hapa unakwenda zake pengine mpaka Fumba, wanautia *hooks* tofauti tofauti na ndowana, halafu wanaulaza katika utaratibu wa X *and* Y, wanakuja zao mpaka unafikia pahala wanauweka wanauwacha na baada ya muda kama saa 4 au 5 au wakati mwengine wanaacha kwa siku moja au mbili, wakati mwengine wanaacha kwa muda wa wiki wanapita na wanaanza kunyanyua ile *long liner* yao na ndivyo wanavyovua masamaki hayo makubwa kwenye maeneo hayo ya EEZ au kwenye maeneo ya *territorial water.*

Mhe. Spika, lakini ukija kuzungumza katika meli hizi ambazo tunaziita meli zinazotumia uvuvi wa nyavu. Hawa ni wavuvi ambao wanakwenda baharini kuvua kwa maana ya kwamba wanaburura, wanakokota na wanapokokota kwa sababu tunazungumzia kina kile cha maji tunachokizungumza, hakuna nyavu itakayokwenda chini kule mpaka kufikia kwenye kina, kwa sababu hiyo nyavu itakayokuwa kwenye meli ni kubwa sana na kama kuna meli itakayoweza kubeba nyavu hiyo kutokana na uzito wake, hiyo meli yenyewe pengine inaweza ikazama.

Maana yake tunapozungumzia mita 7000 *deep* katika *Indian ocean* sio masihara. Lakini hizi ni nyavu za kawaida ambazo zinavua samaki wanaojulikana kwa jina *pelagic* na ndio wengi wao hawa tuliokuwa tumewaeleza hapa au samaki wanaojulikana kwa jina la *maygretoripata*, wale wanaosafiri na kuhama hama.

Kwa hivyo, hizi meli za nyavu kawaida zinavua kwa maana ya siku hizi sayansi na teknolojia imekua, wanakuwa na vyombo ndani ya meli zao, *equipment* ambazo zinaonesha kama ni rada, wanawasha wanawaona wale

samaki waliokuwepo chini ya bahari wana-*set* mtego wao katika utaratibu kama ni wa duara au kama ni wa *sea*, halafu linapita kama ni gunia linasomba wale samaki kwa wakati mmoja na wanamaliza kazi ile.

Vile vile wanaweza kuvua *visual* kwa sababu wanapokuwa baharini mara nyingi ndege ni alama kubwa ya kuonesha kwamba pale pana samaki, kwa hivyo wanafuata wale ndege na wana-*set* mtego wao na wanavua kwa mara moja. Kwa hivyo, uvuvi huu ni uvuvi ambao unakwenda *maximum 3 hours* huwezi ukapindukia hapo, kwamba wanakwenda wanavua wanamaliza wanapandisha hadithi imekwisha, tofauti na *long liner*. *Long liner* wanakwenda pole pole sana unaweza ukakaa wiki baharini anasubiri kupandisha mtego wake juu pole pole ili aweze kuvua.

Mhe. Spika, ni nani mwenye kujua wakati unapotokea mfarakano kwamba yeye atasalimika. Naweza kusema kwamba hakuna mwananchi hata mmoja katika nchi yoyote ambaye anayeweza kutoa *guarantee* kwamba ukija mfarakano mimi nitasalimika na nitakuwa simo kwenye matatizo haya tena nitakuwa katika hali ya salama.

Sasa kama kuna njia ya kuondoa mfarakano ili usiwepo na wala usitoke kwenye nchi yetu basi njia hiyo tuipite *(Makofi)*.

Mhe. Spika, wenzetu wa Afrika ya Kusini wamekuwa na mfarakano mkubwa sana wa kikabila pamoja na mambo mengine mbali mbali. Kwa sababu Afrika ya Kusini ni nchi iliyopata uhuru katika taratibu za kikawaida za kupata uhuru, lakini wenyewe ni wanamapinduzi, maana waliingia msituni mpaka baadaye wakarudi pale wakaingia kwenye masuala ya muafaka na kukubaliana na kuingia katika uchaguzi.

Kwa kweli wanao utaratibu wa kuondoa mfarakano katika nchi yao, lakini utaratibu ule haukuvivunja vyama vya siasa. Kwa hivyo, vyama vya siasa vimeendelea kuwepo, pia utaratibu ule haukuvunja uchaguzi wa kila kipindi cha uchaguzi lazima ufanywe, yaani wakati wa uchaguzi unapofika basi lazima ufanywe katika nchi ile, vyama vinashinda na watu wanapitana kwa kura na mambo mbali mbali.

Pamoja na kuwa na utaratibu kwamba tukifika hatua fulani, basi anayeshinda ataunda serikali yake peke yake, hatua fulani itabidi tuungane na tufanye Serikali ya Umoja wa Kitaifa na makubaliano hayo wanayo wenyewe, tena yanakwenda vizuri na wala hakijafa chama chochote cha siasa.
Mhe. Spika, ninahakika Chama cha Mapinduzi katika Tanzania hakitakufa kwa kuwepo utaratibu huu hapa. Isipokuwa najua kitaimarika sana na wala sio

mchezo. Lakini jambo geni unapoliingia kuna matatizo yake, kama vile kujenga wasi wasi hata kujifundisha baskeli.

Kwa mfano, wewe mwenyewe utakuwa na hamu ya kujifundisha baskeli, lakini ukiona unakwenda kukaa juu ya baskeli wasi wasi unakuwa mkubwa sana, unatetemeka na matatizo mengine, baadaye unaijua ile baskeli ambayo itakusaidia kwa kazi zako, kama vile kuachia mikono, kuganda pamoja na mambo mengine mbali mbali kwa sababu umeshaizoea *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, tupigeni Kura ya Maoni na tufanye maamuzi na tukiangukia kuingia kwenye utaratibu huo tutazoea na kuachia dede na chama kitaimarika. Hayo ndiyo mawazo yangu, kwa sababu nina hakika chama kitaimarika na wala hakuna wasi wasi wowote, tena amani itapatikana pamoja na mshikamano utakuwepo na mambo yatakwenda vizuri kabisa *(Makofi)*.

Kura ya Maoni itapigwa kwa uhuru, yaani itakuwa huru kabisa na kila mtu atafanya maamuzi yake anavyotaka, ndio maana kikawekwa kifungu kinachoeleza kwamba hutotakiwa kueleza umepiga kura ile vipi, kwa kweli hii ni demokrasia ya hali ya juu sana. Isipokuwa kitu muhimu watu wetu tuwaeleweshe faida ya suala hili tunalotaka kulifanya na nina hakika wataelewa.

Wakati fulani Mhe. Spika nilikuwa Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Rais, wakati ule kulikuwa na utaratibu wa *devaluation*, yaani kupunguza thamani ya pesa. Kwa sababu siku zile shilingi ikipunguza thamani inatangazwa na wala halikuwa dogo hilo na lilikuwa kubwa sana. Kwa kweli Chama cha Mapinduzi kikalazimika kuunda tume maalum kutembea Tanzania nzima, kwa ajili ya kuzungumzia suala la *devaluation* na watu walifika mahala na kulifahamu.

Mhe. Spika, leo kila mtu anafahamu maana ya *devaluation* na hivi sasa inatiririka wenyewe wala haitangazwi. Isipokuwa watu wanatizama leo shilingi imepanda na kesho imeshuka na mambo yanakwenda vizuri na wala hakuna tena tufanye suala la nini au vipi kwa sababu wameshazoea *(Makofi)*.

Mhe. Spika, ni vyema tumuombe Mwenyekiti Mungu atupeleke katika jambo zuri ambalo lenye manufaa na sisi pamoja na nchi yetu kwa jumla. Kwa hivyo, hiyo ndio dua ya kuomba kwamba atupeleke kwenye jambo zuri lenye manufaa na sisi katika nchi yetu na Mwenyezi Mungu mkimuomba anakuleteeni la kheri na wala sio la shari, isipokuwa atatuletea jambo la kheri tena nina hakika tutakwenda vizuri kabisa.

Kwa maana hiyo, tuache wasi wasi juu ya masuala haya na tukubalini na ikibidi kubadilika, basi tubadilike twende katika mabadiliko na tuendeshe nchi yetu na

mabadiliko yoyote yatakayokuja yanakuja katika kheri na hiyo ndio hali halisi ilivyo *(Makofi)*.

Mhe. Spika, mswada huu wa Sheria ya Kura ya Maoni ni wa kudumu na Mhe. Waziri amesema wakati alipokuwa akiwasilisha hapa, hivi sasa tunampa nafasi Mhe. Rais anayekuwa kwenye madaraka anapotingwa na jambo ama apokee azimio au akiona suala hili lipo sana hapa, bora niwatake wananchi wafanya Kura ya Maoni, basi litamsaidia katika kumrahisishia uongozi, yaani kumuondoshea matatizo kwenye uongozi *(Makofi)*.

Kwa sababu atakuwa anayo nafasi atakapoona maneno yameshakuwa mengi. Kwa mfano, sisi hapa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukatoa maneno, basi anaweza kusema ah! Mbona maneno yamekuwa mengi hebu nikawaulize wananchi, sheria hii inampa uwezo moja kwa moja kuwauliza wananchi na kuagiza Tume ya Uchaguzi kwa ajili ya kufanya Kura ya Maoni. Suala hilo litakuwa ni zuri kabisa.

Kwa kweli hizo ndizo sababu ambazo mimi naunga mkono mswada huu. Vile vile nawaomba wenzangu tuunge mkono Mswada huu wa Sheria ya Kura ya Maoni tuwe nao na tuwatake wananchi wetu wapige Kura ya Maoni. Kwa sababu sheria hii imesema wazi kwamba matokeo ni *binding* takavyokuja ndivyo tayakavyotekelezwa na wala hatuna sababu ya kuwa na wasi wasi na hii ni sheria ikesha kuwa sheria inabidi itekelezwe hivyo *(Makofi)*.

Mhe. Spika, wenzangu wamesema mengi sana na mimi nimeona niseme hilo. Lakini nasema tuchagueni lenye manufaa na mambo haya tena ya kukimbilia mwituni au mashimoni yaondoke. Kwa hivyo, tuishi hapa katika nchi yetu na tustarehe na lile wazo la Zanzibar Njema Atakaye Aje, iwe ni njema kweli wakati huo na kila mwenye kutaka aje *(Makofi)*.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii pia niwashukuru wazungumzaji wote walionitangulia. Kwa kweli yaliyokwishazungumzwa tungesema yanatosha, lakini kwa umuhimu wa suala hili, basi kila mmoja akitia neno moja ndipo namna ambapo mswada huu utakuwa bora zaidi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, leo ni siku nyengine muhimu sana katika zama hizi za Demokrasia ya Vyama Vingi katika nchi yetu. Ni siku muhimu kwa sababu mihimili ya dola yote mitatu imetambua umuhimu wa maamuzi ya wananchi.
Baraza letu lilitoa azimio likaenda serikalini na serikali ikaleta mswada na wala haukuja moja kwa moja kutoka serikalini lazima umepita kwenye muhimili wa

sheria ya kuangaliwa, iwapo sheria hii iko safi kwa ajili ya kupelekwa Barazani kwa lengo la kujadiliwa.

Mhe. Spika, nikisema mihimili mitatu ya dola imefahamu umuhimu wa mwananchi katika kushirikia kwenye harakati za kiutawala na maendeleo ya nchi yetu.

Nadhaani tungekuwa na uwezo wa kumaliza masuala haya humu kama wakaida. Baadhi ya watu wengine nje walikuwa wanasema kwa nini mnarefusha muda namna hii kwa masuala ambayo yako wazi wazi na msipitishe tu mule na kusema jamani tumeshapitisha sheria hii ya kuwa na Serikali ya Pamoja, wako wenye maoni kama hayo huko nje. Kwa kweli wanaona hiki kitendo cha kuzungumza na halafu kwenda kwa wananchi kama kinapoteza muda.

Lakini hakipotezi muda, kwa sababu misingi ya kuwa na uamuzi wa umma katika nchi ni misingi madhubuti zaidi. Kwa kuwa demokrasia ya moja kwa moja mara nyingi ndio inayoambiwa bora na iliyomadhubuti zaidi kuliko hata ile ya uwakilishi.

Hii ni kweli kwa sababu wananchi hivi sasa wanapata ile fursa kwa suala hili pamoja na masuala mengine ya nchi. Kwa mfano, wakati mwengine sisi kama Wawakilishi tunaweza kuzungumza mazuri kwa kufikiria kuwa yanayo maslahi kwa nchi pamoja na wananchi kwa jumla, kumbe ikawa wananchi wenyewe sivyo wanavyoliangalia lile suala kama tunavyoliangalia sisi, isipokuwa Kura ya Maoni inawapa nguvu sasa.

Mhe. Spika, kuna msemo mmoja wa Kiswahili unaosema kwamba "Anayevumbua kijungu ndiye anayekuwa mpishi". Sisi ndani ya Baraza hili tumevumbua kijungu na lazima hivi sasa tusimame tupike *(Makofi).*

Kwa kweli suala hili litakapokwenda kwa wananchi basi ni jambo letu Wawakilishi sote na kama kutakuwa na mtu anafikiria kwamba ni la mtu fulani na mimi halinigusi, maana yake anajishtaki mwenyewe kwa wananchi. Kwa maana hiyo, Baraza letu halikuwa na maana na wala halikufanyakazi na wala hatuwezi kufika hapo tukajishtaki wenyewe kwa wananchi kusema kuwa sisi hatuna maamuzi mazuri.

Mhe. Spika, nadhani ni vyema tusimamie maamuzi yetu vizuri sana. Hii ni sababu nyengine baada ya ile sababu ambayo inatutaka sisi Wawakilishi na wananchi kuunga mkono juhudi za viongozi wetu wawili waliokaa pamoja na kulibuni suala hili na mpaka leo likawa jambo ambalo tunalijadili kwa ajili ya utekelezaji. Kwa hivyo, niseme kwamba tunajadili sheria hii na mwishoe

tutaipitisha. Lakini lazima tuwe na mashirikiano mengine ya kuisimamia kuona kwamba utekelezaji wake unakwenda vizuri.

Mhe. Spika, tafsiri ya Kura ya Maoni imetolewa hapa na waandishi, watafiti pamoja na wadadisi wengi wa masuala ya kisiasa wametoa tafsiri ambayo haipingani na tafsiri yetu ni nzuri kama tafsiri nyengine. Kwa hivyo, wamesema kwamba hii ndio demokrasia nzuri ambayo ni madhubuti zaidi.

Mhe. Spika, naomba nimnukuu mwanafalsafa mmoja anaitwa Dogdoner 1981 alisema hivi: "Maoni yoyote dhidi ya Kura ya Maoni anasema yeye ni maoni dhidi ya demokrasia". Maana yake utakapoipinga ile kura ya maoni, kwamba haina maana kwa sababu hawa wanatuchezea tu, basi Dogdoner ni maoni dhidi ya demokrasia. Sisi tumekaa hapa kwa ajili ya kuimarisha demokrasia *(Makofi)*.

Kwa hivyo, nadhani tunawajibika sana kuithamini, kuipa nguvu pamoja na kuisimamia Kura ya Maoni, ili ilete tafsiri halisi katika demokrasia yetu.

Mhe. Spika, mtu mwengine ni Butler and Runny katika mwaka 1994 wao waliitafsiri na kuichanganua na kusema "Demokrasia hii ya Kura ya Maoni, yaani *direct democracy* inaweza kuwa ni *prospective*". Kwa maana tunaweza kuanzisha sisi au Rais na Katiba yetu imetoa nguvu hizo.

Lakini wao wamekwenda zaidi na kusema demokrasia hii vile vile inaweza kuwa ni *citizen initiative*, yaani ikaanzishwa na wananchi wenyewe na nafikiria hapa sisi tunaanza. Nafikiri tutafika pahala wananchi wenyewe sasa bila hata ya kupitia hii mihimili ambayo tumeitaja leo, basi watakuwa wamepata nguvu ya kutekeleza Kura ya Maoni au ya kutusukuma sisi tutekeleze jambo ambalo wao wanaliona zuri na sisi humu bado tunaliona halijakaa vizuri.

Mhe. Spika, yapo masuala mengi ya aina kama hiyo, kwa mfano, mambo yanayohusu *moral issues* kama vile kutoa mimba, yaani mambo ambayo jamii inaweza kuona ni *immoral*, mara nyingi yanaanzia kwa wananchi, basi wananchi wakatoa kilio chao kwa serikali na serikali kuteleza kilio cha wananchi.

Kwa hiyo, wananchi wafahamu kwamba suala hili lililokuja ni muhimu sana, wala asitokezee mtu na kwenda kubabaisha kwa hali yoyote ile kwamba jambo hili ni kupoteza muda. Kwa kweli ni jambo ambalo lenye misingi madhubuti ya demokrasia *(Makofi)*.

Mhe. Spika, labda nitoe mifano kidogo ya nchi ambazo zimetumia.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, muda umekwisha nadhani ungesema maneno ya mwisho.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, ikiwa nitapata dakika tatu au 10 kwa ajili ya kumaliza basi nitashukuru sana *(Makofi)*.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nikuombe umalize maneno ya mwisho ya kufunga hotuba yako.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, kwa hivyo sitotoa mifano ya hizo nchi, lakini niende moja kwa moja kwenye vifungu vya mswada huu. Mhe. Spika, naunga mkono hoja *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nakushukuru sana pengine sikumtendea haki kama nilivyowatendea wengine, lakini muda ndio umetukwaza na maoni yameshatoka mengi.

Lakini kesho tukijaaliwa tutaendelea mjadala kidogo na baadaye tumuombe Mhe. Waziri afanya majumuisho juu ya mswada huu kipindi cha asubuhi na jioni nadhani Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira nitamwita.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 30/03/2010 saa 3:00 asubuhi)